CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

CKRC

VERBATIM REPORT OF

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MVITA CONSTITUENCY, HELD AT QUBAA ACADEMY**

**ON**

## TUESDAY 30TH APRIL 2002

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MVITA CONSTITUENCY, ON TUESDAY, 30TH APRIL 2002 HELD AT QUBAA ACADEMY

**Present**

1. Com. Pastor Zablon Ayonga
2. Com. Salome Muigai
3. Com. Paul M. Wambua

**Absent with Apologies**

1. Com. Prof. H. W. O. Okoth - Ogendo

**Secretariat in Attendance:**

1. Eunice Gichangi - Programme Officer
2. Phillip Mollo - Asst. P/Officer
3. Regina Obara - Verbatim Recorder
4. Milka Mahindu - Sign Language Interpreter

**The meeting started at 8.35 o'clock with Com. Pastor Zablon Ayonga in the Chair.**

Nachukua nafasi hii kwanza kuwashukuru nyote kwa kufika hapa asubuhi ya leo. Baridi baridi naona tuko nayo kidogo tumepata lakini tumejikakamua tukafika mapema. Tutaanza na maombi kutoka kwa mtu moja halafu tutaendelea.

**Prayer:** Inaudible.

**Com. Ayonga:** Asante sana kwa maombi. Namshukuru mungu ametupatia nafasi ingine siku ya leo ili tuanze kazi yetu ya kuchukua maoni. Nami, kwa niaba ya Commissioner mwenzangu Salome Muigai tunawakaribisha. Na tunatumaini zote tutashirikiana kwa kutoa maoni, si kutoa maswali, tunajua mmejitayarisha kwa kutoa maoni. Leo ni siku ya maongeshi yote yale ambayo mnataka kuona yamefanywe. Na pia nataka kila mmoja wenu apate nafasi ya kuongea. Na kwa hivyo, ili kila mmoja apate nafasi ya kuongea ninapo kuambia kwamba wakati wako umekwisha, tafadhali kubali ili kila mmoja apate nafasi kwa sababu wakati ni mdogo. Kwa hivyo kwa orodha ambayo nimeshika hapa, kuna wengine kati yenu mmekuja kuongea na pia wanamaandishi katika memorandum. Lakini ikiwa huna memorandum, utakayoyasema hiyo ndiyo tutachukua kama memoradum. Lakini pia katika hii memorandum yako pengine ungetaka uzifupishe sehemu fulani fulani ili uzimulike, ni vizuri, nitakupa nafasi ya kufanya hivyo. Na pia ikiwa unamaoni wewe kibinafsi pia tutayachukua. Sasa nadhani tuko tayari nanitamwita ndugu Abdulahi.

Huyo ni Abdulahi K. Ndunga. Na tafadhali kabla Bwana Abdulahi hajaanza kuongea wale tulio na simu za mkono tafadhali simu hizo zizimwe, simu za mikono, zizimwe. Sababu ni nini? Maneno mnayo ongea siku ya leo tunayanasa kwa kanda kwa hivyo usije ukafikiri neno unalosema kwamba kunalo halitanaswa. Hata ukikohoa wakati unaposema, kohozi lako linanasw. Kwa hivyo kila mmoja azime simu yake. Na pia tuwe na ukimiya ili mambo itakayonaswa yawe ni yale ambayo yanastahili. Basi Bwana Abdulahi, nafasi ni yako na nimekupa dakika kumi. Unasema jina lako, kama unasimamia kikundi basi ukitaje jina.

**Abdulahi Ndunga:** Asante sana Bwana mwenyekiti wa Tume hii, na ndugu zetu walio hudhuria hapa. Mimi kwa jina naitwa Abdulahi K. Ndunga. Mimi ni mwanakamati wa kamati ya waumini wa Msikiti unaoitwa Riadha hapa Majengo ya Lizard. Kuhusu maoni yetu, waumini wa Msikiti wa Riadha; kwanza kuhusu ofisi ya Chief Kadhi, maanake sisi tunaonelea kabla hatujaanza kutoka nje, tuangalie yalioko nje kwanza, tuanze kuangalia ndani ya nyumbani kwetu ndio tutoke kuangalia yale yalioko nje ya nyumbani mwetu. Ofisi ya Chief Kadhi imetajwa katika kifungu katika Katiba. Na tunataka katika Tume hii tunasema kifungu hicho ambacho kimetajwa ofisi ya Chief Kadhi, kibakie hivyo hivyo katika Katiba itakayokuja. Tunatoa vile vile maoni yetu tukitaka ofisi hii vile vile ipanuliwe. Ofisi hii ya Chief Kadhi iwe na mahakama kuu ya Chief Kadhi. Na iwe na mahakama ya appeal ya Chief Kadhi. Na tunataka kesi yoyote itakayo kuwa imefika mpaka kwenye mahakama ya appeal ya ofisi ya Kadhi, iwe hapo ndio mwisho wa kesi ile. Isiende kupelekwa katika mahakama nyingine yeyote, wala kusiwe na mahakama nyingine yote ina uwezo wa kukosa kutambua ile judgement au hukumu iliotolewa na mahakama ya appeal.

Maoni yetu ya pili, ni kuhusu Wakfu Commission. Wakfu Commission ni mali ya Waislamu, ambayo kwamba ni haki Waislamu wajifae na ile mali, lakini katika Kamati yetu tunaona Wakfu hizi hazina faida yeyote kwa Waislamu zinaolete, na kwa sababu yake ni nini? Zinasimamiwa na PC ndio Chairman, na PC amesimamia ki Serikali hasimamii Ki-slamu. Kwa hivyo sisi tunakua hatuna faida yeyote Waiislamu tunayopata kwa ile Wakfu. Kwa mfano tutaipa hii Tume mfano mzuri sana. Utaenda ukute jumba la gorofa tatu, lile jumba liko na karibu room kumi na tano. Lakini Commission hii ltasikitika kusikia nyumba ile kodi yake ni shilingi mia nne. Nyumba ya gorofa tatu, room, zaidi ya kumi na tano, kodi yake ni shilingi mia nne ndio yalipwa. Na isitoshe, hizo shilingi mia nne zikilipwa hiyo Commission ikichukua, kule zinakokwenda, sisi Waislamu hatufahamu. Hatuoni faida yeyote. Tunataka huu Wakfu usimamiwe na Waislamu wenyewe, iundwe Tume na ofisi ya Chief Kadhi ikishirikiana na Vyama vya Kislamu kama vile baraza la Maimamu, na Supreme Council na Chama kinachoitwa Kenya Koran Teachers Union. Waunde Tume ambayo kwamba ndiyo itakayo kuwa inahusika na mipango ya Wakfu ya Waislamu. Natunataka hicho kiwe ni kifungu ndani ya Katiba itakayo kuja na iwe ni sheria.

Maoni yetu ya tatu ni kuhusu Madarasa yetu ya kusomesha Koran. Madarasa yetu ya kusomesha Koran tunataka yatambuliwe ki Katiba kwa kuwa ni elimu kama elimu zingine. Kama vile zimetambuliwa shule zingine zozote tunataka na madarasa zetu zitabuliwe kuwa ni shule kama shule zingine. Na waalimu wake wapate misaada, na madarasa zipate misaada kutoka ndani ya Kenya, na nje ya Kenya. Tunataka pia Waalimu wa Madarasa wawe na haki ya kwenda kufungua account ya kwendesha ile Madarasa, kulipa waalimu na kutafuta mahitaji mengine kama kutaka kuongezea madarasa bila kusumbuliwa, kuambiwa iko wapi registar ya madarasa yako? Natunaka hii iwe ni kifungu ndani ya Katiba, na iwe ni sheria.

Maoni yetu ya nne ni kuhusu kitambulisho, passport, na birth certificate. Tunapenda kuifahamisha tume hii, vitu hivi, hati hizi, ambazo ni haki mwananchi kuzipata; sisi Waislamu tunanyanyaswa sana katika hali ya kupata hivi vyeti. Natunaipa hii Tume mfano moja ambao kwamba unatosha na tunaoujua, na ni wa haki. Leo watoto wawili ni wa baba moja na mama moja, huyu wa kwanza anaitwa John Karanja, na wapili anaitwa Suleiman Karanja. John Karanja atakapo kwenda kutaka kitambulisho, ataambiwa aende alete kadi ya ubatizo kutoka kanisani. Na akisha kupeleka ile kadi ya ubatizo itakua kwake yeye hakuna taabu, atapata kitambulisho. Suleimanm ndugu yake, mama moja, baba moja, atakapo kwenda kutaka kupata kitabulisho, ataambiwa kwenda ukalete birth certificate ya baba yako na ya mama yako, na ya babu yako, itatoka wapi? Itakua Suleiman kwake kupata kitambulisho au hati nyingine ni taabu kwake. Tunaiambia hii Tume tunaona sisi, tunanyanyaswa haswa Waislamu. Watoto wawili wa mtu moja hali ni hiyo.

Tunataka Waislamu na sisi, tukienda kuomba hizi hati, iwe kitambulisho cha baba cha tosha mwanae apewe kitambulisho. Na kama si hivyo aambiwe aende akachukue barua kutoka kwa Imamu wa Msikiti wowote ulioko karibu, na hiyo yatosha apewe kitambulisho. Na tunataka hiki kiwe ni kifungu ndani ya Katiba itakayo kuja, na iwe ni sheria, sio kitu cha kuondolewa kesho kutwa.

Maoni yetu ya tano, ambao kwamba Bwana Chairman ndio itakayo kua ya mwisho. Ni kuhusu wanyama wa porini. Tumetoka kidogo kwa upande wa Waislamu tunaingia katika taifa nzima. Wanyama wa porini hapa Kenya wamepewa dhamana kuliko mwananchi. Wanadhamana kubwa kuliko mwananchi, kwa mfano, mwananchi akienda akikanyagwa na ndovu, au auwawe na nyati, au mnyama wowote, ridhaa atakayolipwa ni shilingi elfe thelathini. Hata skuta iko na pesa nyingi kuliko mwananchi hapa Kenya. Skuta ukienda kununua dukani utaipata kwa pesa nyingi. Mwananchi alipwa shilingi elfu thelathini akiuwawa na ndovu. Shilingi elfu thelathini zinawezaje kusaidia familia itakayo bakia ya huyu mtu? Wanyama wa mwituni wakiingia ndani ya shamba ya mwananchi, wakiharibu mimea yake yote, halipwi hata ndururu moja, anabakia kuhangaika atakula nini, hana pesa hana chochote.

Wanyama wa porini wana ardhi maeka na maeka, wanatembea vile watakavyo. Wananchi wengi wa Kenya hapa hata hawana pahala pa kuweza kujenga kibanda cha nyumba. Wakati huu wananchi wengi hawana mahala hata pa kuweka mbawe zao. Tumechoka kuambiwa wanyama wanaleta pesa Kenya; hizo pesa ziko wapi? Bona hatuzioni. Mwananchi alipwa shilingi elfu thelathini. Tunataka na tunatoa wito kwa hii Tume hii iwe kifungu kwa sheria. Wanyama wa mwituni wakimuua mtu, apewe ridhaa, watu wake uchache uwe ni kuanzia million tano na kuendelea juu. Na wanyama wa mwituni wakiingia ndani ya shamba la mwananchi waharibu mimea yake, serikali iangaliwe mimea yake, idhaminiwe, alipwe ridhaa. Ikiwa wanyama twambiwa waleta pesa nyingi kutoka nchi za nje, hizo pesa zinaenda wapi basi? wananchi tunapata taabu namna hii wakati ambao wametuingililia. Basi Bwana mwenye kiti kwa hayo machache tuliyoyazungumza hapa sisi wanakamati, waumini wa msikiti wa Riadha tunakwambia sasa mwenye kiti tuokoe katika haya mambo uone yameingia ndani ya Katiba itakayo kuja. Asante sana Bwana.

**Com. Salome**: Mimi swali langu ni moja, umezungumza kuwa wanyama wana shamba kubwa kuliko wananchi, hukutupa pendekezo juu ya hilo? Yale mengine mawili umetupa mapendekezo mazuri, je unataka tufanye nini na hayo mashamba yenye iko na wanyama?

**Abdullahi Ndunga**: Asante sana Madam, ambao ni mwanakamati wa hii Tume. Sisi twapendekeza hivi, sababu gani wanyama wawe na ardhi ya kutembea vile watakavyo mwananchi hana mahala? Hii ardhi ipunguzwe wananchi wapewe. Ardhi hii yote, T-sub East and T-sub West na kule kwingine kwenye buga zikatwe nusu zigawiwe wananchi waweze kupata mahala pa kuweza kujenga vibanda vyao vya kukaa. Kuliko wanyama wakae tu, tunaabiwa wana pesa na hatuzioni pesa; twahangaika. Ipunguzwe wananchi wapewe ardhi.

**Com. Ayonga**: Asante. Je kuna yeyote hapa (inaudible) mzee unaweza kujiandikisha na utupe hiyo memorandum yako.

**Com. Ayonga**: Next wakati anapo endelea, namtaka Athmani Mohamed Ahmed. Unaweza kuanza.

**Athmani Mohamed**: Salaam Aleikum,

**Com. Ayonga**: Toa majina yako yote.

**Athmani Mohamed**: Jina langu ni Athmani Mohamed Ahmed kutoka Majengo Liberty. Niko katika kamati ya waumini wa Msikiti wa Riadhi na ijapokua hatukujitayarisha kuzungumza lakini naona nimetajwa. Basi nilikuako na point yangu moja ndio nataka kuelezea tu. Ok. Point inaeleza hivi, mimi kama mwana kamati wa waumini wa Riadhi ningependelea ile Katiba ya kwanza iliowekwa Lancaster House Uingereza irudishwe. Na niko na kipengee juu ya maoni hayo. Katiba hiyo ya kwanza ilikuweko inahusisha sana Majimbo, na katika Majimbo kwa imani yangu, na imani ya Wakenya wengine, hususan ni kizungumzia wa Pwani, haki zetu zimetupwa katika kaburi la sahau. Wengi wa Wapwani haki zao zimekua hawazitambui na wala wakizitambua hazifuatiziwi. Mfano wa kugandamizwa haki za Pwani ni kama katika mambo ya ardhi, mambo ya employment na, kutengwa katika kazi za kiserikali na mengineyo. Yangu ni hayo tu, niliokua nayo.

**Com. Ayonga**: Asante Bwana Athmani, yeyote ana jambo basi anaweza kwenda kule ajiandikishe na pia atwachie memorandum. Mwingine ni Said Karama.

**Said Karama:** Salaam aleikum. Mimi memorandum yangu nimeiandika, wajua ziko memorandum namna nyingi, za kuzungumza, za michezo ya kuigiza, na za kuimba. Mimi nimeadika kwa sababu ni mshairi nimeandika kwa mashairi. Na nimeandika mashairi kudai serikali iwe ya Majimbo. Serikali ya Majimbo itatuondolea mambo mengi ya kunyanyaswa. Yaani, kwa mfano uwe uko hapa, kazi imetokea percentage kubwa ya wale wafanyi kazi wachukuliwe kutoka katika Jimbo lile na

wale wengine, sio kwa kwamba wasipewe, lakini percentage kubwa, kama themanini katika mia wawe wa Jimbo lile.

Jambo la pili kimetokea cheo cha kazi na kuna mjuzi hapa, aletewa mtu kutoka Kisumu, hii haifai. Apewe yule haki yake, maadam ana ujuzi, apewe. Sasa kwa mfano shairi hili limechanganya mambo yote hayo ya kunyanyaswa ambayo halafu tutayapiga chapa katika gazeti la Majimbo. Kila moja ataiona, na copy moja itakwenda kwa Commission: Kusubiri tushachoka, ngonja haiwezekani, bunga ashaerevuka, ametoka ujingani. Sasa Majimbo ataka, mpingao samahani. Ukisha amua wa Pwani, Kenya iwe ya Majimbo. Msiambiwe twawabagua, mkaingia hasirani. Sasa au sana tuliwachukua, mkatutoa dhamani. Leo tusha amua kupiga about turn, tusha amua wa Pwani, Kenya iwe ya Majimbo. Asanteni.

**Com. Pastro Ayonga**: Asante sana. Hii ni copy yetu. Next Rajab Sumba, Hamisi Hassan, Elijah Miyogo. Wewe ndiye nani?

**Rajab Sumba**: Rajab Sumba

**Com. Ayonga**: Tafadhali anza.

**Rajab Suba**: Salaam Aleikum.

**Com. Ayonga**: Rajab Sumba ningependa utoe majina yako kamili na useme, kama ni maoni yako wewe mwenyewe, au unasimamia kikundi fulani. Na pia kama unamaandishi unaweza kumulika kwa yale makubwa ambayo yako, badala ya kusoma maneno yote.

**Rajab Sumba**: Mimi jina langu ni Rajab Sumba. Afisa mkuu wa Kanu katika eneo la Mvita, na hapa hivi leo, nimekuja kuwasilisha maoni ya Waziri wa Nchi katika Office ya Rais Hon. Sharrif Nassir, ambaye kwa masikitiko yeye hakuweza kupatikana kwa sababu ya kazi za kiserikali zilizo mlazimisha kwenda Nairobi. Kwa hivyo hapa mimi natoa mapendekezo haya kwa niaba ya Mheshimiwa Sharrif Nassir. Na vile vile tunamapendekezo ambayo tumeyaandika na tuta yatoa lakini kama ulivyo sema, kwa ufupi ni weze kupitia mambo haya, kuyafafanua ili muweze kuyasikia na kuyaweka katika records zenu. Hon. Kamishena wa Tume ya marekebisho ya Katiba, ndugu zangu waliohudhuria hapa, maneno ambayo nataka kuyasema, kwanza, ni kua twa shukuru mmekuja kutupa nafasi hii, ili kueleza tuliyo nayo. Na iwe ndio kinga ya kuzuia matatizo ambayo yanaonekana yaweza kutokea mbeleni. Kama mnavyo jua kumetokea umwagikaji wa damu katika Kenya nzima, kabla ya uchaguzi wa mwaka tisini na mbili, na wa mwaka wa tisini na saba. Na haya yote hayawezi kutokea, bila ya sababu, na sababu zenyewe ambazo zimefanya mambo haya yatokee, kwanza ni sababu za ufisadi.

Pili, sababu za ugadamizaji wa haki za kimsingi, na vilevile kutotekeleza sheria zilizoko katika Katiba. Sisi twajua kama hivi sasa kuna Katiba. Lakini pia sisi twajua hivi sasa Katiba ilioko, kuna vifungu vingi ambavyo havitekelezwi kisawasawa. Kwa hivyo tunavyoomba ni kwamba Kenya iwe ni nchi ya vyama vingi vya kisiasa. Kenya iwe ni nchi ambayo ya heshimu dini ya

Mwenyezi Mungu mmoja. Na Kenya vile vile iwe ni nchi ya amani na usawa kwa kila mmoja. Usawa kwa matajiri na maskini, usawa, kwa waume na wake, vile vile uweko usawa wa wazee na vijana, usawa wa wazima na vilema vile vile. Huo ndio utangulizi. Muundo wa serikali ambao tunautaka ni muundo wa serikali za Majimbo. Hiyo tunaouna itakua ni kinga kubwa ya kuondosha hatari ambayo tunaiyona mbele na tunampogeza ambaye amechagua Tume ili kila mtu atoe maoni yake, na maoni haya yapelekee kutengenezwa Katiba nzuri ambayo itatizama mambo haya yote na kulinda hatari ilioko mbele. Serikali ambayo itakua ni serikali itakayo simamiwa na Rais, iwe ni serikali ya kufuata muundo wa Majimbo. Itakua ni serikali itakayo kua na Makamu wa Rais kila Jimbo. Na hawa Makamu wa Rais wa kila Jimbo ndio watakao simamia serikali za Jimbo wakiziendesha chini ya wale wajumbe ambao watakua wako katika Jimbo lile. Ni serikali vile vile ambayo itakua na Waziri Mkuu atakae kua ndio kiongozi wa serikali. Manaibu wawili wa Waziri Mkuu ambao watakua wakifanya kazi chini ya Waziri Mkuu. Baraza la Mawaziri litachaguliwa na Rais.

Tukiondoka katika muundo wa serikali ambao utakua na mabaraza mawili Senate na Lower House.

Daraja ya tatu ni bunge la Jimbo. Sisi hapa tutaingia katika kifungu cha Uraia. Uraia tunaona uwe mtoto akizaliwa baba na mama ni Mkenya, awe Raia moja kwa moja. Akizaliwa Kenya akizaliwa nje ya Kenya. Vile vile ikiwa baba ni Mkenya, mama si Mkenya mtoto akizaliwa awe Mkenya. Na bila ya kufanya ubaguzi wa jinsia mama vile vile akiwa Mkenya na baba si Mkenya mtoto huyu vile vile awe Mkenya. Yule ambaye ni mgeni lakini amekaa katika Kenya kwa tabia nzuri kati ya miaka mitano aweze kukubaliwa kama Mkenya iwapo ataomba kuwa Mkenya. Nasikia kama saa zinamalizika lakini nina meneno mengi ya kuzungumza. Lakini nafikiri nitapata nafasi ya kuzungumza habari ya Land Act. Indian Land Act. Kenya baina ya kupata uhuru kwa miaka thelathini na nane, wameendelea kutupia colonial Land Act mpaka leo. Yaani sheria ya ardhi ambayo ilitoka India, ndio ambayo tunatumia hapa mpaka leo, na mtasitaajabu Macommissioner mlioko hapa ikiwa mtaweza kupata nafasi ya kutembea hapa Mombasa, najua Commissioner mmoja alikua hapa Mombasa, alikulia hapa. Lakini wale wengine watembee hapa Mombasa waone katika Mvita Constituency, yaani sehemu za Kisauni, Changamwe na Likoni ambako pia matatizo hayo yako. Hapa Mombasa kuna Ward ya Bondeni, kuna Ward ya Tononoka, Ward ya Mwembe Tayari, Ward ya Majengo, Ward ya King'orani na kuna Ward ya Shimanzi. Katika mitaa hiyo yote utakuta kwamba mtu anakodishwa ardhi, badala ya mtu kukodishwa nyumba akawa mpangaji wa nyumba, anakua mpangaji wa ardhi. Mtu mpangaji wa nyumba awe mpagaji wa ardhi? Lakini kwa sababu ya kufuata ile Indian Land Act, ndio matatizo haya yote yanatokea, system inayo endelea, watu wanakua na nyumba zao kwa miaka mia, miaka mia mbili lakini ardhi siyake. Leo sisi tunaona vituko vinavyofanyika katika ulimwengu kama kule Palestaine, ma-bulldozer yanaingia yanamaliza miji yote kwa sababu ya kua ni miji ya refugees. Sisi hapa ndani ya nchi yetu bulldozer vile vile huingia saa nyingine zikamaliza kila kitu. Kwa hivyo tunawaomba, hii Indian Land Act ibadilishwe, ardhi yote iwe ni ardhi ya serikali na kila mwenye nyumba apewe kipande chake cha ardhi ya ile nyumba yake mwenyewe alokaa.

Unajua, sisi Waheshimiwa Makamishena, sisi hapa Mombasa urban area, hatuna mashamba. Shamba lake mtu ni ile nyumba anayo kaa, kwa sababu hana tena communication na kule rural area alipotoka, pengine yuko hapa miaka mia, pengine yuko

hapo miaka mia mbili. Yaani babu na babu na baba na mama na watoto na wajukuu wote wazaliwa hapa. Lau sasa hivi wavunja nyumba yake pale yeye hajui aende wapi kwa sababu hana, Tiwi, hana Malindi, yaani hana Mazera, hana popote, yaani ile nyumba yake ndio shamba lake, ndio mji wake. Kwa hivyo urban areas zichukuliwe zingine katika Constitution hii ijulikane kama kuna permanent resident wa urban area. Nasikitika nina mambo mengi lakini wakati ni mchache. Na madhari hii memorandum ninayo kwa sababu nilikua nataka kuzungumza habari ya basic rights, yaani haki za kimsingi lakini ninaona ni fuate taratibu iliowekwa, yaani ningezugmza hapa labda mpaka saa sita lakini nawashukuru.

**Com. Ayonga**: (Inaudible).

**Rajab**: Nawashukuru sana.

**Com. Solome**: Swali moja kwako umesema kua watu, (inaudible).

**Rajab:** Kwa mwenye ardhi, hapa tuna Landlord ambao nitofauti na the rest of the country. Yaani huko kuliko bakia katika nchi ardhi ni ya serikali, au ardhi ni ya community. Hapa kwetu ni tofauti, ndio sababu ya kuwaambia hii Indian Land Act Itupwe. Hapa kwetu mtu ana ardhi yake labda eka mia moja, na ardhi ile anaikata Swahili layout. Kujenga Swahili type houses, kisha anaeka land tenancy ya yule anayejenga nyumba, anamlipa yeye shilingi mia tano kila mwezi, kwa ile nyumba aliyo jenga. Bali na rent ya houses; hii ndio system ambayo iko hapa peke yake hapa Pwani. Kwa hivyo tuokoeni system ya Kenya, na system ya Pwani iwe moja. Nchi isiwe na system mbili.

**Com. Ayonga**: Asante, unajua sisi tumejifunza jambo ambayo tulikua hatujui asante, sasa peleka memo yako ujiandikisha na utuachie hiyo memo. Hamisi Ali. Abraham is here. Elijah Mindoko. Wewe ni Elijah? Ali Amran.

**Hamisi Ali:** Salaam Aleikum. Mimi kwa majina naitwa Hamisi Ali Abran, niko hapa kwa niaba ya vijana wa Majengo, mimi ndio mweka hazina wao. Nina mambo tofauti ambayo nitakayo ya zungumzia hapa, kuhusu vijana wa Majengo, au vijana wa Pwani. Kwanza nitazungumzia kuhusu Majimbo, elimu, michezo, kazi na kisiasa. Nikianza na Majimbo, natumai serikali ya Majimbo ndio itakayokuwa suluhisho kwa vijana wa Pwani. Kwanza, tukiwa na serikali ya Majimbo, vijana tutapata nafasi za kazi kwenye mashirika yaliyokwenye maeneo yetu ya Pwani. Nikitoa mfano, utakuta sisi vijana wa Pwani tunanyanyaswa sana ki kazi. Leo zikitoka nafasi za kazi katika mashirika yalio katika Pwani, mfano kama KPA, Posta, Railway na Power and Lighting, utakuta ni vijana wanaotoka bara, ndio huletwa kufanya kazi hizo, hio 80% ya vijana wa Pwani inakua 80% ya vijana kutoka bara. Sasa sisi kama vijana wa Pwani tukiwa na Majimbo nafikiri haki zetu zitakua sawa. Kwa sababu tutaweza kupata nafasi hizo za kazi. Pili nikizungumzia ki michezo sisi kama vijana wa Pwani. Nafikiri michezo mingi Kenya ilianza hapa Pwani. Lakini leo unakuta michezo mingi yote nafasi za michezo zinapotoka unakuta leo watu wa Bara ndio wanaifadhi hizo nyafidha. Kwanza nikianza kama mchezo wa kadanda, utakuta huu mchezo wa Kandanda hasa histori yake ulianza hapa Pwani. Lakini leo utakuta mchezo wa Kandanda, Pwani umekufa, sio umekufa, umeuliwa.

Tukiingia upande wa kisiasa, vijana kisiasa hatuna haki. Kwanza nitatoa mfano ya haki kisiasa kwa vijana. Sisi kama vijana tungependekeza kwenye bunge la Kenya, vijana wapewe haki yao wawe na mwakilishi wao wa vijana. Kama vile tunavyo chaguana vijana kutoka sub-location upto national level. Leo utakuta tunaambiwa kuna vijana kwenya bunge, lakini vijana hao hawajui haki za vijana walioko chini. Tatoa mfano, utakuta kuna Wabunge vijana kama Uhuru Kenyatta, Mudavadi, Katana Ngala. Vijana hao mimi ninapojua tangu wakizaliwa hawajajua shida ya vijana. Wote walizaliwa katika royal family, watu hawa hawakujua shida ya ki-elimu, watu hawa hawakujua shida tunazo pata sisi vijana, sasa tungetaka sisi vijana tupewe haki ya kuchagua vijana kuanzia chini sub-location upto National Level. Tuwe na Mbunge wetu wa vijana. Nitatoa mfano ya nchi jirani kama Uganda. Leo Uganda utakuta wana Mbunge wa kina mama, wana Mbunge wa wasiojiweza, wana Mbunge wa vijana. Ningependa mfumo huu ufuatwe katika bunge letu la Kenya ndio kila mtu atakua na haki yao.

Pili, nikiingia kwa upande wa wazee wa mitaa, kutetea vijana, pia kwenye mtaa ule, haja mpata mzee wa mtaa akajua kua mimi nimekuja mchukua kijana fulani, kusudi mzee wa mtaa yule na chifu atakapo jua kijana fulani amechukuliwa, ni rahisi yeye kujua yule kijana atafanywa nini huko alikokwenda. Leo unakuta kijana anakuja anachukuliwa, baadaye hajulikani alipokwenda. Huwezijua kijana labda alipatikana na makosi fulani, akapelekwa kotini, unakubali ama hukukubali, sikukubali, romande. Kijana yule anaweza kuozea kwenye jela zaidi ya miaka mitano kwa kitu asicho kijua. Ningetaka sana serikali iwape wazee wa mitaa uwezo wakuweza kumiliki mitaa yao. Kabla kijana hajakuja kuchukuliwa, askari yule kwanza apitie kwa mzee wa mtaa amueleze mzee wa mtaa nimekuja kuchukua kijana kwa makosa fulani, fulani, mzee wa mtaa aende kwa chifu, kijana yule atolewe na mzee wa mtaa. Hayo ndio yaliokua maoni yangu na sina mengine isipokua nataka Ma-commissioner swala la vijana mlipeleke lisikilizwe sana katika bunge na kwa serikali nzima. Asante.

**Com. Salome**:Asante sana Bwana Hamis Ali nashukuru kuwa umepata nafasi yako ya kuzungumza. Swali langu ni moja inaonekana kuwa watetea vijana wawe na mwakilishi moja katika bunge, na tunasikia kuwa katika Kenya vijana ni karibu sabini kwa mia ya watoto wa Kenya. Ni wengi kweli, basi wewe watetea huyu kijana mmoja, atastahimili kazi kubwa ya kuwakilisha sabini kwa mia ya watu.

**Hamisi:** Natumai, Bi.Commissioner, nataka unielewe. Sisi kama vijana tuwe na uwezo wa kuchagua kijana kwanzia chini mpaka juu. Kwa sababu tukipewa nafasi hiyo, leo kijana asimame kwanzia chini, tumchague kama mwakilishi wa vijana katika bunge, watakwenda kwenya district level, mpaka kwenya national level. Sasa yale yatakayozungumzwa juu yatakua yametoka chini. Kijana yule ataweza kuwakilisha maombi yetu. Sio sisi twambiwe kuna kijana kwenye bunge. Kijana yule nikama vile nilivyotangulia kukuambia ni royal family. Yeye atazungumzia maoni yake ambayo alikua nayo.

**Com. Salome**: Je kijana unatakaje tafadhali, ni maombi gani uliojali?

**Hamisi:** Kijana mwenye kuaanza miaka kumi na nane mpaka miaka thelathini na tano, huyo ndiye kijana.

**Com. Ayonga**: Lakini nataka pia ujue, kwamba sehemu zingine ikiwa baba yako yuko hai na wewe ni mzee ni kijana wa baba. Kwa hivyo kijana kwenu huwezi kusema umri wake ni huu, lakini unajua, unamaanisha watu wa umri huu wa dot.com. Thank you, ngoja kidogo.

**Com. Wambua:** Bwana Abran ulisema ya kwamba huu mchezo wa kandanda, (inaudible) wao lakini ningependelea ueleze jinsi unaweza kuwasaidi vijana upande wa michezo, hatukupata specific proposals kutoka kwako ama pendekezo uko nazo?

**Hamisi:** Pendekezo langu, natumai miaka ya nyuma. labda wakati huu nilikuwako sija zaliwa, lakini historia niliopata, nafasi ambazo tulikua tukipata sisi vijana wa Pwani, palikua na mashindano ya kimichezo, haswa kama kandanda. Kulikua na inter-province. Michezo ile itakapochezwa ya kila mkoa, zile talent zilioko zitapatikana. Lakini leo unakuta kocha ametolewa uko mzungu anazugushwa Nairobi, Kisumu, Kakamega na maeneo mengine. Hapa mkoani Pwani analetwa tu team inapokuja kucheza, sasa vijana wetu hawapati nafasi hizo.

**Com. Ayonga**: Tafadhali naomba uwende kule ujiandikishe na pia utuachie maandishi hayo kwa maana mambo ya vijana lazima yaandikwe. Mohamed Shallow. Tafadhali unaweza kuaanza.

**Mohamed Shallow**: Salaama aleikum, Ma-commissioner, mabibi na Bwana. Mimi ni Mohamed Shaib Shallo, na wakilisha Muslim Civic Education Trust (MCET). Tasisi ya Waislamu wa Kenya hususan hapa Pwani. Kuzugumzia juu ya mada ya Katiba na kubadilishwa kwake, msingi wa mazugumzo yangu itakua ni yale maneno aliyoyasema yeye mwenyewe Rais wetu wa Kenya, Bwana Moi, alipokua kule Safari Park IV katika ukumbi wa kule, ambao ulikuwa vile vile ni ukumbi wa Katiba. Kiongozi wangu kama Rais wa nchi yangu Kenya Bwana Moi alisema wazi wazi alipoulizwa, alijibu, "power za Rais ni nyingi zafaa zipunguzwe zirudishiwe watu". End of quote.

Rais mwenyewe aliposema haya yalikua ni ya halali kwa sababu yeye mwenyewe ana experience kama Rais. Yeye mwenyewe vile vile alikua ni Mjumbe na mpaka leo ni Mjumbe kwa muda wa miaka mingi. Na yeye mwenyewe ni Mkenya halisi, na ana jamaa zake hapa Kenya. Kwa hivyo sidhani kama yeye mwenyewe Rais aitakia nchi hii matata yoyote hela baraka. Ndipo aliposema yale kwa minaajili ya watu wa Kenya. Kwa hivyo tukiangalia maneno ya Rais aliyo sema ni mambo ya kidemokrasia, power ya watu, yaani warudishiwe watu. Utarudisha vipi power ya watu kwa watu, hiyo ni greater democratization.

Kwa mitindo ya kupiga kura, watu wakupa kura uwatumikia watu. Kwa hivyo watu lazima warudishiwe matokeo fulani, wapewe power wajisimamie wao wenyewe ili wapate maendeleo ya nchi nzima. Greater democratization. Kwa hivyo basi, kupitia hii greater democratization, ina maana gani? Ina maana ya kwamba Katiba iwe ni mfumo wa kutoa nafasi zaidi kila mtu ashiriki katika demokrasia ya Kenya.

Na hii ni kwa upande wa Majimbo. Kwa upande wa federalism, yaani tuweke tawala za kihaki ambazo zitatabulika na serikali yao wenyewe. Zile establishment tutaziita State. State with authority na State zile zikipata mamlaka ndio watu wanapata mamlaka yale. Hivi sasa power zote zimefungwa, zimetiwa katika kifurushi kimoja zimetundikwa pale Nairobi. Ukitoka pande za Lamu au Lunga Lunga unaabiwa nenda Nairobi, ukitoka pande za Homabay, Kendu bay unaabiwa uende Nairobi, ukitoka pande za Elewak unaambiwa nenda Nairobi. Sasa hiyo Nairobi ndio Kenya peke yake? Mabadiliko hayo lazima tuyalete kwa sababu, sera za kizamani wale wazee wetu walikua wakifanya bila Nairobi, kulikua hakuna Nairobi. Na nchi ilikuweko, na watu walikuweko, na wakiishiana vile vile, wakifanya biashara vile vile, na wakiishi salama salamini, imekuwaje leo? Hilo liangalieni sana Bwana Commissioner. Kwa hivyo utaratibu ambao sisi katika MCET tukishirikiana na Waislamu wenzetu, ni kupinga ile marginalization ambao Waislamu katika nchi hii waliletewa, tuliona tufanye tasisi hii natuwaelimishe Waislamu ndugu zetu, wake kwa wanaume, na matokeo yao yakawa kupitia katika seminar wakaunda kitabu hichi. Kitabu hichi, Waislamu Kenya Waitakayo, kimeundwa kwa sababu ya zile seminar zao walikua wakija katika institute, wakiangalia maswala tofauti, tofauti. Wakitoa rai zao, na sisi tukiwahudumia mpaka tukafika pahali tukaona kwamba lazima tutoe mapendekezo fulani fulani. Na tukaona tukileta mapendekezo ya State Federation, hapo tutakua kila mtu wa Kenya, sio Pwani tu, kila mtu wa Kenya twampa mamlaka kulingana na yale alosema Rais Moi, kwamba power za Rais zipelekwe huko kila pahali. Na ndivyo utaratibu ambao utafaa kufuatwa, ili kila mtu, kila pembe ile authority inakwenda kwake, tuondoshe ile myth ya Nairobi kwamba Nairobi ndio kila kitu. Nairobi itabakia vile vile, itakua na maswala fulani. Maswali ya bendera kuu ya nchi, masahala ya wimbo wa taifa sawa, maswali ya ulinzi Kenya nzima, sawa, maswali ya mambo ya Foreign Affairs sawa. Kwa hivyo nduguzanguni tunaomba ukumbi huu uniunge mkono mimi kupeleka kitabu hiki kukieka kwenye meza yenu wa kubwa, na Katiba hii itakua ni Katiba yetu zote na ndugu zenu na watoto wenu pia itawahusu.

Vile vile katika Katiba lazima tuwe na Preamble, Preamble itasema hao Wakenya ni watu gani? Leo twasikia Waswahili wamo, mara hawamo, ni vivi hivi Bwana? Twavutana sisi wenyewe kwa wenyewe, haitufai. Kabila za Kenya zajulikaniwa wazi wazi, kuna wale Elmolo ambao ni wachache, twawajua. Na Waswahili wako vile vile. Na kunawengine Wa-embu kabila ndogo, ndogo watiwe nao. Kwa hivyo katika Preamble tutaandika makabila ya Kenya taslim, yote yarekodiwe katika kitabu ambacho sisi twasema ndio kitabu cha ujumuia katika Kenya nzima. Na vile vile katika Preamble, zitiwe conditions maanake twataka Kenya taifa libakie moja. Itiwe condition kwamba kila state ni lazima ibakie kuwa ni sehemu ya Kenya. Twajua mipaka ya Kenya, kama Kenya, na Tanzania, na Uganda yajua mipaka yao, na zile State vile vitakua by the Law so established. Zitajua mipaka yake vile vile. Na lakini lazima kila State ibakie ni State ya Kenya, kama vile tunavyo ona kwa mfano India ilipata uhuru katika 1940's – 1947, in a State zake, ina Chief Ministers wao, na ina Parliament yao kubwa, na kuna ma Prime Minister, na kuna President vile vile. Utaratibu namna huu waweza kufanywa katika Kenya. Basi hakuna haja ya kusema zote sisi ni wana Kenya huku wana Kenya wenzetu waumia.

Katiba bora ni ile Katiba ambayo inaturidhisha sote katika nyoyo zetu. Ambayo twaweza kuilinda kwa afya zetu na damu yetu. Mmoja wetu akigongwa sisi tutasema kwa nini huyu mmoja wetu amegongwa. Mmoja wetu akilala na njaa tuweze kuuliza

kwa nini yule analala na njaa? Ndio katiba bora. Kwa hivyo Preamble lazima iweko ya Katiba. Na mipaka yaani ino ya nchi yote ambayo imepiwa yatiwe ndani ya Katiba, na mipaka ya State itiwe ndani ya Katiba. Kwa hayo tu na washukuru na natoa asante sana.

**Com. Ayonga**: Asante sana Bwana Shallow, kwa ku-submit hicho kitabu. Ngonja kidogo. Asante unaweza kwenda ujiandikishe na unaweza kutwachia hicho kitabu. Yusuf Abubakar. Useme majina yako vizuri:

**Yusuf Abubakar**: (Inaudible).

**Com. Ayonga**: Naitana kulingana na vile majina yalivyo aandikwa. Ni kwa nini kuna shida?

**Interjection**: (Inaudible).

**Com. Ayonga**: Ndugu yangu nataka kama unataka uje hapa uakikishe, uje uhakikishe. Ninafuata orodha ya majina jinsi yalivyo kua.

**Interjection**: (Inaudible), mimi nilijiadikisha kusema, makarani katika gate pale walikua wakiandikisha list mbili,wanakuambia kama una memorandum uandikishe hapa, kama huna memorandum jiandikishe hapa. Sasa hii list ambayo unatangaza ni ile list ya watu ambao hawana memorandum.

**Com. Ayonga**: Basi mimi sina habari.

**Interjection:** Sasa sijui hao watu walikua wakiandikisha walikua wametolewa wapi.

**Com. Ayonga**: Hiyo habari mimi sijui. (Silence for some time). Wakati ambao tunangoja hii list ingine badala ya kuharibu wakati, wacha huyu kijana aendelee, sivyo? Kijana endelea.

**Yusuf Mahamud Abubakar**: Asante sana mzee wangu, kwanza kwa majina mimi naitwa Yusuf Mahamud Abubakar, na niko hapa kama Secretary General wa Shirikisho Party of Kenya. Kwa hivyo maoni nitakayo toa, ni maoni ya chama cha Shirikisho, kwa sababu maoni haya tumeyaandika nitagusia katika vile vipengee muhimi ambavyo nafikiri nimuhimu kwa sote kuvijua. Kwanza,

**Com. Wambua:** Mimi nafikiri nilikuona huko Tononoko.

**Yusuf**: Sikutoa ilikua ijakua tayari, sikutoa memorandum siku hiyo nilizungumza kuhusu kitu kimoja.

**Com. Wambua:** (Inaudible)

**Yusuf**: Ni tofauti kidogo siku ile nilizugumzia kitu kimoja kwa sababu ya wakati ulikuwa ni ndogo.

**Com. Wambua**: Inaudible

**Yusuf**: Sawa sawa, asante sana

**Com. Ayonga**: Kulingana na maneno ambayo Com. Wambua amesema ndugu zangu na dada zangu ikiwa kwa wakati mwingine umeshatoa maoni, yale maoni yalichukuliwa kwa kanda yako na kwa hivyo uwachie wengine pia nafasi ili waweze kutoa maoni, tusiwe tuko kule leo, kesho tuko kule na ni wewe tu. Kwa maana maoni hayana tofauti yeyote. Kwa hivyo wale ambao mmeshatoa maoni mapema mtusamehe, na msamehe wenzenu siku ya leo watoe maoni. Na ikiwa unatakakutoa kitu mpya toa tu hiyo kitu mpya badala ya kurudia mengine. Endelea.

**Yusuf:** Asante sana Com. Wambua na Ma-commissioners wengine. Yangu ni ku-summarise ile document ambao sijaitoa kwa Commission. Kwanza kama inavyojulikana Shirikisho inataka serikali ya Majimbo, kitu ambacho hatukuelezea ni Majimbo mangapi na ni Majimbo ya aina gani. Shirikisho inasema Majimbo yawe manane kulingana na zile provinces ambazo tuko nazo. Na vile vile inapendekeza kuwe na Reginal Assemblies apart from the Federal Government ambao ile Federal Parliament itakuwa ni Senate na House of Representative. Kuwe na Regional Assemblies halafu kuwe na local authorities. Na vile vile Shirikisho inapinga kuweko kwa Waziri Mkuu, inataka kuwe na Rais ambaye atasaidiwa na Makamu wa Rais na ichague cabinet kutokana na watu ambao sio wabunge. Kwa hivyo baraza la Mawaziri litakua liko katika mikono ya watu ambao sio wabunge. Na twasema tumependekeza kwamba zile wizara kumi na sita, ambazo zitakua ziko katika Constitution zimekua katika Constituion na Rais atakua hana nguvu ya kutengeza wizara mpya ama kuondoa. Ziwe ni zile zile kumi na sita, na ikiwa kuna haja ya kubadilisha, basi ni Constitution iwe amended kuongeza ama kupunguza.

Tukija katika nguvu za Rais, tunasema wenzangu walo tangulia kwamba nguvu za Rais zimekua nyingi na yote ni kwa sababu alipewa uwezo wa kuandika na kufuta baraza la ma Waziri, kuandika na kufuta Constitional Office Holders. Kwa hivyo ikiwa kutakua na vipengee vya kuangalia power kama hii basi itakua amepunguziwa. Kwa hivyo Rais kazi yake atakua aki-appoint, Ministers ama maofisa wakubwa wa serikali halafu wao wakiwa vetted na Parliament. Kwa hivyo Parliament ikikubali ndio watakua wamekubalika kama wafanye kazi zao.

Jambo lingine ambalo tumegusia ni kuhusu ardhi. Tunasema ardhi iwe katika mikono ya wananchi, kusiwe kama vile ilivyo, iwe ardhi iko katika mikono ya serikali. Na wananchi watawakilishwa katika kumiliki ardhi kupitia Regional Land Commission, ambazo wao ndio watakua na nguvu ya kuchagua zile kamati katika wards, ama location, ama katika vijiji vya kuweza kupeana

na kugawa ile ardhi. Na vile vile tumependekeza kwamba mtu atakae pewa ardhi ikiwa ni ya ukulima aweze kuitumia ardhi ile katika miaka mitano. Ikiwa atashindwa kuitumia, basi ardhi ile inaweza kugawanyiwa ile sehemu ambao ameshindwa kuitumia igawanyiwe wengine ambao hawana ardhi. Na ikiwa ni ardhi ya makazi waweze kujenga katika ardhi ile ndani ya miaka miwili ikiwa mtu atashindwa kwa njia moja ama nyingine, basi ardhi ile iwe inaweza kupewa mtu mwenye kuweza, lakini kupitia hapa ni kwamba ikiwa mtu ni mnyonge na amepewa ardhi ile, kuweko na njia za kumsaidia, ya kupitia local authorities kujenga zile nyumba hata kama atakua akikatiwa kidogo kidogo. Kuwe na loan ya kumsaidia kujenga nyumba kupita local authority awe akikatiwa kidogo kidogo.

Katika natural resources tunasema hizi zitakua katika milki ya Local Authority ambao watamiliki tija yake asilimia thelathini na tano na ile asilimia iliyobakia ya sitini na tano itabakia katika region. Na pesa hizi zitakua zikiwa subjected tunasema 80% ya zile pesa zitakazoweza kuwa collected katika region zitabaki, 20% zitakwenda katika Federal Government. Na pia tunasema kuna ardhi ambazo zimepewanwa kwa njia ambayo sio ya sawa. Ardhi hizi tunasema zichukuliwe tena zigawiwe watu ambao wanastahiki kupewa ardhi hizi. Ikiwa kuna ardhi ilichukuliwa kwa njia ambayo si ya sawa iregereshewe wale ambao walikua wanastahili.na ikiwa kuna mtu alinunua ardhi kama hii bila kujua kwamba ilipewa kwa njia ambayo si ya sawa anaweza kulipwa ridhaa kwa sababu yeye hakushiriki katika unyanganyifu ule halafu ardhi ile irudishiwe wale ambao wanastahiki kupewa ardhi kama ile. Halafu katika mambo ya koti za kadhi. Tumesema kwanza kuna area nne ambazo ziangaliwe, kwanza ni shirikishe ama ile nguvu ya zile koti za Kadhi Kulingana na sasa ni kwamba koti za kadhi zinaamua mambo yanayohusu personal laws. Tunasema jurisdiction hii iongezwe iwe ita include mikataba ya kibiashara ambayo Waislamu wenyewe watataka kuifanya kwa njia ya Kislamuu. Ikiwa kuna mikataba ya biashara ambao wataka kuipeleka Kislamu basi district yeyote ipelekwe kwa hizi koti za Kadhi. Na vile vile mambo za nyafs ziwe zitazungumziwa katika koti za kadhi. Mambo ya gifts ama hiba ipelekwe katika koti za Kadhi. Na vile vile usimamizi wa Misikiti na Madarasa za Kislamu yawe yakiamulia katika koti za Kadhi. Jambo la pili ni Structure. Zile koti za kadhi ziwe namna gani? Tunasema koti za Kadhi zile za chini kabisa ziwe na uwezo sawa na ile Chief Magistrate Courts. Halafu kuwe na High Court Department ya Kadhi ambao wao watasikiza rufani ama appeals kutoka kwa koti zile za chini za Kadhi, na wale Ma-judge ambao watakao kuwa hapo wawe ni Makadhi ambao wamepewa uwezo sawa na Majudge wale wengine wa High Court. Halafu jambo la tatu ni appointment.

**Com. Ayonga**: Wakati wako unakwenda.

**Yusuf**: Asante na maliza katika appointment. Ni kwamba hao Makadhi ama Chief Kadhi na Makadhi wawe watakua appointed na Judicial Service Commission lakini kupitia ushauri wa vyama vya Kislamuu kama vile Supreme Council of Imams na chama ambacho kitawakilisha Mawakili wa Kislamuu. Nafikiri kulingana na wakati mengi yako katika document ambayo tutapeana, hayo ndio maoni ya chama cha Shirikisho kuhusu Katiba tunayoizugumzia. Asanteni.

**Com. Wambua**: Kuna ya kwamba yale mashamba yalioibiwa halafu yakauzwa yachukuliwe na serikali na yapewe wale ambao hawana mashamba, na pia ukasema kwamba kama kuna mtu ambaye alinunua haya mashamba kutoka ka wale

walionyakua, serikali iwalipe ridhaa wale walinunua, je hayo maono si una sema serikali inunue shamba ambazo zilikua zimepewa watu kwa ki makosa?

**Yusuf**. Maoni yangu nimesema ya kwamba ikiwa kuna shamba lilitolewa ki makosa, halafu kuna mtu, bila yeye kujua shamba lile limechukuliwa ki makosa kwa sababu anataka kua na shamba ama na nyumba, akanunua bila kushiriki katika makosa yale, yule hajafanya kosa lolote. Kwa hivyo itakua si haki anyangangwe kwa makosa ya mtu fulani bila ya kupewa ridhaa. Kwa hivyo mtu kama yule apewe ridhaa yake lakini lile shamba lichukuliwe wapewe wala wanastahili.

**Com. Wambua**: Na mwenye makosa afanywaje?

**Yusuf.** Mwenye makosa asipewe ridhaa kwa sababu ya makosa yake.

**Com. Wambua**: (Inaudible).

**Yusuf:** Ikiwa makosa yatadhibitika nafikiri kuna njia za kisheria ambazo zinaweza kuchukuliwa kwa mtu kama yule.

**Com. Ayonga**: Asante, unaweza kujifikisha kule na toa memorandum yako. Je katika list ya leo sioni mama yoyote katika list ya wale ambao wanaongea?

**Interjection**: Tuko hapa.

**Com. Ayonga**: Mko?

**Interjection**: Ndio

**Com. Ayonga**: Ni kwamba sijafikia pahali penu, sawa, sasa wale ndugu mmefikia karatasi ambayo yapo majina yenu sasa, sasa hapo ndipo nitaendeleza mpaka nifike kati kati. Wa kwanza kufuatana ni hii ni Hassan Hamza. Na Hassan atafuatwa na Musa.

**Hassan Hamza**: Salaam aleikum. Mimi maoni yangu mimi ninavyotaka, kwa jina naitwa Hassan Hamza Hassan ni mkazi wa King'orani hapa. Nimekuja na mapendekezo na moani. Jambo la kwanza ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu Majimbo. Kama vile wenzangu wamezungumzia mimi ni kutia mkazo tu. Kama walivyotangulia kusema mbeleni, kuwa tumekua marginalised kwa muda mrefu, tumenyanyaswa, haki nyingi zetu zimekwenda. Kwa hivyo kitu ambacho ninakisisitiza kwa sasa, kwa kwanza naanza na upande wa employment kama walivyo gusia hao wamesema 80% ya kazi ambazo zinatoka kwenye mashirika zipewe wakazi wa Pwani. Mimi nasema hata 80 ni kidogo, 90% ya kazi hizo zipewe wakazi wa Pwani, sababu,

tukiangalia kama shirika la Kenya Power and Lighting, jambo la kusikitisha ni kua hata meter readers pia, mpaka watoke Kenya waje hapa, waje wafanye kazi. Hapa hakuna watu wamefika form four kuja kufanya kazi ya meter reading katika Kenya Power and Lighting? Kwa nini vitu kama hivyo viwe? Kwa hivyo kitu nasisitiza, Katiba ibadilishwe tuwekewe Jimbo letu, kazi zote shughuli zote za Pwani zifanywe na watu wa Pwani.

Kitu nataka kuguzia tumekuwa na taabu kubwa hapa kwetu. Kitu chenyewe kinaotusumbua ni drug abuse. Madawa ya kulevya, ningeomba kwenye Katiba iekewe mkakato mtu yeyote anayeleta madawa ya kulevya katika nchi yetu penalty yake iwe ni kifo moja kwa moja. Jambo la kusikitisha ni kua, mkitoka hapa hata Bi. Commissioner Bwana Macommissioners msiende mbali, mvuke barabara mtaa wa kwanza ama wa pili. Mtasikitika kuona vijana wa kwetu wamegeuka mazombie. Kwa madawa ya kulevya, jambo la kusikitisha kua ni vijana hao peke yao ndio wanashikwa na kutiwa kotini. Wanaoleta hakuna, middle men hawaonekani, hao watu watatumia madawa ya kulevya namna gani ikiwa hao watu hawatashikwa. Kwa hivyo tunataka chain ifuatwe. Anaye leta, middlemen na hao vijana wetu kuokoka ni hao watu wakuwe punished inavyo wezekana.

Point yangu ya pili ni kuhusu elimu. Ningeomba kwenye mambo ya elimu tuwe na system ambayo itanufaisha jamii yote ya Kenya. Kusema vitu kama hivyo tunasema kuna shule ambazo ziko mashambani. Facilities za kufanya vitu kama Biology, Chemistry, Physics, hakuna na watoto wale wale wa mashambani anafanya mtihani ule unaofanywa na mtoto wa Alliance. Facilities na kila kitu kule kiko, halafu mnasema kua Kenya watu wanasoma. Mwambao wa Pwani watu hawasomi. Ikiwa hakuna facilities kama hizi mnatarajia performance zetu zitakua namna gani, definitely zitakua chini, kwa hivyo tunaomba zikue facilitated, facilities zilizoko Alliance, Mang'u, Starehe, ndio facilities zipelekwe shule zilizoko katika vijiji vya kwetu ili tuweze kuboresha elimu yetu hapa katika Mkoa wa Pwani.

Point yangu ya mwisho sitaki kuwachosha sana na muda ni mdogo ni Presidential powers tunataka zikue trimmed. Kusema hivi kua,, Rais wa Kenya kwa wakati huu akiwa na raha utafaidi, akikasirika na wewe umeenda. Kitu cha kwanza ni kwambie, anachagua Mawaziri, ana nguvu zakufuta kama vile ilivyo semekana hapa. Tuchukulie mfano kitu kimoja, unamchukua mtu unampatia wizara ya afya. Haja kanyanga darasa, unaenda kumpatia Wizara very sensitive atai-run namna gani Wizara kama ile na mambo ya utabibu kwake hakuna. Definitely ataharibu, ndio utakuta kwa wakati kama huu Kenya is in chaos kwa sababu hizi political appointees kwa sababu wewe unani favour mimi we Bwana chukua kazi kwa sababu unaninufaisha. Kwa hivyo vitu kama hizi tunaomba presidential powers zikuwe trimmed kiasi chakua appointment zote zinazofanywa, zifanywe achague watu, parliament ikisema ndio wale watu wapitishwe ikikosekana, ikisemekana hakuna ni hakuna. Tutoe mfano mwingine wako Mawaziri kwa wakati huu wako na kashfa hata kutembea kama ni watu binadamu za kisawa sawa wangekua wanangalia chini hivi. Lakini ndio watu wako katika uongozi wa serikali hii yetu. Kwa hivyo vitu kama hivi, mtu mwenyewe kashfa aina yeyote asiwe na mamlaka ya kukaa ofisi yeyote ya serikali. Kwa kumalizia, ningeomba kama vile kijana amesema, tunataka vijana tupewe kipao mbele kwenye serikali yetu. Kwa hayo nimesema asante.

**Com. Ayonga**: Ngonja kidogo kuna swali?

**Com. Salome**: Asante sana kwa mazugumzo yako, swali langu ni moja. Umezungumza kua ungetaka kuona kazi zikipewa wenyenji wa Mkoawa Pwani, lakini hali hii imekua ni kua watu wanatoka Kenya kuja kufanya kazi hapa, je Kenya ni ipi na Mkoa wa Pwani ni nchi gani hiyo?

**Hassan:** Kutokana na Katiba ilioko kuwa Mkoa wa Pwani ulikua uko katika British Protectorate, ni mwambao wa Pwani, na walipo ingia serikali iliyotangulia waka-amend sheria lengine mpaka wakafanya sisi tukaingia kwenye Kenya ndio sababu ya chanzo ya taabu zote hizo tuliopata.

**Com. Salome**: Je kwa wakati wa sasa, bado kuwa baada ya uhuru manajizugumzia kuwa watu wa Kenya, kama mkaazi wa Pwani mnajichukua mko katika nchi gani?

**Hassan:** Mimi kama mkaazi wa Pwani, kwa sasa tuko katika Kenya kwa kupelekwa kwa lazima, lakini kwa ukweli wa mambo, sisi bado ni wakaazi wa Pwani vile vile, Mkoa wa Pwani.
Mwambao wa Pwani.

**Com. Ayonga**: Thank you, hayo ni maoni pia, na kila mmoja ana haki ya kutoa maoni yake, na tuyaheshimu maoni yake. Next Musa Athmani. Ningalipenda tuokoe wakati na wengine pia wapate nafasi kwa hivyo ndugu zangu mnapo toa maoni ikiwa fulani amesema wewe wacha kusisitiza maneno ya mwingine toa maoni yako tu speak to the point. Unaweza kuendelea ndugu.

**Musa Athmani**: Salaam aleikum. Jina langu Musa Mwela Athumani, Secretary wa Majengo House Owners. Mimi nitazungumzia juu ya ploti za Majengo, lakini kabla sijazungumzia hiyo nataka kuonyesha dalili ambayo inasababisha nchi hii kuwa na matatizo. Katika uwezo wa Rais, ni mkubwa sana, kiasi cha kwamba mtu mmoja amepewa uwezo wa kufanya kila kitu katika nchi hii, na uwezo huo unadhuru watu wengi sana, ningeomba upunguzwe ule uwezo wa Raisi ili kwamba kuwe na mashirika mengine ambayo yatakua yanahudumia sehemu zile ambazo Rais anachukua. Kwa mfano, Rais peke yake ndio anauwezo wa kutoa ardhi kwa mtu yeyote katika Kenya. Yeye ni binaadamu, anaweza kukosea, halafu Rais anapeana uwezo ule kwa Commissioner wa Land, hakuna mtu mwingine yeyote ambaye anauwezo isipokua Commissioner Land, na yeye anapewa uwezo na Rais.

Kwa hivyo katika Majengo plots kuna matatizo ambayo yanasababisha watu kuwa na huzuni nyingi sana. Plot za Majengo kama alivyotangulia kusema Bwana Sumba, ziko katika sehemu ambayo kuna landlords, ambao landlords hawa walizinunua zile ardhi kutoka kwa watu binafsi. Mzee Kenyatta alipokuja alikuta kwamba watu wako katika Majengo ni ma-squatters, akatoa

amri kwamba nyumba za Majengo watu wauziwe zile plots. Zikauzwa zile plots baada ya kuafikiana kwa jumla ya shilingi alfu thelathini kwa residential plots, I mean commercial plots. Na residential plots zikawa ni shilingi kumi na tano alfu. Serikali ikachukua udhamini wa kwamba watahakikisha pesa zile zinapewa wenye viwanja, yaani landlords. Pesa zile zililipwa kwa DC lakini, ajabu ni kwamba hazijulikani pesa zile ziliwafikia wenye plots ama hazikuwafikia, kwa sababu ni watu nusu tu peke yake ambao walipewa title deeds. Na wengine mpaka leo wameshalipa elfu thelathini na alfu kumi na tano na hawajijui wako wapi. Na baadhi ya wale wengine landlord walikataa kuuza zile ardhi, ijapokua kulikua na directive za Rais lakini hawakufanya vile. Mpaka sasa bado wanakusanya zile shilingi mia tatu za monthly rent. Na wengine wame charge zaidi ya elfu moja mia tano. Na serikali iko na inaangalia na inajua kwamba watu wanapata matatizo. Kuna mwenyeji moja katika landlords ambaye yeye ardhi kubwa katika Majengo ni zake yeye. Yeye alipokwenda kwa Commissioner wa Lands akapewa title deeds za majumba yote ya Majengo badala ya kulipa shilingi alfu thelathini anakwambia tena utoe laki moja ama 50,000 ili ndio akupe title deed. Haki iko wapi jamani? Kwa hivyo tunasema ile Land Act inamruhusu Waziri wa Lands peke yake kutoa title deed, itakuaje mtu binafsi apewe uwezo wa kuchukua title deeds za watu wote alafu yeye awagawia watu?

Tunasema Commissioners ni lazima mwangalie mambo hayo kwa makini sana. Baada ya miaka kumi na tano ya kupitishwa kununuliwa kwa ardhi hizi. Huyu Landlord huyu huyu mmoja amechukua open space zote na amepewa na road reserve zote amechukua. Na hii yote amepewa na Councillors ndio wamempa uwezo wa kuchukua ardhi hizo. Sisi tunasema, ikiwa Councillors wale ambao walihusika kupeana ardhi hizi kwa mtu kama yule, katika Katiba tunataka kiongozi yeyote wa aina hiyo awe disqualified kusimama katika uchaguzi.

Tunasema kuna wananchi ambao ni maskini, katika ka zile alfu kumi na tano na alfu thelathini hawana uwezo wa kulipa, na serikali wanasema wana ondoa umaskini. Watauondoa umaskini vipi ikiwa wao wenyewe wanasababisha wananchi kuwa katika hali duni kama hii? Tunauliza serikali ichukue jukumu la kuhakikisha ya kwamba zile alfu thelathini na alfu kumi na tano wanazilipa ili kuondosha umaskini kama kweli wanaamini wataka kuondosha umaskini. Vile vile tunasema, Njonjo Commission of Inquiry, imezungumzia sana habari ya ardhi. Sisi tunapendekeza kwamba hiyo recommedation ya Tume ya Njonjo iwekwe katika Katiba. Na ionyeshe wazi kabisa kwamba recommendation hizo katika Pwani ardhi zake ni tofauti na katika Bara. Kwa hivyo wananchi wa Pwani wapewe haki katika zile nyumba zao zote walizo nazo wawe watauziwa zile ardhi na ile mali iwe ni yao wenyewe. Nikimalizia ninasema kwamba zile open spaces na road reserves ambazo zimechukuliwa kwa njia isio halali ziwe revoked. Na wananchi waregeshwe ardhi zile wajenge nyumba zao ama wajenge sukuli, hosipitali na mambo kama hayo. Kwa hayo na sema shukrani.

**Com. Ayonga**: Asante, Bwana Musa, unaweza kutoa hizo karatasi zako na ujiandikishe. Next atakua Habib Haba.

**Interjection**: Ashatoka huyu.

**Com. Ayonga**: Abdala Amani,

**Interjection:** Hapana usifuate orodha hiyo maanake watu wengi washakwenda.

**Com. Ayonga**: Waziri Muhamed, Yusuf Muhamed, hayuko? Mwinyi Juma Babu. Chukua nafasi. Huyu ni Mwinyi Juma Babu.

**Mwinyi Juma Babu**: Salaamu aleikum. Kama mlivyosikia mimi ndiye Mwinyi Juma Babu na ni mkaazi wa Majengo Ward. Natoa maoni yangu mwenyewe, sina memorandum. Nilikua na pendekeza tuwe na serikali ya Majimbo. Majimbo hayo yatakua na serikali kuu, yaani Central Government. Na kuwe na vyama vingi kama hivi tulivyo sasa. Kuwe na Rais mmoja, halafu kuwe na Makamu wa Rais wawili, yaani first and second Vice President. Huyu first Vice President awe ni Muislam, halafu tuwe na Prime Minister ambaye ndio atakua na uwezo mkubwa kuliko wa Rais. Halafu tuwe na Mawaziri ambao watachaguliwa na Rais. Halafu kila Jimbo kuwe na Governor, ambaye Governor huyu, atachaguliwa na wananchi au wanati, yaani wenyeji wa pale katika Jimbo lile na yeye pia awe ni mwanati. Na DO, DC na Chifu wote watafuata msururo huo huo wa wanati. Halafu hao hao kina DC, DO na Chifu watakua wao pia wamechaguliwa.

Tuje katika mali ya asili sasa, natural resources. Kila Jimbo lijaribu kuchuma ama kuleta uchumi wao iliwajifaidishe wao wenyewe katika Jimbo lao, halafu kupatikane kitu kidogo, mimi nimetoa maoni kama 10% ndio ziende kwa serikali kuu. Lakini 90% ziwe wenyewe Jimbo letu. Halafu katika hii mali asili watakao simamia hiyo mali, wawe ni wanati, sio mtu kutoka Eldoret, ama kutoka wapi aje atusimamie.

Nazungumza katika uajiri, yaani employment. Ningependekeza uajiri uwe angalau 75% iwe ni wanati, 75% watakao andikwa kazi wawe wanatoka katika lile Jimbo, halafu 25% nyingine watoke kokote kule watakako. Halafu katika idara za serikali, yaani parastatals, iwe wote wakubwa wale Commissioners ama wale head of department wawe ni wanati; isiwe pia ni watu wakutoka sehemu zingine kuja kuangalia au kusimamia mambo kama haya ya parastatals, ambao vyengine kutamka jina la Mwinyi pia hawezi. Halafu ofisi ya Chief Kadhi, ofisi ya Chief Kadhi yapendekezwa kua Kadhi apewe power zaidi, hata naona ikie kiwango cha Judge maanake mpaka sasa nafikiri ni Chief Magistrate. Halafu huyu Chief Kadhi achaguliwe Kiislamu. Awe elected, sio kuwa appointed na mtu ambaye hata si Muslim.

Elimu tuwe na free primary education, lakini iwe ni free kweli. Sio kama hii inavyoendelea mara unasikia kuna building fund, kuna nini, afadhali ile ile tuliokua tukilipa sisi inaonekana ni free, kulika hii ambayo ni free na sio free. Na kila Jimbo liwe na Chuo kikuu sio Majimbo yote hivi sasa yana University lakini nafikiri Majimbo mawili moja likiwa ni hili Jimbo letu halina University kabisa, wala halilifikiriwi kujengwa University.

**Com. Ayonga**: Time inakwenda.

**Mwinyi:** Tukiangalia na afya, tunaabiwa kuwa kuna free health ama free medical care, hatuioni. Kwa hivyo napendekeza pia tupate free medical halafu tuwe na local government kama hizi Municipality, ziendelee hivi hivi, kwa hivyo kwa hayo yote ndio niliokua nayo. Asanteni.

**Com. Salome:** Swali tu kwako wewe peke yako nafikiri ni kwa wewe vile ulivyo zungumza juu ya kuwa na uzalishaji Jimbo, tisaini kwa mia ya uzalishaji huo ukae umo ubaki kule kwenye hilo Jimbo. Hua pia umetupasha kua watu wengi wanataka Kenya ibaki kama ilivyo, moja. Kwa hivyo kuna wajizaji wauzalishaji ingawa sita kwa mia kwa Jimbo katika kusaidia ile serikali kuu, sasa tu tutajie kwa Majimbo yale utaita uzalishaji wa hali ya juu, una mwelekeo gani kwako hili tuweze kuyasaidia Majimbo pia?

**Mwinyi:** Katika maoni niliotoa, yale maoni ya asilimia tisaini ilikua ni maoni, lakini ikiwa asilimia kumi haikutosha serikali itafikiria kitu cha kuongeza, lakini kuwe na kiwango kikubwa ambacho kitabaki katika Jimbo.

**Com. Ayonga**: Asante ndugu kwa maoni yako, je una memo?

**Mwinyi:** Memo sina.

**Com. Ayonga**: Basi uende kule ujiandikishe. Rashid Suleiman Galgalo. Wapi Rashid Suleiman?

**Interjection:** Ashazungumza.

**Com. Ayonga**: Mzee unaweza kuendelea.

**Rashid Suleiman Galgalo**: Okay, Hon. Commissioners, wananchi wenzangu, mabibi na maBwana salaam aleikum.

**Com. Ayonga**: Tafadhali tuwe na kimia.

**Rashid**: Jina langu ni Rashid Suleiman Bagadi natoa maombi kwa ukumbi. Juu ya maoni yangu haya, yote mazuri ni yetu pamoja, mabaya mtaniachia mwenyewe, asanteni. Katiba tuitakayo Kenya: Katiba tunayoitaka watu wa Kenya ni Katiba inayo jali maskini, ni Katiba inayojali walemavu, ni Katiba inayojali wanawake, ni Katiba inayojali watoto. Ni Katiba inayojali na kuheshimu utawala bora. Ni Katiba inayeheshimu uhuru wa dini zote. Ni Katiba inayowapa motisha wote kwenye vipawa fulani vya kuletea manufaa ya taifa, ni Katiba inayo walinda na kuwapa motisha matajiri bila ya kuwadhulumu maskini ili waweze kuweka raslimali zao hapa nchini. Ni Katiba inayojali mahakama uhuru kwa maana ya uhuru. Ni Katiba inayojali uhuru na nguvu za mahakama ya Chifu Kadhi. Hapo hapo kufanya marekebisho katika mahakama ya Chifu Kadhi. Ili isiwe tu inauwezo

wa kuhukumu kesi za talaka na ndoa bali vile vile kesi za jinai. Vile vile kuweko katika mahakama ya Chifu Kadhi, mwanamke mwenye uwezo wa kielimu ya dini ya Kislamuu na ya kisheria za nchi hii. Ili aweze kuwahudumia wananwake wenzake kutokana na baadhi ya mambo ambapo wanawake hao hawawezi moja kwa moja kumueleza Kadhi au Chifu Kadhi. Na hilo litamwezesha Kadhi au Chifu Kadhi kujua kwa undani zaidi matatizo ya kijamii na kutoa ukumu muafak kwa wanao husika, yaani mwanamke na nyumba yake. Vile vile Katiba inayojali haki kwa wote yaani kusiwe yaani kama navyosema mwenyewe social inequality. Kusiwe na raia wa daraja tofauti tofauti, kama vile katika mfano wa kupata kitambulisho. Sio kwa mfano Ramadhani Salim ambiwe lazima alete birth certificate ya nyanya lakini Kariuki Johnson ambiwe tu alete kitambulisho cha ubatizo.

Katiba tunayo itaka Kenyans ni Katiba inayojali zaidi mambo manne. Nalo la kwanza ni dini, elimu, kilimo na afya. Yaani pesa nyingi za uma zitumike katika mambo hayo manne niliotaja hapo juu. Kwa sababu ikiwa kila Raia atakua ametosheka na masilahi yake ya kila siku hatakua na haja tena ya kushutumu au kuitakia mabaya serikali. Kwa maana hiyo haitakua na haja serikali kutumia mapesa mengi sana kwa jeshi. Na hayo yote yatawezekana ikiwa serikali zitakua ni za Majimbo. Asanteni.

**Com. Ayonga**: Asante mzee, unaweza ukaenda huko, ukajiandikisha: Muhamed Saidi.

**Muhamed Saidi**: Asante sana Ma-commissioner kwa kunipatia nafasi hii.

**Com. Ayonga**: Tafadhali tumpe ukimia hili aweze kuendelea. Kama tunaweza kusikiza tu.

**Muhamed Saidi**: Salaam aleikum. Makaratasi ni mengi lakini mimi nataka summarize kwa hiyo sehemu ulioniambia, na jambo la kwanza nataka lianzia, ni kuhusu mahakama ya Kadhi. Wajua ijapokua inatajwa sana, kila mmoja anajia vile ambavyo anaipresent. Katika mahakama ya kadhi, tunapendekezo la Kadhi Surbodinate Court ambacho kiwango chake iwe sawa na Chief Magistrate. Na daraja nyingine iwe ya Kadhi High Court ambayo kiwango chake iwe sawa na Judge wa High Court. Kisa kiwango cha tatu, iwe ni Kadhi Court of Appeal. Katika haya mahakama haya matatu, kama kesi imetoka kwa Surbodinate Court inaweza kwenda appeal; ya kwanza kwa Kadhi's High Court na appeal ya tatu iende kwa Kadhi's Court of appeal na hapo iwe mwisho wa kesi hiyo. Isiwe kama vile inavyoifanyika sasa, inatolewa katika upande wa Kadhi's Court kisha inapelekwa kwa mahakama ya High Court ambayo Ma-judge wenyewe sio Waislamu.

Sasa narudi katika uchaguzi wa Kadhi's Court, Surbodinate Court, Kadhi mwenyewe, Chifu Kadhi na Kadhi's court of appeal. Uchaguzi huu wote nilazima kuweko na national committee ambayo kwa wakati huu hatuna committee hii, ambayo qualification ya hao national committee itakua in machehe na wale maulamaa, maulamaa ni wale ambao ni scholars katika Islamic religion ambao wana shahada kutoka viyuo vikuu mbali mbali kuhusu mambo ya dini. Committee ile ndio itakua kazi yake kuwafanyia interview wale Makadhi na kupeana recommendation yao ambayo kule inapokwenda inakua nikama formality, lakini kila kitu washamaliza. Na Kadhi Surbodinate Court, tuna shida nyingine watu wasafiri kutoka Kwale au

watoke Taita huko wawe wanakuja Mombasa kwa mambo ya ku-attend Kadhi's Court, Tunapendekeza ya kua hii Kadhi Surbodinate Court, iwekwe katika kila district. Na Kadhi's High Court ambayo itakua ndio Court ya pili kutoka Subodinate court iwekwe katika kila Province. Na hii Kadhi's Court of Appeal ni ile ambayo itakua stationed Mombasa na itakua ina move kama vile inavyo move ile Court of Appeal nyingine. Na mtu kuwa Kadhi katika ile condition nyingi lazima ziwekwe kama umri wake awe baina ya 35-60 years. Na awe amesomea sheria za Kislamu kutoka Chuo Kikuu cha Kislamu kinachotambuliwa, na yeye mwenyewe awe na tabia nzuri zaa Kislamu, na ambaye anakubaliwa na wengi katika ile committee ya Machahe na Maulamaa. Na kama kawaida, hii nafikiri ni natural, lazima Makadhi hao wote wawe wenyewe wameoa.

Sasa nikitoka hapo narudi katika power za President. Kama vile mnavyo elewa serikali yetu ina mikono mitatu, Legislature, Executive, na Judiciary, yaani wabunge, na cabinet, na kisha tuna mahakama. Sasa ukiangalia katika haya mambo yote matatu kama ambayo yote yanaongozwa na mtu mmoja. Kwa ile power aliopewa. Sasa pendekezo langu ni kua, upande wa hii Executive, kuweko na President, Vice President, Ministers kama kawaida, lakini hawa mawaziri, wachaguliwe na bunge lenyewe. Kwa sababu yake itakua ile nafasi ya mtu mmoja kuonelea asubuhi alikua ni Waziri, saa saba anasikiza news anaambiwa kama umeaondolewa itakua hakuna kusikia hizo. Na kisha vile vile mtu mmoja yule, ndiye ambaye anachagua kuanzia Ma-judge wote, sasa itakua kesi yeyote ambayo inapelekwa ule ukweli wake haipatikana shauri yule Judge alioko pale, pia yeye anatakalinda hile post yake aliyonayo. Yule aliomchagua ndio ambaye amemweka pale kwa hivyo ni lazima vile vile asikize pale.

Tukipeana mfano mdogo hapo hatutaja jina. Lakini kulikuako na Waziri msaidizi ambaye alishtakiwa tu mambo ya sukari kidogo kesi ilopelekwa saa nne asubuhi ya ile kukataa kesi ikatiwa tarehe saa saba ya tangazwa uwaziri mdogo hana tena. Lakini kuna Waziri ambaye alipelekwa mahakamani na akienda mahakamani anaenda na bendera na ma-body guard wake mpaka kesi ile ikamalizika na kesi ile ikatupiliwa mbali. Hakuondelewa Waziri. Nafikiri Ma-commissiner kulikobakia nyinyi mtamaliza. Sasa kwa sababu hiyo, powers za President mziangalie sana katika section hiyo. Tukija upande wa nominated MP ambaye President tena anapewa power kuchagua. Katika Kenya nafikiria Waislamu tuko Karibu 12M, 12M tumezidi one third of the Kenya Population. Ikiwa tumezidi one third of the Kenyan Population inamaanisha katika wale Wabunge12 ambao nominated Waislamu lazima wangechaguliwa at least four of them. Lakini hilo halifanyiki.

Sasa Judiciary nayo; rules zenyewe nikama vile mnavyojua yaweza kwambiwa kesi fulani umfunge mtu kuanzia one day umepewe maximum ten years. Lakini sasa kwa vile kua kuna ile influence dani yake ya yule aloweka pale kwa mfano. Inakua sasa unaangalia hapana, hii kesi huyu anafaa kupata only three weeks kisha halafu aripoti katika kifungo cha nje kwa miezi sita. Kesi kama ile ile imepatikana na yule ambaye anakutwa yeye atakafungwa kabisa asizungumze tena, anapewa maximum sijui miaka tisa na nusu. Sasa nafikiria hapo kidogo naondoka na rukia mahali pengine. Katika mambo ya elimu, kama mnavyo elewa maskuli yetu yameenea kila mahali, elimu ni hiyo ambayo twambiwa ni ya bure, lakini ni hiyo bure ni theoretically, practically we are to pay. Sasa kitu kimoja hapa kilichoko nikatika hii dini yetu ya Islamic Religious Education. Hapo ni msibha mkubwa sana, skuli ambazo hata katika mkoa wa Pwani wote twaweza kwambia, ndani ya Mombasa District hapa katika

Mkoa wa Pwani na ndio headquarter ya Islamic religion katika Kenya nzima, Wanafunzi wa Kislamuu wanalazimishwa, sio by force, lakini indirectly. Wajua waweza kulazimisha mtu – directly and indirectly. Indirectly wanalazimishwa paper itakuja katika standard eight ya exam afadhili mchukue CRE kwa sababu yake hakuna walimu wa IRE na sasa kama hamkuchukua CRE itakua hii paper wewe uta-fail wakati wa exam. Sasa inakua wanafunzi wa Kislamuu wanachagua CRE na Commissioner ikiwa unataka majina ya skuli naweza kukuletea privately.

Sasa la mwisho, nataka summarize, katika kusummarize kwangu, ningegusia mambo madogo madogo hayo. Issue kama ya National Identity Card. Nafikiri katika hii Katiba ya sasa inatupa sheria ilioko nikua ni sisi tuende tu-apply kwa National Identity card uwe nayo baada ya 18 years. Lakini hakuna sheria inayosema ni lazima tubembe tuzunguke nayo. Kwa hivyo ingekua hiyo iwe recorded katika hii Katiba mpya ya kuwa tusisibuliwa na habari ya ID. Na Ma-Commissioner nikiwaeleza hivyo ni kua, polisi wale wale ambao wa Kenya, vile ambavyo wana-behave hapa Mombasa, polisi wale wale ni tofauti wakikuona up country vile wana behave. Nairobi police wanatuheshimu kabisa, lakini nikitembea hapa Mombasa hawaniheshimu. Kwa hivyo kwa hayo machache, napendelea kidogo kama time iko ningeendelea zaidi lakini na kwenda kujirekodi pale, lakini kidogo ningemuomba Com. Wambua, usije ukaniona Mikindani siku ya alhamisi ukasema nilikuako hapa. Hapa nimekuja in my capacity as a leader of the Mosque, Mikindani nitakuja in my capacity as a treasurer wa Changamwe Mosque.

**Com. Ayonga**: Hebu kwanza endelea na hayo mtaongea na Com. Wambua baadaye.

**Rashid:** Ndio.

**Com. Ayonga**: Kama nilikusikia vizuri, umesema Mawaziri wachaguliwe na Bunge, vile nilivyosikia ni sawa?

**Rashid:** Ndivyo

**Com. Ayonga**: Lakini sasa nataka kukuuliza, hukutwambia kule Bunge ni nani ambaye angechagua Mawaziri kwa maana kwamza tuelewe kwamba watu wote waliomo katika Bunge wamechaguliwa. Wamekuja wote ni Wanabunge. Sasa unapofikiria hao Wanabunge kila mmoja angependa awe Waziri, sio? Sasa nani angechagua Mawaziri kati ya hao wote ambao wamefaa pia kuwa Wabunge kuwa Mawaziri?

**Rashid**: Asante sana Commissioner, kitu kilichoko system nafikiri unaelewa vile tunavyo chagua Mayor katika mabaraza. Mayor yule anaingia anaingia kama Diwani pale kisha kutoka Councillors zinakua vile vile. Kwa hivyo the same system Wabunge wakishainga pale katika ka Parliament.

**Com. Ayonga**: Wachaguane.

**Rashid:** Katika ambaye ni Mbunge yuko pale ana chance ya yeye kupigania ule u-president.

**Com. Salome**: Asante sana kwa maoni yako Bwana Rashid, kila mahali tumeonyesha wadhifa ule unatumiwa kuwachagua Wabunge wachague Mawaziri. Unajua kila mahali tunaenda tumeeleza kuwa Madiwani wasimchague mayor, Madiwani wasimchague chairmen, walimu wameingilia hiyo nafasi vibaya sana, sasa nawe unasema hiyo taratibu kwa hivyo haukukana kwenye udiwani sasa tuupitishe kwenye bunge, je maoni yako ni nini?

**Rashid:** Asante sana Madam, kitu kilichoko hapa ni lazima tuelewe ya kuwa hao waliotoa, walitoa maoni yao, no. 1. No. 2 mabaraza tulio nayo kama kwanza sasa, baraza tulionayo katika Mombasa sasa, utakuta ya kua sio kama yale mabaraza yalikuwako zamani, wale walikua ni watu ambao walikua na exeperience, wanaujuzi, lakini hao mabaraza tulionalo sasa ni lile baraza kila mmoja alikua yuwakaa angalie lile tumbo lake. Qualification za mtu kuchaguliwa kama Diwani zilikua pia hazifuatwi namna hiyo. Umeinua mkono ku-support the motion na mimi na-support wewe umenielewa? Na Wabunge wenyewe wale ambao watachaguliwa hawatachaguliwa Wabunge ambao sio watu ambao wana paper qualification au hawanaexperience ya kutosha. Watachaguliwa highly learned people ambao wana integrity, ambao wana personality, ambao wanajua zile shida ambazo zinawafika Raia. Na wale tuelewe kwamba wale ni indirect democracy kwa maana wale ndio wanawakilisha ile Uma. Uma hauwezi kuchagua mtu ambaye ni bunga wakampeleka kule, watamfuata mtu ambaye nisawa, sawa,ambaye anaweza kuwakilisha watu mpaka kuchagua kwa Rais ni jukumu lake. Nafikiri nimejibu kwa kutosha.

**Com. Ayonga**: Asante, ndugu Rashid, sasa kwa hayo maandishi yako uyatoe kule na ujiandikishe. Next ni Muhamed Abedi.

**Muhamed Suhed Abdil**: Salaam aleikum. Mimi ndiye mwenyeji wa hapa Headmaster wa sukuli hii, sikupendelea vile watu wanavyo kaa, pengine saa nane tutakuja badilisha wanaume wakae bali na wanawake wakae bali. Kwa sababu shule hii ni ya mfumo wa Kislamuu.

**Interjection**:Jina lako?

**Muhamed**: Muhamed Suhed Abdil. Jambo la kwanza ningependa Katiba ishughulikie sana juu ya kabila la Waswahili. Waswahili hawatabuliwi katika Katiba tuliyo nayo sasa. Waswahili ndio waliotoa lugha ya taifa katika Jamhuri ya Kenya na nastajabu mimi mwenyewe nilipokua Chuo Kikuu ndio nilijua kunawaswahili. Lakini upande wa primary, secondary, watoto hawafundishiwikuwa kuna kabila la kiswahili. ambayo hii ni kinyume kabisa. Ukiangalia map za Kenya waswahili wamewekwa katika Indian Ocean. Sijui wao ni samaki au ni binadamu. Kwa hivyo twaomba litabuliwe kirasmi Waswahili kwa ufupi wako aina tatu lakini sitaki kutoa tarehe yao. Kuna kitabu ambacho kimeandikwa na Shahabudin Sheragdin. "Kiswahili na wenyewe", katika dunia hii hakuna lugha isio kuwa na wenyewe kabisa, na Waswahili wanautamaduni wao, wana nyendo zao, na kila kitu, kwa hivyo kwa nini wasitambuliwe kama kabila katika Kenya hii. Kwa hivyo twaomba ma-commissioner wetu

swala hili walizingatie vizuri sana.

Na twataka pia proportional representation katika serikali ya mfumo mpya wa Katiba hii. Sisi twajua Waislamu hapa tuko thuludhi nzima katika jamhuri ya Kenya. Leo ukiangalia mawaziri ikiwa ni thelathini basi Waziri mmoja ama wawili ni Waislamu. Kwa hivyo ikiwa ni thelathini kumi twataka wawe ni Waislamu. Jambo jingine ni kua, hapa jirani yetu Tanzania kuna Katiba inayosema Rais akiwa anatoka Tanganyika basi Makamu wa Rais atoke Zanzibar, kwa hivyo Katiba mpya tulishugulikie jambo hili, ikiwa President atakua Mkristo Vice President awe Muislam. Katika General Election itakayo kuja Muislam awe Rais na Rais mdogo awe Mkristo, ikiwa Malawi wana Rais Muislam kwa nini na sisi tusiwe na Rais Muislamu katika nchi ya Kenya.

ID cards: sisi tunabaguliwa vibaya sana tukienda kuchukua ID cards, sisi ni wenye lugha ya taifa lakini tukienda kule twabaguliwa. Mimi natoa ID card yangu ya the first generation ya Nyayo nataka kuchukua hii mpya naambiwa toa ushaidi zaidi kuonyesha wewe ni mwananchi wa Kenya. Mimi nishapata hile card kuonyesha tayari mimi ni mwananchi halafu nambiwa nitoe ushahidi zaidi, ushahidi zaidi ya aina gani? Maanake ukienda kule utambiwa ulete certificate ya babako, ya nyanyako, ya nyanyake nyanyako sijui na nani. Kwa hivyo ubaguzi namna hii uondolewe kabisa. Mtu akienda akitoa jina lake, ato birth certificate yake apewa kitabulisho kama hao watu wengine wanavyo fanya. Ikiwa kama wewe unaitwa James, unaitwa Jane ama nani unapatiwa kitabulisho chako bila tabu. Lakini kama wewe ni Muislam jina lako Muislam, ikiwa basi utaonekana labda unatoka Eskimoland, Mars, Jupiter, ama unatoka wapi?

Na ningeomba kuwe na kifungu, kukataza wanasiasa wetu hata ikiwa ni Rais kusema nchi hii ni ya Kikristo. Hii nchi si ya Kikristo hii nchi ni ya watu wote. Na twataka mfumo mpya wa serikali hii iwe wa Majimbo, tuwe na Majimbo, kila moja awe na Governor. Mimi sitaki ati Vice President. Tuwe na Governor ambaye ataweza kututawala. Na Jimbo kama la Pwani ambao majority ni Muslim, North Eastern Province tutawaliwe na sheria ya kidini ya Kislamu. Wale ambao si Waislamu watashugulikiwa na Federal Law. Kwa hivyo twaomba serikali ya Majimbo kuwe na Rais ambaye ni Executive President, ambaye atakua na madaraka, lakini President huyo he should not be above the law. Ikiwa amefanya makosa aweza kuteremsha cheo chake akaondolewa.

Na vile vile twaomba wakfu, wakfu za Kislamu, mali ya Kislamu uisimamiwe na Waislamu wenyewe, sio aje mtu kutoka Bara aje asimamie wakfu za Kislamu, hiyo hatuwezi kukubali. Twaomba serikali ambayo itasimamia wakfu za Kislamu. Na katika census ambao tunafanya za kujua idadi za wa Waislamu, ni wangapi katika Kenya hii? Maanakae haitolewi hesabu ya Waislamu hata siku moja.

Na Koech Commission imezunguka nchi yote ya Kenya na wananchi wa kasema hawataki 844 system lakini serikali ni lazima kufuata mfumo huu. Sisi twasema twataka mfumo wa zamani wa 7423, kwa sababu 844 haiwapi watoto wetu wa Kislamu nafasi ya kusoma dini yao.

Na Rais akiwa anachagua Mawaziri, anachagua Parastatal, anachagua permanent secretary wale wawe elected na MP’s katika

bunge si mtu yeyote tu kama mtu rafiki yake anahusiana naye ama ni kabila lake anamchagua na hana uwezo au hana elimu ya kutosha ya kuendesha idara ile.

**Com. Ayonga**: Nasikitika saa zimeenda.

**Muhamed:** Nina mawili matatu na ya mwisho, kwa hivyo twaomba wale watakaochaguliwa wawe vetted na MP's katika bunge sio mtu yeyote tu yuwaweza kuchaguliwa. Twaomba pia vile vile Idd ul Haj iwe ni public holiday katika Kenya. Na vile vile twaomba ikiwa nchi kama Japan na China imeendelea sana katika technology kwa nini Kiswahili kisifanywe medium of instruction katika skuli zetu za Kenya? Na Kiingereza kifundishwe kama somo tu la kawaida. Na time naambiwa hakuna lakini twaomba vile vile Katiba mpya mtu akipewa kazi moja iwe ni kazi moja, sio mtu apewe kazi kumi mtu mmoja na wakenya karibu million ngapi hawana kazi ya kufanya.

**Com. Wambua**: Umesema ni maoni yako Rais akiwa ni Mkristo naibu wake awe ni Muslim, lakini hukasimamia hapoa, hukusema je Rais akiwa Muslim, Mkristo ndio atakua makam. Maoni yako vipi?

**Muhamed:** Ni hivyo hivyo maanake mwaka mmoja miaka mitatu ile ikiwa Mkristo ni Rais, Vice President awe Muslim. Next General Election Muslim awe Rais Vice President awe Mkristo.

**Com. Ayonga**: Ndugu unaweza kwenda kule ukaeka maandishi yako kule na pia ujiandikishe jina. Ili tufanye mabadiliko kidogo, lazima kuna wamama kati yenu ambao wamejiandikisha hapa ambao hatuwezi kutabua majina yao, nivingumu kuyatambua, yanaweza kua kule chini, bona tusisikie sauti ya mama akiongea. Kuna moja hapa ambaye aitwa Zubeda Suba.

**Zubeda Sumba**: Jina langu naitwa Zubeda Sumba. Mimi nawakilisha District Development Committee Mombasa. Nazungumza hapa kama mwenye kiti. Na maoni haya ni yetu yote ya district nzima. Katiba ya Kenya iangalie masilahi ya wananchi bila ya mapendeleo. Mfumo tunao sasa ni wa Majimbo kila Jimbo lifanye mambo yake likisimamiwa na mwenyekiti wa Jimbo lile. Na pia watu wa Jimbo wapewe sifa umbele kwa upande wa kuajiriwa kazi, kama kuna, university ama tasisi zozote watu wa Pwani wafikiriwe kwanza, na kwa upande wa colleges na maskuli pia iwe ni hivyo hivyo. Na kwa upande wa ardhi, watu wapale wafikiriwe kupewa ardhi kabla ya kupewa wageni. Kila eneo la bunge, ama constituency wa pale kuwe na kiti kimoja ambacho kitagombaniwa na kina mama. Pia tunapendekeza wale ambao wako mahosipitalini amabo ni wa Kenya na wanaweza kuongea wakachukuliwe maoni yao kwa sababu wao pia ni wa Kenya. Pia tungeomba wale ambao niwafungwa, yaani prisoners wao pia ni wakenya, ningeomba Commissioners waende kule wakachukue maoni yao kwa sababu na hao pia wanamatatizo yao. Pia ningeomba kwa upande wa polisi na Kadhi's Court, kuwe na women day, kwa sababu ki maubile yetu ama kizalendo hua si sana mwanamke kwenda kwa mwanaume kumweleza shida zake zote. Kwa vile zile women dates zatatusaidia kutoa maneno yetu bila ya hofu yeyote. Kwa upande wa Kadhi na kwa upande wa polisi. Asante.

**Com. Ayonga**: Asante mama Zubeda na unaweza kuchukua hayo maandishi yako, kabla huja chukua, mama mwenzako ataka kukuuliza swali. Na yule mama mwingine ujiweke tayari.

**Com. Salome**: Asante sana mama Zubeda nina swali moja kwako, umesema kwamba kila kikao cha bunge ni vizuri kingekua na kiti moja cha kina mama, sasa unamaanisha kiti kile kiwe tofauti na cha kumpeleka mbunge kwa bunge au vipi? Tena nina swali lingine, umesema pia kwenye polisi na kwenye kikao cha Kadhi kuwe na desk ya kina mama za kuwahudimia, ni huku tu kwenye akina mama wanapata shida ama kungekua (inaudible) na kina baba na kina mama (inaudible) tunasikia zaidi ya wanaumi kumi ndio tusikia maoni ya kina mama, je unaona hata vifaa kama hivi (inaudible).

**Zubeda:** Ingekua bora, kama akina mama wangekua na kikao chao kwa sababu sio wengi wetu wanaweza kuzungumza mbele ya umati wa wanaume kama huu. Ndio ukaona tumekuja wachache na si wengi ambao wanaweza kuongea lakini tukiwa wanawake peke yetu tutakua na uhuru mzuri wakusema yale matatizoyetu tulionayo. Na kwa upande wa kiti cha bunge. Wanaume ni wenzetu lakini wanatungadamiza sana, kwanza hutumia pesa nyingi kung'ang'ania zile viti. Ukiangalia sio wanawake wengi ambao ni matajiri lakini ikiwa kile kiti kitatengewa katika kila constituency Kenya nzima hapo tutapata wanawake katika bunge. Kwa sababu vyovyote vile watakavyo ng'ang'ana lakini lazima mwanamke mmoja ataingia. Kwa hapo tutakua na wanawake lakini kama ni hivi tu wanatudang'anya.

**Com. Ayonga**: Asante mama Zubeda, yule mama mwingine jina lako ni nani kwanza ili nijue kama uko katika orodha.

**Mariam Sabit**: Jina langu ni Mariam Sabit

**Com. Ayonga**: Okay unaweze kuendelea mama.

**Mariam Sabit**: Salaam aleikum. Natoka Pambo Women Group, mimi naitwa Mariam Sabit ambaye ni Chairlady wa Maendeleo ya Wanawake Mombasa District. Leo nimekuja kuwakilisha kikundi changu ambacho chaitwa Pambo. Kikundi cha akina mama ambacha kinafanya miradi ya kuweza kujipatia maisha na elimu ya watoto wao. Utangulizi: Kwenye utangulizi katika taifa ni muhimu kwa sababu hii tutadumisha heshima, mapenzi na heshima za kuheshimu haki za kibinadamu ili tuishi pamoja kwa udugu na kuelewana kama one nation, yaani taifa moja, ni lazima tujitafutie kitu ambacho kitakua ndio nguzo yetu. Na guzo yetu iwe ni Kiswahili maanake lugha zilizoko ni nyingi na tukianza kufuata hizi lugha tutaona tunabaguana. Japo lugha ziwe ni za kinyumbani lakini Swahili iwe ni national language.

Uraia : Uraia wanawake kidogo hapa wameonewa, mke akija tolewa na mme kutoka nje yule mume hapati uraia, kwa hivyo tungependa, mume naye apate uraia. Habari ya ID cards, black as I am, it took me three years kupata card ya ID just because jina langu naitwa Mariam Sabit. Nimeenda Veto mara nyingi sana kwa hivyo haya mambo tunaona kama Waislamu ndio tunaonewa. Vyama vya kisiasa; vyama vya kisiasa twataka viwe viwili maana vingi vinatuvuruga. Ikiwa hutaki hichi utakwenda

hichi. Watangulizi wa taifa hili walipoanza walianza na chama kimoja na wakati wa chama kimoja mimi naweza kusema wakati huo ulikua mzuri kuliko huu chama cha watu wengi. Tumevurugwa ile kwenda mbele.

Muundo wa serikali: Muundo wa serikali hauja mpa mama haki yake. Tunataka affirmative action kwa sababu hatuna nguvu za kupigana na kina baba na culture yetu haituruhusu wanawake siku zote ni watu wenye haya. Kwa hivyo 20-30% tupatiwe kina mama na wale wasiojiweza vile vile. Nomination hizi zichaguliwe special commission bila hizo nomination hizo zitakwenda kwa wasio stahili. Serikali za mitaa; tunataka ma-councillor waende kwenye practical test hajue standing orders za local authority, ajue kwa nini yuko pale, kwa sababu nasikitika lakini ni maoni yangu na ya wenzangu wanawake wengi hawajui kwa nini wako pale. Haki za ki msingi, maji, chakula, elimu, serikali lazima iangalie. Kwa sababu mama leo akienda kuzaa ladigirigi hana maji kuna mtu pale anauza maji kidebe shilingi tano cha maji ya moto. Mama huyo kweli ataweza kujihifadhi? It is very devastating, ni kitu cha kusikitisha. Kwa hivyo mambo kama haya yataka tupawe nafasi tuangaliwe sisi kina mama.

Watoto wetu machokara, wao pia wana haki ya kuishi na ni watoto wetu. Je tuwaache barabarani? Si sawa, Local Authority, Municipal Council lazima katika department ya social welfare, iwe na mpango ya hao watoto. Kwa sababu maskini ni wengi matajiri ni kidogo, kesho watakungeukia. Kwa hivyo haki zao ni lazima zitizamwe wafanyiwe hata kama ni center ya kufanya handcraft, na wao wajipatie namna. Kina mama katika hali ya kujidumisha ki fedha, kina mama hawana uwezo wa kutoa mikopo kutoka katika benki kwa sababu interest ni kubwa sana. Kwa hivyo Katiba inataka iangalie kina mama wale wanatozwa 5% to 10% (inaudible) hili tuweze kuji-power economically, tuweze kua na kufanya kazi. Tunajibidiisha sio wavivu kama vile tunavyo sema ya kwamba tunaongoja maembe yanguke, la katika vikundi vyetu sisi wenyewe tunakopeshana kwa shilingi tano faida. Kwa hivyo tunaomba Katiba itufikirie. Kuna wale wanao rape, kumnaridhi maBwana, wale wanao rape tunataka wakatwe au wafungwe milele. It is a very, very bad thing ni kitu kibaya sana jamani, kina mama wengine wanapata tabu sana, ni jambo la aibu, lakini ni lazima tuliseme tuwalinde wale kina mama wenzetu na watoto wetu mitaani. Serikali lazima iangalie. Bibi na Bwana wakiachana ikiwa walichuma mali lazima wakati anamwacha yule bibi kidogo amgayie maanake alipokua yeye akienda kazini kutafuta zile pesa mama alikua anahangaika kumuifadhia chakula kizuri na nyumba safi. Sina mengi hila hayo.

**Com. Ayonga**: Asante sana lakini ngoja kidogo.

**Com. Salome**: Asante mama Mariam, (very inaudible but just to summarize the question) huja tueleza vile tunaweza kuwafanya hao watoto chokora wasiende mitaani.

**Mariam**: Kwanza ningependa kusema tuwe na social workers, ambao social workers watafanya test work. Watawangalia wale watoto individually wajaribu kuwa console mpaka waone wamekua kisawa sawa. Na zamani kulikua na social workers lakini sasa tumepoteza direction, mambo haya hayako tena, na vile vile, kitu kama affiliation kwa sababu mama ameshindwa, baba amemtoroka hana uwezo anamwachilia mtoto anaenda barabarani. Wakati kulikua na affiliation tulikua hatuna mambo

kama haya. Mambo haya yamekuja sasa kwa sababu ya shida hizi kama za affiliation kuondolewa. Na yote hii ni kwa sababu bungeni kule hatuna kina mama wengi.

**Com. Ayonga**: Asante mama unaweza kutoa maandishi yako kule naujiandikishe. Omari Babu Suleiman, Peter Mwasi, Rashid Muhamed, Julius Juma, Bahari Mang'ar.

**Fadi Matano**: Salaam aleikum

**Com. Ayonga**: Unaweza kutupa juu ya memorandum yako, yale makubwa makubwa mengine utatwachia baanda ya kusoma.

**Fadi Matano**: Nimekuja kama mwakilishi wa Ridhwan Mosque. Majina yangu ni Fadi Matano, lakini shindano kuu yaliyokokwenye hino memorandum maanake nina yangu mwenyewe ambao mtaisoma mbeleni. Maoni yangu ni kua utangulizi wa Katiba hii mpya ya Kenya iseme hivi lakini nita-state kizungu maanake iwe ni fasaha kwenu. The people of Kenya should be sovereign than the Constitution. The Constitution or the Legislature should overrule policy and that no policy overrules the Legislature or the Constitution. Kwa mwananchi: mwananchi awe ni mwenye kulindwa kutokana na viongozi lakini si viongozi kulindwa kutokana na wananchi. Uakilishi bungeni- kuwe na muundo mwingine wa kuwakilisha maoni ya wananchi bunge, ila tu si kwa mbunge pekee, maanake mbunge anaweza kukataa maoni ya wananchi, kwa hivyo kuwe na watu kama vile representative wa youth, women au disabled kupeleka maoni ya watu tofauti bungeni.

Kwa upande wa ardhi: Ardhi zilizochukuliwa kwa watu na kujengewa hifadhi zingine kama vile Airport, Bamburi Cement, Oil Refinery, ziwe ni zenye kupewa wenyewe au wenyewe kupewa ridhaa ya kuwaridhisha. Kwa upande wa mazingira: Mazingira hua ni yenye kuchafuliwa na wanadamu na kwa serikali kuhakikisha kua mazingira ni yenye kua masafi, serikali iwe ni yenye kuwapatia wananchi vifaa vya kufanya kazi ili watu wawe wenye kukakaa makwao, sio mtu atoke kwao aje huku ajenge kibanda au slums na kuleta uchafu mjini. Na viongozi au wakubwa wa serikali ningesisitiza kua serikali ihakikishe kua maafisa wa serikali wako maofisini na endapo mkuu atatoka ofisini basi naibu wake awe ni mwenye kua ofisini. Na la mwisho maanake nazungumza shida yetu tulionayo hapa mtaani ni kwamba pia machifu wawe ni wenye kupawa AP, kwa tatizo lote litakalo tokea la wananchi. Sina mengi asante sana.

**Com. Ayonga**: Asante ndugu Matano, unaweza kutwachia hiyo memorandum kule na ujiandikishe. Next. Je kuna Mwinyi kiBwana? Endelea.

**Mwinyi KiBwana**: Salaam aleikum. Bwana Commissioner nikikuomba radhi, umezungumza mazungumza ambayo yameshazungumzwa, lakini kuna feething problems hapa, watu wa Coast wameketi kama watu kwamba hawako Kenya. Kama alivyosemwa yulei kijana ni British Protectorate. Tatizo, ukianza Lunga Lunga mpaka sehemu za Lamu, hakuna mwananchi au mwanati mwenye title deed. Mkikuyu akiuziwa ardhi leo siku ya pili anapewa title deed. Where are we heading

to? Nimezunguka Kenya Bara kwote huko lakini ni kifika hakuna problem ati mtu mwenye nyumba analipa rent, ni sisi hapa wajinga ambao twapiga kura Kanu bado tuko kwenye hiyo problem. 90% or 96% of the land is owned by the Asians here or people who are not indigenous. How did they acquire this land? Where did they get this land from?\. Sisi tumerudi twatolewa wapelekwa Mishomoroni, wapelekwa Kwale wapelekwa wapi, mpaka lini tutaendelea namna hii? When we go back to my point, Commissioners nafikiri hivi sasa mkisema mtafanya constitutional review it is a joke, you are going to make Cosmetic changes to the existing Constitution. Kitu kilichoko wekeni election, wekeni presidential powers na vitu vichache mbadilishe. Mngoje election imalizike muanze kuleta review ya kisawa sawa. President mimi ningeomba awe na running mate, sio President asimame Kamukuji amchague Vice President, akichua kua yeye ni President, Vice President yake ni nani? Asimfute asubuhi wakati anakunywa chai wala asimchague kwenye radio.

Halafu upande wa election, watu wa Mombasa tumelala sisi, au watu wa Pwani. Utakuta Mjaluo ametoka uko kwao amekuja kusimamia Kongowea, Kongowea hakuna mwenyewe? Constitution igeuzwe ifanywe indigenous people wa pale wasimame sio Mjaluo na Mkamba. Hii hapana football team ama football ground mtu yeyote anaingia ndani anacheza.

Halafu tukienda kwa upande wa Chief Kadhi, Chief Kadhi ni senior Magistrate but it is a shame seeing him walking from Magistate's Court to Majengo ambapo the same rank with him, ako na gari, Chauffeur driven anakaa Nyali. Kwa nini sisi Waislamu tunadharauliwa? It should be put in the Constitution, all the privileges wale wanapata watu wengine na Chief Kadhi apate. Halafu system ya Kadhi's Court, it is very peculiar, they is no court of appeal kwa Kadhi, kadhi anamaliza kesi mtu ana appeal Muislam ana appeal inaenda kusikizwa na Njoroge, Kamau, Njuguna ama Otieno who are not conversant with Quran or Islamic sheria. Our rights been taken away, kwa hivyo lets get our rights we as Muslim people in general.

Halafu nauliza Ma-commissioners, mmeanza nyinyi kuanzia Turkana mpaka wapi wapi, all these what you are taking here, will they be considered ama mwisho mtakwenda kwenye Parliament ile inavyotaka Kanu iwe hivyo? Maanake watu walikwenda mbio section two hile kugeuza Katiba ya vyama vingi Kanu ilipokwenda kule Kasarani siku ya tatu ikabadilishwa kwenya Bunge. Je haya mnayafanya will it be taken seriously?

**Com. Ayonga**: Mimi ningalipenda utoe maoni kwa maana ukituuliza maswali sisi hatutakujibu, kitu amacho ningalipenda ufanye ni kutuambia tunataka hii ifanywe namna hii, namna hii hayo ndio maoni. Lakini sasa ukituuliza maswali sisi tutatoka bila jawabu.

**Mwinyi:** Sasa ningeomba ikiwa Constitution itapendekezwa na Raia, chama chochote kisitie mkono iwe ni mapendekezo ya wananchi. Halafu kitu tunacho omba, katika Pwani kuwe na quota system, quota system on employment, kama waliotangulia kusema wanasema katika employment utaona Mombasa hakuna maofisi ya kuandika watu kazi, watu wote wanaoandikwa kazi wanatoka Nairobi, lazima kuwe na autonomy ya KPA mtu wa KPA Managing Director aweze kuandika kazi watu hapa, Customs iandike watu kazi na hata sections waandike watu kazi hapa hapa, sio mtu anaandikwa kazi Nairobi halafu analetwa

Mombasa. Watoto wetu wanabakia viwanjani kunyang'anya mama mkufu, kuuza bangi, kuuza unga, that is our problem now.

Tungeomba Constitution ikibadilishwa sisi tupewe quota system yetu, ambapo watu wa Pwani ikiwa ni Managing Director awe ni wa hapa, personal officer awe ni wa hapa. Leteni engineer kutoka Nairobi, atoke Engineer, wale vyeo vingine wapewe lakini where there is a small bit, hii kazi ya mkono ya kufagia, ama kama moja alivyo sema, meter reader, ile kuzunguka na machine ya kuangalia pale. Hiyo itakua ni maonevu. Hiyo Constitution itakua haijapeleka mambo kisawa sawa, twaomba itufikirie sisi watu wa Pwani. Na itie mambo mengi ambao kwamba sisi tunayaomba. Kwa hivyo kwa mkazo zaidi, hii ninayo yasema nataka yawemo humo ndani.

Indigenous people to considered, hakuna mtu wa hapa Mombasa aweza kwenda Kikuyuni wacha kutaka kusimama, nomination hupati, hata ukisimama na chama cha DP ikiwa si Mkikuyu hupati.

Ya mwisho na omba Waswahili wafikiriwe, hakuna lugha lisilo kuwa na wenyewe. Mjerumani anazungumza Kijerumani ni Mjerumani, Mkamba akizungumza Kikamba atambiwa ni Mkamba, Mswahili anaambiwa hana kabila ni vipi? Asante.

**Com. Ayonga**: Asante, unaweza kutupa hayomaandishi na nataka nikuhakikishie, kwamba yote ulio sema yako hapa kwa hicho chombo, yote ulio sema yame kuwa recorded, kwa hivyo hakuna neno lako linapotea.

**Mwinyi**: Asante sana.

**Com. Ayonga**: Jana nilipata jina la Sole Adhumani, kuna lingine, we mzee siulimaliza nadhani jina lako limeandikwa mara mbili, ningetaka kuhakikisha kama kuna mtu ambaye anajina kama wewe,asante, Sheikh Ali Shee. Mzee useme jina lako vizuri.

**Sheikh Ali Shee**: Nisawa ulivyo taja, Salaam aleikum. Waheshimiwa, wanachama wa Commission yetu ya kurekebisha Katiba mimi Sheikh Ali Muhamed Shee, mimi ndiye Chairman wa baraza la ma Imamu na wahubiri nchi ni Kenya. Nina mengi ambao tumeandika sisi kama ma Imamu ambao tumependekeza kwenye tume hii mambo haya yaje yaingizwe kwenye mapendekezo ya kurekebisha Katiba ya nchi yetu. Kuna mambo karibu mambo kumi na moja lakini yote tumeandika, lakini nitaja kwa ufupi kila jambo katika mambo haya ambao tulioyaandika katika memorandum yetu. Kitu cha kwanza ni utaratibu wa utatawala, tumependekeza utaratibu wa utawala uwe ni utaratibu wa ki Majimbo. Huu ndio utaratibu ambao wananchi wa Kenya wote walopigania wakati wa kupigania uhuru, na ndio Katiba ambao iliotumika wakati wa uhuru wa nchi hii. Ingawa kulipita mabavu na manguvu ambao yalotumika kuondoa katiba hii.

Na tumeona Katiba hii ya Majimbo namna ilivyo leta uhusiano mwema katika ulimwengu mzima hivi sasa tunavyo endelea. Katika utawala wa Kimajimbo tuliopendelea kila Jimbo liwe na mkubwa wake yaani Governor au Makamu wa Rais ambaye atachaguliwa na Raia. Jimbo ambalo lina Waislamu wengi basi Rais awe Muslim na yale Majimbo ambao wa Kristo ni wengi

basi Majimbo yale yawe Rais wake ni Mkristo. Vile vile tumependekeza kua wakuu wa wilaya wawe ni watu ambao walochaguliwa na Raia, kama vile mkubwa wa Jimbo anachaguliwa na Raia moja kwa moja, na wakuu wa wilaya vile vile wachaguliwe na raia. Na tumependekeza kua wakuu hawa wawe ni wanati wa lile Jimbo, ikiwa ni Jimbo la Pwani, mkuu wa Jimbo la Pwani awe Manati wa Pwani, na wakuu wa wilaya vile vile wawe, ni Wanati wa Pwani yaani indigenous people sio watu wakutoka nje, makabila ambao yajulikani haya si makabila ya Pwani au si makabila ya Nyanza, Mtu wa Pwani akienda Nyanza asiwe na haki ya kua Governor katika Nyanza. Na mtu wa Nyanza asiwe na haki kuwa Governor katika Jimbo la Pwani au Jimbo linginelo. Yaani indigenous people watu Wanati wawe ndio wenyewe wa kushika madaraka katika ile Jimbo, na mengine mengi kama hayo ambayo tumeeleza kwa wenye utawala wa kimajimbo, kazi zote zishikiliwe na wenyewe wale ambao ni wanati wa Jimbo lile. Si lazima iwe ni Pwani tu yaani kila Jimbo kama ilivyo sasa kila Jimbo ukienda hivi sasa utawaona kila wilaya walio shikilia madaraka ni wanati wa ile wilaya; ukienda Machakos, ukienda Nyanza, ukienda wapi, hivi sasa Majimbo inaendelea katika area hizi isipokua Jimbo letu la Pwani. Swala la pili.

**Com. Ayonga**: Asante sana. Next ni Ali Taabu.

**Ali Taabu**: Hamjambo ndugu zangu, Commissioners na wananchi wenzangu. Kwanza jina langu mimi naitwa Ali Taabu, mimi nimzaliwa wa hapa Kenya halisi, na hichi kiwanjwa ambacho tumekaa tunazungumzia ni kiwanja ndichonime somea mimi hapa. Kwa hivyo, kuanzia ukoloni niliona serikali yake, na sasa kuanzia serikali yetu ya Kiafrika pia niliona. Kwa hivyo uchungu wa kwote kwote ninau ningependa kuzungumza juu ya Rais. Ningependa kuzungumza juu ya wa kazi wa Mombasa. Wa kazi wa Mombasa wamekaa kwa muda wa miaka mingi sana sana, wakiwa kama ma-squater. Kuanzia babu, zetu hadi baba zetu, mpaka sisi mpaka watoto wetu. Ningeomba hilitatizo liondolewe na serikali yenyewe tukufu, isigonjee damu kumwagika. Ikimwagika damu hua ni mamlaka yale yako mikononi mwao na tumetumana maombi yetu mara nyingi sana, lakini tumeona hatuskizwi. Jambo kama hili liwepo sheria haswa hakuna squatter hapa Coast Province. Especially Mombasa hapa sasa imepawa ni jiji hatutaki kuona mambo kama haya yanaturudia mara kwa mara tunahangaishwa na wenye viwanja. Tumeteseka sana.

La pili; elimu iwe bure, kulingana sisi tulikua twasoma, elimu ilikua shilingi ishirini kwa mwaka. Mpaka dakika hii imekua elimu ya watoto wetu ni maelfu, kazi sisi tume retire kabla ya miaka yetu. Watoto watasoma kivipi? Ikiwa kazi wazazi wame retire; kina mama wamekua na mzigo mkubwa sana. Kwa hivyo uchungu huu uko mara mbili, kwa wazazi wa kiume na wazazi wa kike. Hasa kina mama sasa mzigo ule ulikua ukilemea baba, umelemea mama. Mama achome mahamri, achome viazi, akauze alishe nyumba, alishe watoto, alipe school fees, anunue vitabu, anunue uniform. Hili ni jambo la kushangaza kabisa serikali inaona inajifanya aioni. Kwa hivyo tungependelea uzito kama huu uondolewe kabisa Kenya ikiwa aitakua na watu wenye elimu, basi itakua madhambi yale yote yatahukumiwa juu ya serikali, si juu ya raia. Na jambo lingine ni maji, maji ni natural resource. Ninaona ajabu nyingine za majirani hapa, kama Tanzania, wanatumia maji bure. Kenya mpaka leo tunanunua maji na tunalipa gharama nyingi sana. Ikiwa imebidi sana ingekua hayo maji iwe flat rated kwa shilingi mia mbili kila mwenzi kwa sababu ya kununu madawa, lakini isiwe imepewa mtu binafsi anavuna kwa watu ambao ni wananchi wa Kenya, hili ni jambo kwamba la

kusikitisha sana.

Na la tatu ni taa, umeme uwe ni juu ya serikali kusambaza kila mtaa. Isiwe ni raia; hawezi kuuchukua ule mzigo, kuchukua umeme afute mpaka nyumbani kwake; gogo moja utasikia karibu shilingi elfu arubaini. Mtu yule ana watoto anasomesha. Kwa hivyo umeme yale maguzo yasambazwe na wizara ya nguvu za umeme. Iko pale for nothing haifanyi kazi yake. Kwa hivyo kazi yake iwe ni hiyo. Watoto walemavu, watu wengi wamezungumza hapa lakini wamesahau wale watoto tunao wazaa wengine ni walemavu. Ikiwa mimi sikuzaa, mwenzangu amezaa, watoto walemavu lazima waangaliwe vizuri zaidi kuliko wale wazima wenye afya yao. Yale ni maumbile ya Mwenyezi Mungu hakupenda hata yeye pia kuwa mlemavu angependa kua mzima kama sisi. Kwa hivyo watoto kama wale wapatiwe huduma za kwanza. Wale watoto. Wajengewe nyumba za bure kabisa ziwe ni mali yao wakae na wao wapangishe kama wale wengine.

Na kadhalika, mtu akitimia miaka kumi na minane, umri wa kuchukulia kitambulisho, ingefaa apewe kitambulisho ikiwa yeye anakidhibitisho kamili kwamba ni mzaliwa wa hapa Kenya apatiwe kitambulisho chake, apatiwe card yake ya kura, apatiwe passport yake, vitu vitatu kwa mara moja. Kwa sababu ameshaonyesha kwamba yeye ni mzaliwa wa hapa haina haja tena akimbizane tena mara ikingine atafute kitambulisho cha kura, atafute kitambulisho cha kusafiri, hii naona nikama kusumbua raia na hili hali vitu vile vyote vinatoka mikononi mwa serikali. Kwa hivyo vitu hivyo vitatu akitimia miaka kumi na minane apawe kwa pamoja pap!, amalizane na hizo shida.

Na kama wavuvi, wavuvi wa hapa pwani wameanza mababu na mababu, mimi baba mkubwa aliyezaa nyanyangu na babangu walikua ni watu wa kuvua. Zamani nyumbani walikua wanakuja samaki hata sisi hatuwajui samaki majina yao. Mpaka tunakula wanatuchafua roho. Siku hizi babu hawezi kwenda kuvua wala baba, hawezi kwenda kuvua kila mahali pamewekewa mpaka ukija huko wambiwa wewe hapo hapo, usivuke upande huu. Sasa mzazi kama yule kazi hana, ikiwa ameenda baharini kujipatia risiki pia anazuiwa, aelekee wapi? Na hiyo ni natural resouce ya mtu wa Pwani hata mtu wa Bara pia Lake Victoria pia kule mimi nimefika. Akififikiria nimezaliwa hapa, kule Bara pia nimepelekwa kwa minajili ya kikazi nimefanya huko kwote.

Kadhi Mkuu ni mkuu wa Makadhi, ni Administator na ni mkuu ya sheria ya Kislamu katika mahakama. Hayo mengine yote yaliyo tajwa, that is High Court, Kadhi’s Court of Appeal, yote tumeyataja sisi katika memorandum yetu, nafikiri tunakubaliana na wale ambao waliozungumza, Chifu Kadhi awe na heshima kama vile wenzetu walivyo zungumza mbeleni hatuna haja ya kuregelea. Jambo lingine nila Kadhi kuweko sheria maalum, kama tunavyojua hivi sasa hakuna sheria iliyopitishwa na bunge, kwamba hii ni sheria ambao lazima kadhi aitumie wakati wa kutoa wamzi wake kwenye mahakama. Iwekwe sheria maalum kama kama zile nchi zingine za Kislamu. Kuna ile Islamic family Law, ambayo imekua enacted by the bunge through recommendation of Muslim organizations. Kwa sababu mara nyingi utaona Kadhi wa Mombasa hukumu tofauti pengine afuate sector hii, na Kadhi mwingine wa Wajir au Kadhi wa Nairobi aweza akawa na tofauti katika swala lile lile moja kwa sababu kuna Rai karibu ine au tatu ndio swala lile kutokea kwa wanavyoni. Jambo la tano katika hayo tulo pendekeza ni uhuru wa dini, uhuru wa dini kama ilivyozungumzwa hapa kuna ubaguzi. Mimi nazungumza wazi wazi kua Kenya tuna ubaguzi wa aina mbili.

Tuna ubaguzi wa kikabila, tuna ubaguzi wa kidini, vitu vyote viwili hivi viko. Na ni lazima viondolewe. Moja ni kile ambacho kimetajwa na wenzetu ukaenda wewe wataka kitabulisho wewe na ndugu yako John, baba mmoja, mama mmoja wewe John huna mambo mengi utapata kitabulisho haraka, lakini Abdala ndugu yako baba mmoja mama mmoja, Abdala atapata taabu. Huu ni ubaguzi wa dini, mtu yeyote anaweza niabia mimi niubaguzi gani? Ikiwa siubaguzi wa kidini ni nini? Passport mambo ni kama hayo. Kazi vile vile, katika university vile vile, utaona namna gani ubaguzi ulioko katika admission katika kuchuguliwa wanafunzi wa Kislamu jina likionekana ni Abdala na Mariam utaona namna linavyo fanyiwa ubaguzi. Ubaguzi huo wa kidini uondoke uweko na uhuru wa kidini wa kisawa sawa ule ambao tunakusudia.

Nafikiri jambo lingine ambalo nakimbilia haraka naona Bwana Chairman, ananiangalia, naona unipe nafasi kidogo tu, ni malize na namaliza. Vile vile kuweko na uangalifu juu ya mambo ya wakuf ambao imezungumza, wakfu commissioner, sheria zake zimewekwa 1951, alioweka ni mkoloni, utaona namna zilivyo na ubaguzi ndani yake, kuwa hayo ni mali wa Waislamu si mali ya mtu mwingine wala si mali ya serikali, wala si mali ya uma, wote wakenya, mbali mali ya wenyewe Waislamu walo weka ili yanufaisha Waislamu au miradi ya Kislamu. Mali haya haki ilivyo ikiwa la haki yataka ichungwe yasimamiwe na wenyewe Waislamu. Sio kusimamiwa kama sheria ilivyo sasa. Kua Waziri ndio amemuweka Commissioner wa wakfu kulingana na recommendation za Provincial Commissioner na aweza kuondolewa kulingana na recommendation za Commissioner wa yaani PC. Hii utaona ni kuingilia katika ile sehemu kwenye uhuru wa dini ya Waislamu na njia za unyanyasaji ambao unaendelea.

Swala la mapendekezo mengine; swala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni umilikaji wa ardhi. Nawaunga mkono wenzangu walo zungumza, na mimi nikiongeza ni kwa swala la kuweko ma-squatter katika nchi yetu. Ni swala la usalilifu, swala duni, ni swala ovu ni, marginaliazation in our people in this country. Mambo ya ardhi lazima ya zungumzwe kwa uwazi, wananchi wa miliki ardhi yao, na habari ya ma-squartter ikome na iondoke. Serikali isitoe ardhi kuwa ni zawadi upeana kwa wale ambao wenye kuunga mkono pande fulani. Kwa hivyo Commissioner ningependa ipendekeze katika Katiba kua mali ya ardhi, yawe ni mali ya uma, na wale ambao hivi sasa wamekua ma-squartter wakilipa miaka na miaka mali kama yale wamilikishwa.

Jambo lingine, ni la mwisho nafikiri, au kabla la mwisho ni mambo ya haki za wanawake. Haki za wanawake, naona wanawake wengi hapa labda ni ile walivosema sister wngu kuona haya. Kuna mila nyingi ambao mpaka sasa inaendelea kumnyanyasa mwanamke. Mila kama hizi lazima ziangaliwe kama umilikaji, ingawa katika sheria ya Kislamu mwanamke kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, hana matatizo ya umilikaji mwanamke anamiliki kama anavyomiliki mume na ana ridhi kama anavyo ridhi mume, hakuna matatizo katika swala hili. Lakini swala la wanawake kuadhibiwa kupigwa, swala la wanawake kwa lazima wachukue majina ya waume zao hayo maswala ambao yana discredit the diginity of women. Vile vile ubaguzi ambao alozungumza sister kuhusu mume aliyemuoa mwanamke wa Kenya hapati uraia haraka haraka kama anavyo pata mwanamke au mume aliomuoa mwanamke wa kigeni. Hili ni swala ambalo laonyesha ubaguzi wa gender, lazima lizungumzwe na mlielewe na mliweke kwenya Katiba. Ubaguzi wa aina hii uondolewe.

Vile vile swala la wanawake kupewa nafasi ya ubunge, nafasi za utawala ni swala ambalo ni nzuri. Lakini sio wapewe bure tu, wanawake nawao wajionyeshe ile ability yao na uwezo wao wakuweza kusimama na kupigania haki na wasingojee kupewa, waonyesha ule uwezo wao wasimame imara. Nafikiri hayo Bwana Chairman, mambo ya watoto nafikiri mtakwenda kuyasoma mengine ambao tunaonyesha kua watoto lazima wapewe nidhamu swala kuwa mtoto akipigwa au asipigwe, asipewe nidhamu ni swala ambalo mtalitizama kwa njia mzuri. Nafikiri Bwana Chairman nakuona ushakosa subira ya kunisikiza tena nikomee hapo. Niwe tayari ikiwa kuna swala ni kujibu.

**Com. Ayonga**: Asante sana tumeshukuru sana kwa yale yote ambayoumeyasema mambo mengi ambayo ni makubwa makubwa, ila ningependa tu kukuliza, sehemu zingine umesema ambazo sikukuelewa vizuri ambazo nataka utwambie; kwa mfano, nimesikia kama nimesikia vizuri kwamba una recommend president awe ana rotate from one point to another. Lakini shida yangu ikawa wakati uliposema baada ya miaka mitano. Ndivyo ulivyo sema.?

**Ali:** Nam, baada ya miaka mitano.

**Com. Ayonga**: Hii inamaanisha kwamba katika Katiba tuwe na President yaani, term of government ya Kenyan President, ni miaka mitano.

**Ali:** Ikiwa hata miaka kumi hakuna tabu.

**Com. Ayonga**: Sasa ikiwa kumi si wale wanangoja sana.

**Ali:** Yaonyesha hivyo. Ikiwa itapendekezwa iwe miaka mitano, lakini ikiwa ni kabila moja peke yake tukarudi kwa ule ukoloni wa kingereza, iwe ni kabila moja inakua Rais au Jimbo moja peke yake.

**Com. Ayonga**: Asante

**Com. Wambua**: Tafadhalini tusikilizane, hatusikii vile watu wanasema, kuna kelele nyingi sana, Sheikh nilikua nataka kuuliza juu ya Wakfu Commissioner, huku ulisema, nataka wale ambao watakua Commissioners wawe ni Waislamu, lakini hukutaja jinsi au taratibu itakayofuatwa kuhakikisha wale ni Waislamu. Watakua appointed au elected?

**Ali:** Appointed

**Com. Wambua**: By who?

**Ali**: By the people themselves, the Muslim community.

**Com. Salome**: Asante sana, nitakuuliza swali moja kwako, kwa niaba ya watu wale wamezungumza mbele yako, (inaudible).

**Ali:** Asante, tunavyo sema sisi ni kua, ki sheria na kimaumbile, ni kwa mwanamke anayo uwezo wa kuongoza kazi zote. Isipokua in unyanyasaji wa waume mara nyingi inawafanya wanawake wasiweze kuongoza. Psychologically, wanawake wamekua traumatized; yaani psychologically, ilikua wanawake kuambiwa wewe huwezi, basi imekua siwezi siwezi. Lakini wanawake wanauwezo wa kuongoza na historia yatuonyesha namna gani wanawake kadha ambao walikua wakiongoza. Hakika mimi na wenzetu twasema kua wanawake wenyewe waonyeshe uwezo wa kuongoza, isiwe wanangojea embe literemke wende wakachukue. Wao wenyewe waonyeshe kwamba wao wenyewe waweza kuongoza na wajitokeze watu wawatambue kwamba huyu anaweza kutuongoza. Wampe kura zao, wamchague kwa sababu ya uwezo wake. Ama kupelekwa tu ni show anakwenda na marangi na manini peke yake, ile show mwanamke aweko tu, lazima mwanamke aweza kweli kuongoza. Akia anaweza kuongoza mwanamke afaa awe kiongozi.

Jambo lingine, swala la ubaguzi, ni swala ambalo ni maradhi tuko nayo bara letu la Africa. Ubaguzi wa kikabila, ubaguzi wa kidini, ingawa dini si sana, ukabila ni zaidi kuliko dini katika bara letu la Africa. Lakini liko swala hili na limejitokeza kwa uwazi katika nchi yetu ya Kenya. Ubaguzi wa kidini tuko nao, mimi nitakupa mfano, wakati wa utawala miaka kumi na mitano wa Kenya kua huru, hakuna hata Muslim moja kuwa Waziri au PC, mimi nikimuuliza mtu yeyote nanimuulize PC mmoja, sita mtaja jina, nikamwambia ikiwa huu si ubaguzi wa dini ni ubaguzi wa nini? Kwa nini tusiwekwe Waziri wakati wa Jomo Kenyatta, ambaye jina lake ni Muslim. Kwa nini tusiwekwe? Kwa nini tusiwekwe PC, ikiwa si ubaguzi wa dini ni ubaguzi wa nini? Bila shaka akakosa la kujibu. Kwa hivyo ubaguzi wa kidini tuko nao na nyinyi mkienda mkiandika recommendation zenu muonyeshe kua Waislamu wana lia katika hii nchi kwa wao wanabaguliwa kwenye nchi yao, ambao wametoa mchango zaidi kuliko watu wengine katika nchi hii. Ubaguzi kama huu Bwana Chairman, mtakwenda kwenye record kwenye historia ya Kenya mkiwa hamkutaja wala hamkupendekeza kuondolewa ubaguzi kama huu ambao mimi nikikuuliza maswala kama hayo pia na wewe unataniambia sina jawabu la kukujibu ikawa kwa,nini kipindi miaka kumi na tano bila Waziri, huu ni ubaguzi ambao ni wa kidini.

Kwa hivyo maswala ya ubaguzi wa kidini, na ubaguzi wa gender vile vile, wanawake, ni maswala ambao tuko nao, ubaguzi wa wanawake na waume wote ulimwenguni. Waume wote, hata uzunguni pia, usidangaywe na wazungu. Wazungu pia wanabagua wanawake, tena waovu zaidi, wanamtumia mwanamke kwa malengo yao. Ubaguzi huu lazima upigwe vita kwa sababu unamwadhiri mwanamke na inadhiri maendeleo ya nchi. Kwa hivyo sisi Kislamu, katika maongozi ya Kislamu haitaki mtu abaguliwe na ubaguzi ni haramu ni kosa kumbagua mtu kwa sababu ya dini yake. Mambo hayo Bwana chairman lazima yarekebishwe.

**Com. Ayonga**: Huyo alikua Sheikh Ali Shee, na ametoa maoni ya wa mama; lakini mkumbuke kwamba lazima mfanye bidii nyinyi wenyewe. Hamtangojea embe lianguke mwekewe mkononi. Hebu niwakumbushe, wamama wako katika nchi asilimia

sitini na mbili, nyinyi ni wengi kuliko wanaume. Kwa hivyo mfanye kazi yenu. Asante sana Sheikh kwa mambo ambayo umetupa na hicho kitabu utatwachia. Now najua itakapo fika saa sita unusu, itakua wakati wa kwenda kuswali, lakini kabla sijatangaza saa hiyo, ningalipenda kuona kama kuna mlemavu yeyote hapa ambaye angalipenda kutoa maoni, mtu mwenye ulemavu wa njia yeyote ambaye alifika hapa leo asubuhi, at least tumepata wamama wametoa maoni lakini sija ona mtu mwenye ulemavu hapa ambaye ametoa maoni. Kuna yeyote? Basi, kuna mkono kule nyuma, what do you want to say? Wewe kuja mbele hatusikii hapa. Hebu tumsikize huyo.

**Interjection**: (Inaudible)

**Com. Ayonga**: Endelea, Tafadhali tuwe kimia.

**Bani Shirao**: Asante sana mwenye kiti mimi ni mkaaji wa Tononoka naitwa Bani Shirao. Hamjambo wananchi? Yangu ningependa kutoa mapendekezo kidogo, moja ni juu ya hiyo Katiba. Hii Katiba tunayo hapa Kenya si mbaya. Mengine yako sawa lakini mengine yanaweza kubadilishwa ama tuongezee mengine. Lakini lazima tutoe shukurani na asante kwa walio andika hii Katiba. Walipoiandika waliandika kwa dhati wakiwa na upendo wa nchi yao. Wakiwa wazalendo. Sasa lazima tuwapatie heshima na yote walio andika hawakuandika mabaya. Mengine mabaya ni sisi wenyewe ambao tumeyaharibu. Sasa, cha kwanza walipokua wakiandika hii Katiba na wakipigania walikua wanapigania kuondoa ujinga, umaskini, na ardhi na chakula. Sasa, upande wa ujinga tulikua tunatakikana tuwe na education ambao wakati huo ilikua sawa.

Upande wa umaskini pia walijaribu. Hatukuwako wakati huo watu wengi wakinyakua maplot na kila kitu. Upande wa ardhi pia mashamba makubwa mengi yalikua ni ya wazungu. Ambako tulikua tunaona tumenyanyaswa tunapokonywa nchi zetu ambazo zilikua na rutuba tukinyimwa sasa tunakua maskini tunaomba chakula maanake hatuwezi kuwa na security ya chakula nchi yetu. Maanake nchi yetu sisi tumewai kula hii sima ya yellow, na Uganda wamekua na vita na shida nyingi na hakuna hata siku mmoja wapewa chakula cha relief.

Sasa upande wa education, tuna maskuli mengi ya serikali yamekufa, watu wengi wanafungua private schools, walimu wakiwa ni wazuri, wanapewa transfer kwenda kwa skuli zile ambazo zinafurahisha wale watu ambao wanaendelea vizuri, yaani kuna ubaguzi. Wale walimu wazuri wanapelekwa kwa skuli ambazo watu wenye kujiweza, watoto wao wanasoma huko. Example nzuri ni Mvita hapa, Mvita ilikua skuli kubwa ya wafrika. Sasa tumeiua, ground yote imekua grabbed.

Halafu upande wa hiyo maplot kugrabiwa, wame-grab mpaka kwa milango ya watu, watu wanajenga manyumba, tunasumbuliwa na uchafu, sewage. Tunapata malaria mengi ambayo yanaua watu, hakuna drainage tunaruka mavi tukitaka kupita. Malaria imezidi. Halafu watoto hawana pahali pa kucheza, imebaki kuwa sasa watoto wanakaa vikundi vikundi wakila madawa halafu tunapata shida, watoto wameharibika tunaenda kuleta dunia hii sasa generation ambayo itakua ni mbaya kabisa. Na hii pia ni kwa sababu ya pia sisi watu wazima, tumekosa nafasi kukaa na watoto wetu. Tuko mbioni twafuta pesa hatuna

time kuwa na urafiki na watoto. Tukirudi nyumbani ni kuchelewa usiku, hatuna time ya kuzungumza na watoto, hatujui tabia za watoto wetu, hatujui marafiki watoto wanacheza nao ni aina gani?. Halafu kitu kingine pia, hiyo mambo ya madawa wenye kuuza wanantakikana wakipatikaniwa wafungwe tuna example nzuri hapa Mombasa hii kesi ambayo inaendelea. Wanawekwa ndani wanaachiliwa, wanaharibu watoto wetu.

Upande wa ma-councillor, ningalipenda ma-councillor wakichukuliwa wawe wana kiwango cha O-level yaani form four wamepita vizuri sio watu wamefika Form Four na una E, ututawale na hiyo hatutaki. Halafu ile watu wakishachaguliwa huko kuwa Councillor ukionekana hauwezi ku perform kabla ya miaka mitano kuwe na term ipunguzwe iweze kuvunjwa, election ifanywe tuchague mtu mwingine. Kama you cannot perform and the same should apply to parliamentarians. Kama huwezi kufanya kazi unaenda bunge kulala hatukutaki maanake tunakutuma huko kutuwakilisha, si kwenda kula hiyo nusu milioni, hawapiganii haki za wananchi badala wanapigania haki zao wenyewe. Hawajali mishahara ya watu kwa hivyo sisi tunapata taabu, watoto hatuwezi kufundisha tunajaa na mtu mwenye njaa hasikii, itabidi utakwenda huko na pesa zako na itabidi uibiwe. Utakua huwezi kulala maanake unawasiwasi unaweka ma-body guard wengi. Wale ma-body guard mtakua nao mtakua mnatumikia pesa ya raia kuwalipa mshahara. Halafu upande wa hizi pesa za uma, watu kula wanatakikana wafungwe, si wachukuliwe wapelekwe parastatal nyinigine. Apelekwe kotini ahukumiwe ili haki ipate kufanyika.

Halafu kitu kingine pia watoto wetu ambao tunazaa tuwafundishe nidhamu, kuanzia nyumbani, wakienda masukulini, makanisani, misikitini kwa sababu saa hii katika hiyo Katiba tuliyopigania tuna uhuru wa kuabudu, hawakuchagua Muslim wala Mkristo. Muslim ana wake, Mkristo ana wake, hakuna mtu wakumsubua, kama tuna uhuru wa kuabudu, sio haki mtu alalamike. Lakini upande wa education pia tumeumizwa kabisa, maanake kuna skuli zingine nzuri ambazo haziko hapa Coast, zote zimeelekea upande wa Bara.

Halafu haki za wajane. Wajane saa ingine Bwana akisha kufa upande wa pesa zake na mali ambao aliyo nayo pamoja na watoto wakike. Kama hukuzaa mtoto wa kiume saa ingine unafika kiwango mpaka unafukuzwa kutoka kwa hivyo bomo ndugu zake Bwana wanachukua hiyo mashamba unabakia haunawezo chochote cha kufanya.

Halafu upande wa hizi slums. Watu wamenyakua mashamba makubwa makubwa ambayo hayawafai na haki ya mungu aliyekuwekea haki yako ya shamba kabisa utazikwa na 3,000ha. ya shamba, unazikwa 4 x 6 ile yako ya haki mungu amekuwekea. Maanake utakua na shamba kubwa hauitumikii na watu huku wanapata shida wewe umejiekea maeka mengi hata huilimi imebakia kavu maanake kama utachukua hilo mashamba kubwa ulime tungekua na njaa Kenya hii? Kama tungekuwako tunalima tungekua na chakula hapa Kenya saa hizi. Halafu hiyo umaskini pia tuna magonjwa mengi saa hizi, twalipa ushuru, madawa hakuna mahosipitalini. Madaktari walio soma na ma-nurse wote watoroka nje, maanake pia hawana haki zao wananyimwa inabidi watoroke waende zao nje kufanya kazi. Tunawasomesha wanaenda kujenga nchi za watu nje hapa twabaki tukiumia. Sasa hiyo pia lazima iangaliwe.

Viwete wangaliwe pia, wakati wa kupiga kura wawe na makaratasi yao special mwanzo kipofu, kuna ile kitu inaitwa Braille, waweze kupiga kura, kuliko hile mambo ya kwambiwa wasimame mbele ya watu agent, achague na alikua anataka kufanya siri. Kukiwa na hiyo Braille atajua kushika na amesoma huyo kiweta ataweza kujipigia kura yake mwenyewe. Sasa wawe na facilities zao na kule mahali wata kwenda kupigia kura pia wangaliwe ili wawe na haki zao za kwenda kupata haki zao na mtu ambaye anajiweza. Halafu upande wa ukulima pia, hao wenye mashamba pia, wananchi waweze kupewa begu zilizo sawa ili tuwe na nguvu ya chakula Kenya hii na pia begu za wanyama ili tuwe na vyakula vizuri, maanake siku hizi tumeua kabisa viwanda vyote vya wananchi ambavyo vinaitwa ma-co-operative tukileta vitu ambavyo vimetoka nje ambavyo ni hafifu, zetu za maana tunazitupa. Importation na kila kitu .

**Com. Ayonga:** Saa inakwisha.

**Bani:** Sawa.

**Com. Ayonga**: Hebu tuwe kimia ili mama amalizie.

**Bani:** Upande wa haki za watoto, hiyo haki ya watoto sawa, kuna point ambazo ziko sawa za kulea mtoto wako umsomeshe na umpe matibabu na kila kitu. Lakini kuna pande zingine ambazo azifurahishi mwananchi wa kawaida ni za mtu tajiri. Maanake kuna watu wengi hawana TV na kila kitu mtoto atajidai ni haki, yake hawezi kukusaidia nyumbani kufanya kazi anadai ana right zake. Hiyo hatutaki, mambo mengine kama hayo yanatakikana yangaliwe yaondolewe katika hizo section zao.

**Com. Ayonga**: Asante sana. Sasa nataka Bwana Fesan Said.

**Fesan Said**: Mimi kwa jina naitwa Fesan Said. Ni naibu mwenyekiti wa Araba Welfare Society, lakini hapa maneno ambayo nitazungumza ni maoni yangu mwenyewe si ya chama. (Arabic dialect) Pengine Bwana mwenyekiti ingawaje usomi wangu kuna Masheikh ambao wamenishinda itakua si kisawa sawa kuitafsiri haya hii kwa sababu hatuko kwenye kikao cha dini. Lakini, hiki kipande cha mwisho (Arabic Dialect) Muslim hafai kufanya uadui isipokua yule mtu anaye mdhulumu, naikiwa utaninyima haki zangu za kimsingi sidhani kama kuna dhuluma zaidi ya hiyo. Kwa hivyo tukinyimwa haki zetu za kimsingi hua tayari tushaanza kuleta ule uadui.

Mimi simsemaji mzuri pengine, lakini tumezungumza mengi ambayo sitayarudia na ni mambo ambayo yatukera sana sisi kwa jumla, ningependa kidogo kuzungumzia ule mwongozo alotoa Prof. Ghai, kwamba hii sheria amezungumza yeye ni kama (it is a water shape) ni kitu ya kugawanya maji na kwa hivyo sisi ule mchoro wa maji itakua ni shida sana kuigawanya. Halafu akatwambia hii ni hadhi, exortation, I do not know if it is the right meaning. Sasa hadhi hii tutailinda vipi sisi wa Kenya, kwa sababu ya kuuliza hivi ni kwamba wengi wetu twataka Majimbo, tumezungumza habari wa Waislamu kudharauliwa, ukitaka kitambulisho ulete kutabulisho cha nyanyako na hayo yote Bwana mwenyekiti katika sheria ya zamani si dhamani kama iko,

maanake sijui katika kifungu gani imeandikwa mtu akitaka kitambulisho aende akapeleke birth certificate ya nyanyake nyanyake. Hii pengine ni kuwa sheria yetu pengine kama alivyosema yeye, do we need a preamble? Yes we need this, and it should have a lot of barriers to say most probably, kwamba hii sheria ilivyo tungwa ni lazima watu waichukue kama sheria. Nikizungumza pengine habari ya Majimbo, ingawaje sina ujuzi huo lakini juzi tulikua tuna kikao na nilikua na ndugu Bwana Shallow amesema, kwamba Sessional Paper ya 1961, madha no. tisa kulikua ni tawala ya kila mtu apate tawala yake, na Nairobi iwe central. Sasa ilibadilishwa vipi? Ilikufa vipi? hiyo ni mambo ambayo pengine kwakua hakuna preamble kuifanya ile Katiba iwe na hadhii yake ndio mambo hayo yakafanyika.

Jambo ambalo pengine litanihusu zaidi ni kuhusu Chifu Kadhi na mambo yake, ingawaje pia nasema tena si msomi hivyo. Lakini mapendekezo yangu, ni kwamba Chifu Kadhi atakaye chaguliwa awe ni msomi wa dini sheria ya Kislamu, pengine ningefananua neno sheria, maanake mara nyingi tukizungumza sheria Waislamu watu kufikiria ni kukata mkono peke yake. La sivyo hivyo, sheria ni sheria itakavyo kua, sijui nitafsiri vipi, kwa hivyo atakae kutetea au kupigania au kuchaguliwa Chifu Kadhi, awe ni mtu ambaye amesoma sheria ya Kislamu sawasawa, pengine apate ile shaada ya mwisho kabisa. Na lugha ambaye itamfaa iwe ni hiyo sheria ya Kislamu na lugha ya Kiswahili. Secular education hiyo to me is irrelevant. Pengine tutasema he will be the administrator. Twaweza kumwandikia administrator akamfanyia kazi zake zile za ku-communicate na wale ambao pengine hawajui lugha atakayo izungumza yeye. Secular Education should not be a course or a reason to disqualify somebody from being a Chief Kadhi, that is my opinion.

Jambo la pili, tumeambiwa ya kwamba Islamic organizations, with due respect to to Supkem and other registered or elected offices, si dhani kwamba we have a system of doing it properly, hii itakua katika mambo ya kwamba Waislamu ile misaada inayokuja isiende kwa watu binafsi, kwa sababu Uislamu hautaki kugawanywa, aliko Muslim kokote msaada lazima umfikie. Nikishapata kazi, hii wakfu Kamisheni imezungumza sana, la kusikitisha ni kwamba chairman wa Wakfu Kamisheni ni PC, by the virtue of him being a PC he is the Chairman of that work. Hiyo si sawa sawa, kimimi naona si sawa sawa, awe Muslim, ambaye ajua zile sheria za ile wakfu, kwa sababu wakfu ni aina mbili, kuna wakfu ya mtu amejitolea haya mambo yaende kusaidia mambo ya Kislamu na kuna Wakfu nyingine ni ya mtu amekufa watoto wake ni wadogo zile pesa zitunzwe mpaka watoto wake wakubwa; sasa ikiwa wewe si Muslim hujui kwamba mwanamke ana haki yake ingawa je ni mmoja kwa mbili na mwanamme lakini iko haki yake. Sasa wewe PC waijua vipi haki hiyo imewekwa katika Koran? Utaamua vipi kesi kama hiyo ikija kwako? Kadhi uamzi wake uwe wa mwisho, ni aibu na niharamu Muslim (Arab dialect) nafikiri Waislamu twajua maanake nini. Haiwezekani wewe Muslim umekwenda kwa Kadhi waomba ardhi kwa portion yako ndogo ki haki wenda fanya appeal kwa Judge ambaye si Muslim. Ushatoka kwenye uislamu ndugu yangu.

Mwisho, ni mengi, lakini mimi nazungumza habari ya uraia. Sisi kitu gani kinatufanya tusijulikane kama raia. Kumepigwa mifano mingi sana hapa. Mfano pengine mdogo Bwana mwenyekiti ambao tungeutoa, na pengine ushasikika kwa watu ni kwamba kisa cha Kamau na Hamau. Hao ni watoto twambiwa wawili walisoma Lamu pamoja kutoka primary mpaka walipofika secondary. Kamau akaenda akachukua kitabulisho bila tabu, ilipofika wakati Hamau lahaula (Arabic dialect) Aliulizwa

nyanyake nyanyake nyanyako passport yake unayo. Kwa hayo machache Bwana mwenyekiti na shukuru na kama nimekosea mimi ni mwanadamu. Salaam aleikum (Arabic dialect).

**Com. Wambua**: Yale umetoa ni maoni hakuna kukosea umekosea. Tutamwita Salim Said Islam. Yuko?

**Salim Said Islam**: Salaam aleikum. Bwana mwenyekiti na ndugu zangu Waislamu na wasio Waislamu, ningeomba kamati hii kitu ya kwanza ibadilishe sheria ya mkuu wa sheria. Jina langu ni Salim Said Islam, Naomba kikao hiki, mtu akipelekwa mahakamani, mkuu wa sheria analeta barua ya kuweza kesi ile isikilizwe. Inamaanisha ya kua serikali imetoa amri ya mtu yule apigwe sack, na kuna kesi nyingi kama hizi, mimi mwenyewe ni moja ambaye kwamba nina kesi yangu Mkuu wa Sheria ameweka non-prosequi baada ya kupigwa search siku 36. Tarehe saba January 1997, kwa hivyo naomba mahakama hii.

**Com. Wambua**: Tafadhali tusikize yale anayosema mzee.

**Salim**: Mahakama ibadilishe kifungo hicho na pia ibadilishe kifungu cha Mkuu wa Sheria wasting of time. Mshtakiwa yeyote akishtakiwa, kwa nini ipelekwe kwa Attornery General kuulizwa kama kibali hiki kinatoka kwa mkuu wa sheria kimekubaliwa. It is a waste of time. Mtu anaugua ama anaumia na anaariki jela na Attornery General bado ana mafile tele. Kunawafugwa karibu miaka kumi wako jela na kesi zao bado mkuu wa sheria bado haja toa kibali. Naomba sheria ya jela ichunguzwe na kubadilishwa from A-Z. Wafungwa hawafai kuwa jela isipokua wafungwa wa sampuli mbili peke yake. Wakwanza awe ni rapist, wale wanaoshika wanawake kwa nguvu, na wafungwa wa kubaki jela ni wale watakao kua wameua. Hii itasalimisha serikali more than 10 million per month. Wafungwa waliobakia, kuwe na shamba la serikali litakalo zalisha mapato, shamba hili wafungwa wawe wakilala nyumbani kwao, asubuhi saa mbili baada ya kula kwao chakula, sio kulishwa na serikali, waende shambani. Mfungwa atakae kaidi sheria ya kuwa asubuhi saa moja, kamili aweko katika jela aende shamba akitoka shamba anarudishwa jela anapewa ruhusa ya kwenda zake nyumbani, akalale na bibi yake na watoto wake.

Nasikitika kuyambia Tume hii na ninafuraha pia kuijulisha serikali inatia maanani zaidi kahawa na majani ya chai ambako kwamba hivi ni vitu vyote vya sehemu za Bara. Sisi watu wa pwani tumewekwa katika map, kama ndugu yangu mwingine anasema samaki, mimi nataka kuipa Pwani jina la heshima ya hali ya juu. Pwani ni mahali Mwenyezi Mungu mwenye alikuweko mwanzo katika maji. Ni mahali pa roho ya Mwenyezi Mungu ili kua katika maji. Ina jina la heshima ya hali ya juu. Hivyo ndivyo Pwani kuna watu wana vipawa vya powerful positive thinking, na wanakua ignored by the government. Na wanauliwa, wanapigwa risasi. Naomba Tume hii ichunguze kwa makini, mtu akiwa na busara na akili ya hali ya juu Mwafrika anamua, sasa tuko katika karne mpya, badala ya mtu aliye na akili hali ya juu na mawazo ya hali ya juu badala ya kuuliwa, naiomba kamati hii iandike wachaguliwe wale watu wenye mabongo makali, wawe katika committee of advising council. Iweke serikali katika hali nzuri ya kiuchumi badala ya kuwaua. Naiomba Tume hii ijue kwamba Pwani tuna vitu vitatu, amba kwamba vinne lau serikali hii ingetilia mkazo katika mimea yote ilioko katika Kenya, Pwani inge-lead katika upande wa mimea. Pwani inaudongo ambao kwamba lau tutapanda tufaha tunazalisha ambaye kwamba dhamani yake nikubwa kuliko kahawa. Pwani tunaudongo ambao

kwamba lau tutapanda zabibu inamimea ambaye kwamba inapesa kushinda kahawa. Pwani tuna udongo ambao kwamba inakorosho ambao kwamba korosho yenyewe ile yake nimafuta ambayo kwamba ni dawa. Tunda lake ni fruits na korosho yenyewe iliomo dani ni fruit tatu kwa kitu kimoja, ambao kwamba nilienda ua Rabuni safari mmoja nikawa challenged kwamba Mwafrika atumia akili, lau Mwafrika hatumii akil, korosho inazalisha rasimali kushinda petroli. Lakini leo mitambo yote ilioko katika Bara iko wazi, na mitambo yote ilioko katika Pwani imefungwa.

Naomba kamati hii ichunguze kwa makini vita za kienyeji zinavyo endelea sasa hivi katika Tana River. Vita hivi, vinavyoendelea katika Tana River baina ya Pokomo na Oroma inasababishwa na Serikali. Serikali inasababisha vita hivi kwa sababu serikali ya lack Advisory Council. Minister leo ambaye kwamba ni advisor to the President ndiye Minister yeye ni conductor, Minister yeye, ni passanger, Minister yeye, ni inspector, Minister yeye, ni bus, na Minister ni manamba, sasa hiyo inatakikana Minister awe na Committee Advisory Council ndio inaweza serikali yetu tukufu ya Kenya kuwekwa nyota tatu katika ramani ya Kenya na nyota hizo tatu ziwekwe coast. Lakini leo utaona Coast sisi tumefika hadi tunasema wazi na tunarekodiwa come what may. Coast sisi tumefika wakati ya kua hatuna imani na serikali. tumekaa kama kwamba sisi watu wa Coast hatuko Kenya. Tunajihisi sisi wat wa Coast kama kwamba hatuko Kenya, basi kama hatuko Kenya tutengenezewe Pwani yetu. Wangalie tutatawali vipi?

Natoa maoni kuhusu vita vya kienyeji vilioko dani ya Tana River. Vita hivi vinasikitisha sana na vinachekesha, kwa serikali ambaye kwamba ina watu wakubwa wakubwa wenye mabongo makali, lakini yasikitisha wanakaa watoto wadogo wadogo wachanga ambao kwamba tayari wameshawekwa tayari, na mzee mwenyewe anaona yeye bado ni mdogo lakini ashazeeka na bado anataka kukalia kiti. Ikiwa ni kuchaguliwa watu wote na yule mzee aliezeeka zamani sana atoke. Rais atoke katika kiti cha kusimamia sehemu zote. Namna ya kuzitatua shida Tana River, ni wa Pokomo wamebahatika kupata eneo la Tana River, wamepata bahati wao ni watu wa kwanza katika historia wameshika sehemu za mto wa Tana River. Orma na Wasomali wamepata bahati mzuri ama mbaya kwa kupata sehemu za nyasi kwa sababu wao wana mifugo, ng'ombe na mbuzi. Sasa tatizo hili suluhisho lake ni ndogo sana, serikali inunue sehemu ya ardhi ya Wapokomo na iwache barabara ya ng'ombe kwenda kupita kwenda kunywa maji vita zimekoma vya 1919 ambazo zitaendelea ama ikiwa haitafuata hivi navyosema. Serikali inunue ile ardhi ya Wapokomo, naitoe barabara ya wa Somali na wa Oroma kupita katika ardhi ile ya Pokomo serikali itakaponunua naiede wakanywe maji ng'ombe zao sivyo watakatwa mikia na wa Pokomo watauliwa kila siku.

Coast tunataka kazi, watoto wetu wamefika hadhi, tafadhali Bwana kamati sisi tumeamua, na kulingana na sheria ya Kislamu tunaweza kupata kuswali baada ya alasili katika hii. Nafasi hii Bwana kamati, Bwana Chairman nafasi hii itachukua miaka hamsini sisi zote tulioko hapa tutakua tumekufa. Tumeamua na wewe umeamua kukaa hapa usikilize maoni. Maanake nina maaoni kwamba nisipozungumza maoni kama haya mwingine hawezi kuja kusimama akazungumza kama vile mimi nilivyo na maoni kama haya. Pwani tuna watoto wanavuta bangi. Hawavuti bangi kwa sababu bangi ikopale yataka kuvutwa, hawavuti bangi kwa sababu wanaona raha kuvuta bangi, wanavuta bangi kwa sababu kazi zote zimechukuliwa na watu wa Bara. Kwa hivyo Bwana Chairman naomba kamati hii ipitishe mswada ya kwamba Coast, ni watu wa Coast na kilicho Coast kibakie

Coast, kwa sababu nicha watu wa Coast. Rasilimali ambayo kwamba ya serikali inayotoka Coast, ibakie Coast, watoto wetu ambao wamesoma, tuna watu wamesoma mpaka fourth form, tunawatu wamesoma mpaka University na wako nyumbani wamelala hawana kazi ni kwa sababu wanaitwa Salim na Bakari na Athumani. Angekua ni John na Sir James angekua yuko katika makao makuu.

Naomba kifungo cha sheria kinacho sema criminal afungwe bila yule mtu kupata haki yake, jamani hii ni uchali gani huu? Kisha uambiwe tena wewe, utoke nenda kamshtaki kwa Civil Rule, it is a waste of time and waste of money. Serikali imetuma mtu kwenda kushika kesi imepelekwa mtu kotini amehukumiwa kufungwa. Mtu yule aliyohukumiwa kufungwa, basi itoke hukumu ya kua afungwe na alipe deni hilo aliye sababisha kufungwa. Sio afungwe kisha yule mtu aliosababishwa kufungwa ambiwe nenda kamshitaki Civil Court ndio upati haki yako. Kudhibitisha Bwana Chairman, samahani namaliza sasa hivi, sisi Waislamu tunadharauriwa college mbili za Kislamu zilitaka kufunguliwa serikali ikakataa kufungua mpaka to ka threaten serikali, ndipo serikali ikatoa kibali. Ubaguzi zaidi ya hapo uko wapi? Na college yenyewe ingekuwa Mikindani, na moja ingekua Central, Bara. Sasa je, sisi watu wa Pwani tutapata university lini?

Naomba kulingamana na kiti cha Urais, naomba Tume hii ipitishe mswada wa kuhakikisha kwamba tutakua na wapiganiaji kiti cha Rais watatu peke yake ambaye kwamba moja atajiona ashakua wa mwisho mtihani ajiondowe ili kubakie watu wawili ambao kwamba watakwenda kwenye debe, na hapo ndipo 50% itapatikana na ndio 50% itakua equal ya kuweza kumwezesha yule mtu ameingia kwa 50%. Lakini tukiona wagombeaji Urais watano ama sita hiyo 50% haitapatikana yule ambaye kwamba aliyeshindwa na wote ndio anateguliwa anakua Rais. Kwa hivyo tunataka Katiba ibadilishwe tupate wagombeaji watatu peke yake.

Naomba vile vile upande wa watu wa Pwani. Kutoka DO, mpaka DC, mpaka Deputy PC, mpaka PPO, Permanent Secretary, jamani kuna mfanyi hata mmoja? Hakuna kwa hivyo tunataka serikali hii na serikali inayo kuja itilie maanani vyeo vyote hivi vinavyo pewa kabila nyingine na sisi watu wa Pwani tunavitaka.

Namalizia kusema kwamba, ikiwa watu wa Pwani wataendelea kunyanyaswa na sisi tumefika miaka hamsini na mbili tunaendelea basi hatuko tayari kugonjea watoto wetu wafanye lile watakalo fanya, tutalianzisha sisi, tutatafuta Pwani yetu na tunaiomba kwa njia ya amani, tupewe wenyewe Pwani yetu kwa sababu hii Pwani ni yetu na tuko wenyewe mkiwa mnatudharau.

**Com. Ayonga**: Mzee nataka uelewe, kwamba saa pia zinakwenda, hakuna ulete siasa hapa, wakati wa kuswali umefika na jinsi nilivyo ahidi kwamba ikifika saa sita unusu tutafunga, tutakwenda vile ilivyo. Na asante sana kwa maoni yako dhabiti. Na kabla ya kwenda kunamaandishi ambayo utatuachia?

**Salim**: Nitawachia:

**Com. Ayonga**: Asante kama unaweza kuweka saini, sasa ninaenda kufunga na hivi ndivyo tutafanya tukirundi, nataka wao wawe tayari tukianza saa nane na tunaanza na wao. Muhamed Abed, Wycliff Otieno, Hussein Nuru, Brian Mvita, Abudlrahman Ali, hao wawe tayari na Abubakar na Abdulrahman, kuna jina hapa ambalo limeandikwa vigumu nikilitamka vibaya mwenyewe atajua initial ni M, sijui Mviti au Mvisu.

**Interjection**: inaudible

**Com. Ayonga**: Basi yeye amesikia amejijua na iko Elijah Ali, Ramadhan Omar Ethiopia, Lukas Adams, Ali Taabu, Shabidi Omar, Abdillahi, tutafuata order hiyo kwa wakati ambao tutarudi hapa saa nane. Kwa hivyo sasa tuna break. Nataka kuwashukuru nyote jinsi mmetoa maoni na tumewasikiza.

**Com. Ayonga**: Niwangapi wako kwa wale niliosoma, okay, Omar Said, Omari yuko?

**Interjection:** Hajafika

**Com. Ayonga**: Hajafika? Wycliff Otieno, hebu kaa hapa.

**Wycliff Otieno**: My names are Wycliff Otieno, and I am here to present my views as an individual.

**Com. Ayonga**: Tafadhali wengine wote mnyamaze tumsikize Wycliff.

**Wycliff Otieno**: 1. Whenever Parliament is dissolved in any General Election the President should cease with immediate effect to perform functions of the Head of State and the Government. And in his place we should have the Speaker of National Assembly, the Electoral Commission Chairman, or the Chief of General Staff to perform functions of the President.

2. Whenever mass rigging of elections is detected like the one we realized in the year 1992, whereby the ruling party and the opposition rigged, then the public should be allowed to revolt to press the incoming government to have a neutral government. To that I would suggest a military government.
3. The freedom of worship should have some amendment done on it. Because we see so many have abused this issue, so I would suggest that the freedom of worship should have amendment done on it in such a way that we cut the mushrooming churches coming up today and there the issue of devil worshiping in our country today.
4. Then lastly any vote cast in any General Election, should be counted at the polling station; ballots should not be transported to the counting hall.
5. The gutter press should be allowed to operate in a free and fair atmosphere without intimidation or any harassment

from the government. Thank you.

**Com. Ayonga**: Asante Bwana Otieno. Unamaandishi yeyote? Asante nenda huko ujiandikishe. Hussein Nuru, Rajab Mvita, Abdrahman Ali.

**Com. Ayonga**: Shida kidogo tuliokua nayo, Nuru alikua ameongea jana na anataka aongee tena. Hiyo tunaona kwamba wacha wale hawaja sema waseme kwanza. Na kama ni maneno serious ndipo atasema. Maureen. Kuna anayeitwa Maureen. Thank you. Abubakar Abdi Rahman, Ramadhani Omari Ethiopia.

**Ramadhan Omar**: Kabla sijaanza mambo yangu, ningependa sana kutoa mapendekezo. Kijikaratasi tulichopata cha mikao yenu ya sehemu fulani hapa Mkoa wa Pwani naona bado haitoshelezi.. Kwa mfano, Kisauni Constituency, mmesema kua mtafika Mlaleo skuli peke yake. Je zile sehemu zingine itakua vipi, kama sehemu za Mwakirunge, sehemu za Bamburi?

**Com. Ayonga**: Ethiopia, umekuja hapa kutoa maoni, ndio wewe tupe maoni usituulize maswali, wewe toa maoni yako.

**Ramadhan Omar:** Sawa, Jambo langu la kwanza nilikua naguzia usalama wa nchi na nikuguzia usalama wa nchi nazugumzia nguvu za kidola, ambazo zinahusu jeshi, polisi, na askari ambao kwamba wanafaa kueka usalama na kulinda raia wao. Sasa unakuta kuna nguvu za Rais ambazo kwamba zinatumika katika maskari wetu, ikiwa kwa mfano: Watu wametoka mabarabarani kufanya maandamano wanataka kudai haki zao, pale kunatolewa order, wale watu wanatumiwa maskari wanakwenda wanapigwa, wanaumizwa, wengine wanashikwa wanafungwa na wakati wanatetea haki zao. Sasa ningependelea sana jambo kama hilo, linapotokea ni vizuri sana kungekua na kamati ya usalama, katika lile jeshi la dola kuangalia hao watu wanatetea haki zao kuvipi, badala ya kutolewa tu uamuzi kua watumiwe maskari na kupigwa bure. Ile haitafaa kabisa na si haki kulingana na haki za binadamu.

Kitu kingine, hizi nguvu za Rais zingepunguzwa, uwezo wa Rais ungepunguzwa kabisa, kwa sababu tunawatu ambao wadilifu, watu ambao kwamba wamesoma, wanaujuzi fulani, mtu anaweza kujitokeza na maarifa fulani, ukakuta kwa sababu yeye anajua zaidi pengine kuliko Rais, Rais anatumia zile nguvu zake na kumtumia yule mtu pengine maskari, CID, aende akasumbuliwe bure. Na pengine angekua ni mtu bora katika taifa letu la Kenya angetuletea mabadiliko pengine kiasiasa na pia kimaisha yetu kama Wanakenya.

Katika sehemu yangu ya pili inahusu mfumo wa serikali. Vile serikali inavyo takiwa kua katika muundo. Serikali ambayo tulioko nayo sasa, ni serikali ya kuzingatia umoja tu, nguvu zinakua katika dola mahali pamoja. Ningependekeza sana tuwe na serikali ya kugawanya hizo nguvu ili katika sehemu zingine nazo zipate kujitabulisha na pia kujulikana na pia kutumia pia nguvu za dola ili nazo zipate kustawi. Hivi sasa navyosema utakuta nguvu zilizokua zikitumiwa na serikali ambao iko katika madaraka hivi sasa, imefanya sehemu nyingi sana kua maskini na pia kutotambuliwa. Madhana ni kama vile North Eastern, ni sehemu

ambao kwamba imesahaulika na serikali sana. Lau tungekua na serikali kama za Majimbo ungekuta hata uchumi, raslimali ya taifa ingekua inatumika hata wale watu wanashida wakawa nao pia wanapata riziki yao pale pale. Kuliko kua inatumika katika serikali kuu peke yake.

Jambo langu la tatu ni kuhusu bunge, kawaida wabunge tunapowachagua hua tungependekeza kue na kisomo cha kiwango fulani, si mtu aingie katika bunge akiwa hajasoma, ameingia tu pale kwa sababu ya mapendeleo fulani, ama kwa sababu ya kabila fulani, ama tabaka fulani; inakua pale nikutupotezea wakati, na pia wananchi watapata shida sana. Tungepata wabunge wadilifu, wako sawa sawa kimasoma, wanajua matatizo ya wananchi, na akienda bungeni awe ni mbunge ambaye kwamba yuko active, very active si mtu amekwenda kulala bunge anakula mshahara wa wananchi ambao ni pesa nyingi sana ambao tunawalipa hao wabunge. Na kila wakati wanaongeza pesa zao. Sasa kwa hivyo mtu yeyote anayekwenda bunge, mimi napendekeza awe na degree ya university kulingana na kiwango cha mshahara wanao pata hivi sasa.

Kitu kingine bunge likiwa na kamati yake, natumai hivi sasa kuna committee ya bunge ambayo kwamba inaongozwa na Speaker, ambao kwamba inaweza kua na uwezo wa pengine Speaker, vile navyo jua anaweza akavunja bunge ama Rais. Mimi kulingana na kiwango cha kua Rais atavunja bunge sipendelei kabisa. Ni Committee ingekaa na Bwana Speaker wajue wakati gani watavunja bunge, na bunge wakati kabla halijavunjwa lazima wahakikishe kwanza masilahi muhimu ya kitaifa yametimizwa katika bunge kabla ya kulivunja. Natumai kile kipindi walicho maliza, walipomaliza kuvunja bunge kabla hawaja fungua bunge wakati huu; kulikua na miswada fulani fulani ambayo kwamba kwangu mimi kama raia wa kawaida ilikua ni muhimu sana. Wangekalia katika bunge wakaijadili hili tupate manufaa. Bunge lilipovunjwa tu, mimi mwenyewe nilibaki katika taabu zaidi, nikawa nasikitika sana, kwa sababu miswada fulani imesimamishwa na wakati pengine wangeitatua ingekuja ikatusaidia katika maisha yetu. Kwa sababu miswada ka maile ndio inaangalia masilahi yetu sisi kama Raia. Ikiwa wao ni wabunge wanakwenda pale kupoteza wakati na kua hawangalii mambo yetu, basi Raia ndiye atakaye umia na umaskini utazidi kuenea.

Upande mwingine sehemu hiyo hiyo ya bunge kuna hii mambo ya kuchagua mbunge maalum, nominated MP, mimi kulingana na jambo hilo halijanifurahisha kabisa. Ningependa sana kabla nominated MP hajachaguliwa, bunge likae chini, na vile vyama vingine vya kisiasa, wajadiliane nominated MP atachaguliwa wakati gani? Si wakati wa chama kikubwa kina watu wengi na bado chahitaji wabunge wengine maalum. Ile ni kujipatia manufaa ambao kwamba wakitaka kupisha jambo fulani ambalo linaumuhimu katika kuwasaidia wananchi wa Kenya, utakuta wale wenye majority katika bunge wananweza wakalikanyagia guu ikawa jambo lile halitatatuka wanaliblock; ambao sasa wananchi watakua katika matatizo makubwa. Sasa kwa hivyo kulingana na mimi naona kusiwe na wabunge maalum ama tu kwa dharura ikiwezekana.

**Com. Ayonga**: Umemaliza?

**Ramadhani**: Bado naendelea

**Com. Ayonga**: Tafadhali summarize.

**Ramadhani:** Sawa na upande mwingine wabunge, wanafaa kuafikia wananchi kwa njia za uraisi, ningependa sana katika constituency zao sehemu za grassroot kuwe na ofisi ambao wabunge watapata maoni tofauti tofauti, ama pengine mapendekezo ya Raia wao katika sehemu hizo ili wanapokwenda bunge, mbunge aelewe wananchi wake wanata kitu gani, ama wanataka vipi.

Tukija upande ya nguvu za dola, hapa nazungumzia juu ya nguvu za Rais, mimi napendelea sana nguvu za Rais zipunguzwe, kwa sababu, mfumo ulioko sasa ambapo kwamba, kwa kweli Rais anawezakua hana makosa ni ile katiba inamfanya yeye atumie yale madaraka yake vile anavyotaka. Sasa akiwa anatumia yale madaraka yake vile anavyotaka sasa wananchi wanaumia. Kwa sababu ikiwa rais atamka leo ameota ni jambo hili lifanywe, yeye analipitisha linakua kama sheria, sasa pale ndio hua sisi tunashangaa kwanini Rais akipitisha jambo liwe kama sheria? Watu wengi sana wanapata shida. Kwa mfano tuna mambo ambayo yanaendelea na nasema pengine naomba radhi kuyataja, lakini naona ni mambo ya kusikitisha katika taifa. Kuna mzozo baina ya walimu na serikali ambayo walimu wanataka haki yao, imependekezwa na serikali na imepitishwa kama sheria, iko katika gazeti la serikali kama sheria. Wabunge walijiongezea mishahara na pia Ma-PS, wakaongezewa mshahara; ya walimu imedinda kuongozea mshahara. Na kwanini walimu wote wamegundua sasa kua, mpaka Rais mwenyewe aseme wa patiwe pesa zao ndio zitoke. Sasa nguvu kama hizi tunaona watu wengine wanaumia wakimuongejea Rais hawe kama ndio hatakaye tamka ili wapate ruzuku zao za kawaida.

**Com. Ayonga**: Nataka utoe maoni, kwa maana yote yanajulikana, ungependa vitu vifanywe namna gani. Hayo ndio maoni.

**Ramadhani:** Sawa, kwa upande wangu, nguvu za Rais zipunguzwe ili matatizo ya watu wengine yapate kutatuka kirahisi. Na matatizo mengi sana yanahusiana na pengine mambo ya kitaifa. Majangwa ama matatizo mengine, kungekua na committee maalum ya kushugulikia mambo hayo ikiwa Rais pengine yuko kando yeye atakua kama mwakilishi wa mambo mengine.

Kipindi cha Rais mimi nilikua napendekeza kiwe cha miaka mitano, na ikiwa pengine kazi ya Rais ameifanya vizuri na wananchi wameipendelea, anaweza kuongezewa kipindi kingine cha miaka mitano.

Tukija upande wa mahakama zetu, mimi kulingana na vile haki inavyofanyika kule mahakamani naonelea kua kuna matatizo mengi. Ufisadi kweli umeadhiri mahakama zetu. Sasa kuondoa ufisadi nilikua ningependekeza sana kabisa, majudge walipwe vizuri, halafu majudge tumewachagua wawe ni watu wadilifu watu wacha mungu, ambao kwamba watatimiza haki. Watu wengi sana wamedhulumiwa, haki hazitendeki katika mahakama zetu, ufisadi umekithiri sana, na twaonelea hapo pengine majudge hawapati mshahara wakutosha.

Kitu kingine nikiguzia ofisi ya Chifu Kadhi na Makadhi. Makadhi nilikua napendekeza wachaguliwe na Waislamu wote. Kila sehemu itachagua Chifu Kadhi wake na huyu Chifu Kadhi awe anamaadili ya Kislamu, mtu amesoma, dini ya Kislamu anaielewa, awe na shahada ya degree pia ya upande ya uwakili kutoka katika Chuo Kikuu either hapa Kenya ama huko nje.

Mwisho kabisa katika Tume ya uchaguzi. Tume ya uchaguzi ningependelea iwe yenyewe inashugulikia mambo yake badala ya kuhusika katika chini ya nguvu za dola. Iwe yenyewe inafanya kazi zake kando ili haki ipate kutendeka.

Mwisho kabisa hapo ningependelea sana wale wabunge wanao hama vyama vyao kutoka hichi wanakwenda hichi, ama kufanya ndoa ambazo kwamba sijui kama ni halali ama si halali wanatoka chama hichi wanakwenda kingine. Zile sehemu zao za uakilishi bungeni zifanywe kua ziko wazi kupiganiwa tena. Asanteni.

**Com. Ayonga**: Asante sana Bwana Ethiopia, unakitu chote unatuachia?

**Ramadhani**: Sawa.

**Com. Ayonga**: Kwenda uweke pale. Sasa next, atakuwa, Elijah.

**Interjection**: Hajaingia

**Com. Ayonga**: Lukas Adams.

**Lukas Adams**: Kwa jina naitwa, Lukas Adams. Mimi nimeshawahi kukaa hapa Pwani kwa sasa miaka kumi na tano na nimefanya siasa yangu hapa vile vile na biashara yangu. Jinsi ninavyo ona na nimeshakaa kwa hivi vikao sasa karibu tatu, one of the strategies, today's situation in our

country is that the motive of the ruling class is being seriously questioned by majority of Kenyans. For example, our Muslim brothers have essentially opposed the unitary government due to the bad governance that has brought poverty not only to Muslims but to many Kenyans. The same governance has brought inadequate education and, of course, the broken promises that the government promised Kenyans more so during the elections. Indeed the new Constitution, should address the institutional crisis, in particular state crisis. The Constitution should address the least three important issues to promote peoples self confidence, to enhance the respect for life and property both private and public property by the government. Subject the top leader to the rules about the use of power because in our country today, our leaders behave as if they are above the law. We have seen this during the elections whereseveral Kenyans lose their lives after utterances that border on criminal activities. We should subject the top leaders more so the Head of State to the rule of law and to respect the use of power. That power should not be misused.

The absence of an intellectual atmosphere like this one we are having today, to discuss national concerns tend to reduce Kenyans to subservient beings always anxious to take the easy road to issues.

Perhaps the Majimbo slogan could be one of these easy solutions to the complex problem we are having in this country. I can hardly be expected to take lightly those campaigning for the introduction of Majimbo type of government. Neither am I against any system that will bring peace, prosperity and understanding among Kenyans. But in my analysis, the heads of democracy, rest on self discipline not on threats or sanctions. Those who discuss Majimbo, whether unaware or aware, are actually promoting (inaudible). Almost every person who has talked most since yesterday it is very bitter with the present system of government. And this has caused many Kenyans to have harbour hatred among themselves, thinking that perhaps another community or another group of persons is being favoured by this government.

As a Christian I would like to assure Muslim brothers that the suffering is the same, this system of government may not be wrong but, watawala wanaye tutawala wanatufanyia unafiki, mpaka sisi wenyewe wakenya tumebaki tukigawana vipande vipande.

Tunaona ya kwamba, shida kubwa katika Kenya wakati huu ni ukabila. Kuna wengi wenu wamezungumza hapa wakisema serikali inasema hakuna ukabila na huku sisi tunaona kuna ukabila kubwa. Kuna wengine wametaja kwamba ukiangalia sasa kama Mombasa ama Pwani kwa jumla kuna PC kutoka kabila moja, DC ni hivyo, polisi ni hivyo, kusema kweli ni vigumu, binadamu ni kama mnyama mwingine, hatuwezi kuweka fisi anatumikia mbuzi. Lazima awe ni fisi ama ni mbuzi anayeelewa shida za wale mbuzi wenzake. Kwa hivyo tukiangalia wale ambao wametuletea hii mtindo wa Majimbo hawajatupatia foundation ya kutuonyesha hii Majimbo ikiwa introduced itakua kwa njia gani? Tusije tukachukua Majimbo ambaye itasaidia tu wale ambao wanatunyanyasa hata wakati huu. Unafiki hana ukabila, unafiki hana rangi, unafiki hana dini. Mtu kama nimnafiki ni mnafiki, ikiwa anauzia wenzake bangi awe Muslim awe Mkristo atafanya hivyo hivyo. Kwa hivyo mimi ningeomba wadugu zangu, mimi sitoki Pwani ijapokua nimeshakaa Pwani kwa muda mrefu na vile vile napenda Pwani, muangalie sana wakati tunazungumza serikali ya aina fulani, mtindo ya hiyo serikali ndio mbaya au ni uongozi. Na kama ni uongozi ni njia gani tunaweza kubadilisha hiyo bila kurudisha wale wale ambao wametunyanyasa kwa muda mrefu hata kushinda wakoloni. I would like to say that I favour the supremacy of civilians over the rulers and over the army. In this country today there is no link between the Kenyans and the ruler. Today when you see an ordinary Kenyan in discussion with the police or PC he is either being harassed, or is being asked for a bribe. There is no mutual understanding between Kenyans and those who rule them. Ikiwa unaona mtu anazungumza na polisi si ati wanajadiliana kitu ya maana, inaweza kua anataka peana polisi pesa au polisi huyu anataka kumdhulumu, hakuna anayeenda polisi station leo akatumikiwa kama raia wa kawaida mpaka kuwe umesumbuliwa. Certainly our present training and practice by Armed service tends to promote rigid thinking and creating officers who are not able to adopt to changing situations. Kwa hivyo training ya officers wetu lazima iwe inafuata njia ya kuibadilisha na vile vile msingi uwe wa kutumikia watu hasa wale ambao hawana mali. Wenye mali katika nchi hii wanaweza ingia popote, wanaweza lala kwa godoro hosipitalini, wanaweza kulala kwa ngodoro kwa jela, wanaweza kunywa hata whisky

huko kwa jela. Lakini maskini ukienda jela leo uko taabani.

The brocacy of services and the department of defence itself tend to stfle constructive ideas, these compound the problem in our system today, both the army, airforce and navy are put into one seriously impairing the intelectual vitality of the entire officers. Ukiangalia katika njia yetu ya kulinda nchi hii Commander ama yule Chief Commander ni moja katika navy na ndiwe mwenye Air Force hapo yeye ndie ana report kwa Rais. Lazima kuwe na njia moja ya hayo maneno yote kupitia kwa raia. Kwa mfano kwa district kama Mombasa tuwe na committee either ya raia wakisaidiana na yule walio mchagua na hapa tuna chairman ambaye ni DC kitu anajadiliana na polisi huwezi kujua ni nini. Kwa hivyo kwa maneno hayo machache mimi ningeuliza hii new constitution ichukue power zile za rais zote irudishie Raia ndio tutaendelea kwa njia mzuri ndio tutaanza kupata maendeleo.

**Shafket Pervaiz**: Mimi jina langu ni Shafket Pervaiz na represent MEWA, Muslim Education Workshop Association na mtanisamehe ikiwa nitazungumza kwa lugha ya kizungu. Am glad to take this opportunity to thank you very much for giving us the opportunity to speak to you today. Can everybody hear me?

**Interjection**: Ikiwa wanakusikii kwa nini wanajibu basi?

**Shafket Pervaiz**: Okay sawa sawa, anasema mnanisikia kwa nini mnajibu. We were given this book and we have followed this book to the letter and I would like to read out to you what exactly we have taken in this book. What we have in this document is introduction, the Preamble, Constitutional supremacy, citizenship, defence and national security, political parties, structure and system of government, legislature, the executive, the Islamic judiciary, local government, basic rights, land and property rights, management and use of resources, environment and natural resources, and international relations. Those are the topics we felt related to us as the representatives of the Muslim Umma. We as MEWA for your information sir, Muslim Education Work Association was formed in 1985, and officially registered in Kenya on 31st July. The objectives of MEWA are contained in the constitution, the mission statement of the association can be summarized as to: promote, encourage, and improve the standard of education and welfare of the Umma. In the context of the state of MEWA became about, the association invited Muslims at their offices in Mombasa to deliberate and agree on the Constitution Review Process now on going. As a result, the following has agreed and we hereby present it to the Constituion of Kenya Review Commission. Preamble: we felt that the Preamble is important and the Kenyan constitution is being enacted in the name of Allah, as far as am concerned, most gracious, most merciful. To ensure that all Kenyans enjoy the same rights and are accountable to the same responsibilities regardless. Kenya is made up many subnationality that have the common experience of struggling for self determination from time immemorial. It is this common experience that has continued to glue them together and enabled them achieve a prosperous people independent and dependant of one another.

On the topic of citizenship Sir, every person born in Kenya shall automatically be a citizen of Kenya, regardless of the

citizenship status of their parents. Kenya citizenship shall also be acquired through a process of naturalization. The rights of citizens shall be among others; unhindered. Obligation of the citizen shall be among others respect of rights of other citizens. The constitution should allow for dual-citizenship and consider multi-citizenship. Evidence of citizenship should primarily be a birth certificate, either Identiy Card or Passport, should be carried as evidence of citizenship. The structure and system of government we recommend a federal system of government, I think that has been said by many of my brothers twataka Majimbo. The Legislature, all Cabinet appointments shall be vetted by Parliament, some of the most important points. Parliament shall not have unlimited powers to control its own procedures through standing orders. Members of Parliament duties shall be fulltime and they shall not actively engage in other occupation. Voters shall have a right to recall the Members of Parliament by a petition signed by 50% of the constituents in the constituency electors to the Electoral Commission. Members of parliament shall act on the basis of conscious and conviction or on the basis of instruction from the mwananchi and not the party. Removal of the President shall be 2/3 total votes cast. The Executive, that is the President. Qualification of the Presidential Candidate should be age between 45 and 70 years. Education, KCSE or its equivalent with a pass. Budgetry capability Kenya Shillings 500M. The President should serve two terms of five years each and the election date should be fixed and known to all. The President should not be a Member of Parliament and should be elected by popular vote of the entire country.

Now I touch on something which is very important to us as MEWA and my other Muslim brothers. The Islamic Judiciary, that is the Kadhi's Court. The Islamic Judiciary Chief Kadhi and the Kadhi shall be separated from the mainstream Judiciary, funding shall be made as current as now. The Islamic Judiciary shall comprise of a Chief Kadhi, an Islamic Court of Appeal, at list 16 provincial Kenya Kadhis and 52 district Kadhis. There shall be an Islamic Commission that would be required to set up and manage the terms of reference, the process of 5 election, the terms of service, and the employer of the Islamic Judiciary. The Islamic Commission can also take over from the Wakfu Commission and mandate all work. The Islamic Court of Appeal shall comprise Chief Kadhis, two senior Kadhi, two scholars and a senior Muslim lawyer conversant with both common and Islamic Law. The Islamic Commission shall establish an all Muslim law board to advice on all Islamic affairs. The Chief Kadhi inconsultation with this board shall be the government's advisor on Islamic affairs and shall be consulted by the government on all matters pertaining to Muslim affairs: Kiswahili, English and or Arabic shall be the languages of communication in the Islamic Judiciary. There shall be a Commencing Judiciary, a Supreme Court and Anti-corruption Court and a Constitution Court. Appointment of Judiciary Officers in the mainstream Judiciary shall by Judiciary Service Commission. Judiciary powers shall be independent of the Executive and both main stream Judiciary and Islamic Judiciary shall review acts of Parliament to ensure the rights of citizens are maintained.

We have also touched on Local Government among many points. I think I do not have much time, I will clear with basic rights, which is very important. Fundamental rights need to be clearly defined in the Constitution so as to protect the people against police harassment, hap harassment, bailing of religious protection etc. In case of murder, death penalty shall be observed. Otherwise the decision to pardon a murderer to remain with the family of the murdered person in exchange of compensation.

We have many cases now where people have murdered they are rotting in jail while they could be outside and doing murder by default.

Free health care and education to secondary level. Institution that benefit of public funds should not discriminate on employment and other issues. An Islamic religious education to be taught and examinable to all Muslim schools country wide. There should be not a question of noteachers which is a government responsibility.

On land and property rights, all allocation of state and trust land should be handled by the local community in that area. All private land acquired by individual organizations on the pretext of compulsory acquisition by government should be returned to the lawful owners. Any land allocated to the above, must be utilized for its intended purpose and not for sale. If not utilized it can be repossed. With those few points Sir, I will represent this document and a CD to you and we hope this requirements shall be taken seriously, and shall be part of the review Constitution of Kenya. Thank you very much.

**Com. Ayonga**: Please before you leave we have a question.

**Com. Wambua**: You said an MP should serve on full time basis and if they who do not perform they should be recalled. (Rest of the question inaudible)

**Shafket**: Thank you very much, that is a question we deliberated on at length in that meeting we had and I call a team leader who is our Vice Chairman and I would like him to say something on that. If you do not mind with your permission.

**Chairman MEWA**: Members of Parliament who are not performing ought to be recalled. The criteria to be used would be, (inaudible, not on microphone)

**Com. Wambua**: Well let us not pursue it further we will think about it.

**Shafket**: Thank you very much.

**Com. Ayonga**: I want to thank you and if you are going to leave us a copy, go there and sign your name. Now time is against us.

**Swaleh Adinani**: Salaam aleikum. Mimi naitwa Swaleh Adnani. Natoka hapa Mwembe Kuku, na mimi ni Monitor wa Kenya Human Right Commission hapa Coast Province. Yangu mimi yakuzungumza hapa ni makubwa nazungumza nikiwa Pwani, mzalendo wa Jimbo hili la Pwani. Kwanza kwa vile sisi watu wa Pwani ndio watu ambao kwamba tumekua marginalized and discriminated among the Kenyan community we are the most marginalized and discriminated people. Taabu ilioko sasa hivi,

watu wetu wakija hapa kuzungumza mambo ya President, mambo ya nini, nikukosa awareness, watu wetu hawana awareness yakutosha kuzungumza Katiba hii. Na makosa haya Bwana Commissioners yatokana na nyinyi. Kwa sababu mnazungumza haya na hakuna Civic Education iliyofanyiwa watu wetu kuelezwa kuhusu mambo Katiba iliyopita. Mpaka sasa hivi nakwambia Civic Education iliyofanywa hapa mostly ile inaitwa Kanu zone, imekua ikisimamiwa na watu wa Kanu. Watu wale wanafika kuambia watu katika Civic Education kwamba, chukueni kura maadui wa Moi waja, maadui wa Kanu waja watawanyang' anya viti. Hiyo ndiyo Civic Education watu wengi waliopatiwa ninaushahidi wa kutosha. Civic Education Providers, kwa mfano wa Mvita Constituency, hapa ni Bwana Msehu na Bwana Rajab Sumba ni Chairman na Vice Chairman wa Kanu. Ukienda Changamwe na Kadhalika Bwana Mikidadi ndio masekretari wa Kanu hao ndio Civic Education Providers, kule kwingine hakukufanyika kabisa. Twataka kujua kama Lamu, Tana River, na wapi hakuna kitu kama Civic Education iliyofanyika. Watu wetu hao, Bwana Commission kuna swali?

**Com. Ayonga**: Mimi nataka kukuuliza na kukuambia kwamba hapa tumekuja kutoa maoni na tungalipenda utoe maoni yako kuhusiana na Katiba. Lakini si kusahihisha Civic Education ilifanywa au haikufanywa. Kwa maana sisi sote tumekuweko hapa, jana na leo watu wametoa maoni. Yawe ya kutokana na Civic Education, yawe yale mawazo ambao walio nayo, experiences zao, watu wametupa maneno. Kwa hivyo na wewe utupe yako.

**Swaleh**: Asante Bwana Commissioners hii ilikua for information, kukujilisha kwamba mtakayoyafanya yoyote watu wetu wawe aware. Lakini sasa tatizo kubwa linalo sisi tunataka Katiba ibadilishwe kuhusu mambo ya ardhi. Ardhi yetu hapa Pwani ni ardhi ambayo kwamba babu zetu na baba zetu wameishi hapa kutoka kizazi cha kwanza. Leo Mpwani halisi hana haki ya kumiliki ardhi. Mimi nakwambia haya, mimi wazazi wangu wametoka sehemu za Lamu. mahali panaitwa Wito ni 300 years back kijiji chetu kilichoundwa mpaka leo hawana haki ya kumiliki ardhi. Lakini mtu akitoka Upcountry kwa vile anajua procedure, anajua namna gani atafuata katika Ardhi House vile atafute hati. Mimi nitamuzia kwa sababu nataka kusomesha mtoto wangu nina ekari mia moja za kukodisha, nitamuzia ekari tano hili nipata school fees. Eka tano zile yule atakaye nunua just two months anakuja na hati ya kumiliki ardhi. Mimi ardhi ile nimekaa nayo for 300 years, 400 years hatuna hati ya kumiliki ardhi kabisa. Ardhi hatujui namna gani tutafuatilia kwa sababu the system is against us.

Jambo lingine ambayo kwamba nataka kuzungumza ni kuhusu education, sisi education watu wa Pwani hatupewi usawa kabisa katika serikali. Kuna Vyuo vikuu vingi vya serikali, Polytechnic na nyingine, lakini watoto wetu wanapopita mitihani kwa bahati, kama skuli ni mbaya, Parents Teachers Association ni mbaya watu hawana awareness ya kujua maana ya elimu ni nini, hawapati nafasi ya kujiunga na college zile. Nataka serikali itengeze system ambayo kwamba kila college kwa mfano, Kenya Polytechinic, Nairobi ama Kenya Science Teachers College, ama Utalii college iwe ikichukua wanafunzi from every district. Sikuangalia tu kwamba wanafunzi fulani ama Principal apewe nafasi ya kuchagua watu anaotaka. Angalie Kwale district, lazima Utalii College ichukue wanafunzi watano kila mwaka. Lamu district namna hiyo, iwe twachukuliwa katika zile colleges ili na sisi tuweze kupata elimu.

Jambo lingine nazungumza ni kuhusu mambo ya Uislamu. Kwanza nazungumza Upwani maanake nafikiri Wapwani walikuweko

kabla huu Uislamu na Ukristo hujaja. Uislamu umekuja kutukuta baadaye. Nazungumza kuhusu Uislamu kwamba sisi Waislamu hii dini ni yetu na hatuna haki ya kuomba mtu kwamba mimi nataka kuabudu. Hii nobody can deny us. Hakuna mtu anaweza kutukataza sisi kuabudu. Tunapo katazwa kuabudu itakua ni jambo la makosa tunayofanyiwa ki sheria. Lakini kwa sababu ya Kenya nzuri na mambo mazuri nataka tuwe nayo ni kwamba tunapotunga Katiba mfikirie sana kuhusu Kadhi's Court. Leo Kadhi's Court yeye nikama Magistrate, Chief Kadhi mwenyewe ni kama Magistrate hana uwezo wowote. Tunaomba katika Katiba hii Chief Kadhi awe ni sawa sawa na Hakimu Mkuu wa Kenya. Hii ni kwamba uamuzi wake uwe final kama ndugu zangu wengine walipotangulia kusema na mambo mengine yale yanayohusu Waislamu sisi yote yakubalike kulingana na wanavyuoni wetu, na Maimamu wetu walivyopendekeza kwenu.

Haswa kuja hapa kwangu nilikua nataka tu kuwajulisha kwamba watu wa Pwani walipodhulumiwa kwao hii Hall haingekua hivi ingefurika sana watu hawana awareness, they do not know what is going on, hawajui watakuja kuzungumza nini, ndio unaona wamekuja watu wachache sana kuja kuzungumza, ijapokua wao ndio waliodhulumiwa sana, ndio walionyanyaswa sana na Katiba iliotangulia, lakini they do not participate fully katika hii Constitutional Reform ilioko kwa sababu ya wao kutokua na awareness. Asanteni sana.

**Com. Ayonga**: Na sasa nitakaye jambo moja linalo sema kwamba waliomo hapa hawana awareness.

**Speaker:** Mambo ya kilimo ilitupunguze matatizo ya wafanyi, vijana ambao hawana kazi.

**Com. Ayonga**: Naona dakika zako zimekwisha.

**Elisha Miogo**: Asante Bwana Commissioner, namalizia kabisa.

**Com. Ayonga**: Summary hiyo ya mwisho.

**Elisha Miogo**: Ndio ya mwisho hiyo, naomba tuzugumzie kuhusu mambo ya Majimbo, kwa kweli Majimbo ni kitu mzuri, lakini inamatata chache, kwa sababu tukiangalia kama nchi zaWest Africa nyingi zimekumbwa na matatizo ya aina bali bali kwa sababu ya Majimbo. Walikimbilia Majimbo hawakuwa na mipangilio, nchi ikaingia katika misukosuko zugu ya ghasia, nchi zikaingia katika kumwaga damu ya wananchi, na mpaka sasa wale wanaosoma kuhusu nchi za West Africa wanajua. Mimi ningeliomba mipangilio tulioanza nayo ya district focus, ni nzuri, ililetwa kwa mfumo mzuri na wananchi wakaelewa, haikuleta shida katika Kenya. Naomba watalamu hao wanaotilia mkazo Majimbo watuonyeshe, watoe practice ya kuridhisha kwamba hii Majimbo ya kija maana yake ni hii na hii na hii. Lakini ikiwa watashindwa mimi naomba wachane na mambo ya Majimbo wataalam wa kisheria waweze kutafuta namna watakavyo leta policy ya Majimbo na ndio tuweze kuifanyia kazi.

**Com. Ayonga**: Asante hayo ni maoni, kila mtu ana uhuru wa kutoa maoni yake, yeye hapendi Majimbo, kuna wale

wanapenda Majimbo na mwingine anapenda kingine ni maoni yako.

**Elisha Miogo:** Nitatoa sababu moja, kama jana nafikiri tulipokua pale mbele, wengi wameleta maoni yao, ambayo ni kawaida anasema anataka kama ni Chief, atoke hapa hapa Majengo sawa, kama ni DO, atoke hapa hapa Majengo, kama ni DC atoke Majengo, kama ni PC atoke Majengo kweli hiyo itafanya Kenya kuwa katika hali ya shida ninaomba tu kwamba Mkenya yeyote mahali alipo atambulike ni Mkenya .

**Com. Ayonga**: Hayo ni maoni yako hapa hatuko katika debate. Yule aliyeona DC atoke Majengo, PC atoke Majengo ni maoni yake na kwa hivyo tusiingilie maoni ya mtu yeyote hapa. Kazi yetu tumekuja hapa kuchukua maoni. Ningalipenda kuendelea tafadhali, ningalipenda tuwe na ukimia ili tuendelea. Yusuf Nuru yuko? Hajaonekana. Rashid Mvita, Francis Gathu Njenga, James Mwangi, Mustafa Muhamed, ni wewe?

**Mustafa Ahmed:** Commissioners, kwa jina naitwa Mustafa Ahmed na niko hapa kuwakilisha Muslim Youth ya Mombasa. Bwana Commissioners, wazee, na viongozi wa sehemu mbali mbali ambao wako hapa. Kina mama na kina baba salaam aleikum. Ni furaha kubwa kwangu mimi kwa niaba ya wenzagu kuwa hapa leo ingawaje nilikua hapo jana nikifuatiliza mazugumzo haya kuhusu mambo ya Katiba na leo kuja hapa kueleza machache ambayo tumekaa chini tukafikiria kuongezea. Kwa yale ambayo wenzetu wengine wamejaribu kurekebisha sehemu baadhi. Ningemshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha ste kua hapa kwa pamoja kwa hali mzuri na njema na ya afya na haya ambayo nitayasema hapa aniongoze niweze kusema mambo ambayo yatafaa, jamii yetu, Kenya yetu na kwa watu wote kwa jumla. Na wenye kupokea nawomba Mwenyezi Mungu ajalie wayachukue maneno haya na wayadhibiti waende nayo na yawe yatakua ni ya manufaa kwa sisi sote.

Kwanza ningependelea kuzungumza, kutoa maoni kuhusu upande wa Uraia ambapo iko kulingana na kitabu ambacho tumepewa kama guideline zetu. Mtoto yeyote atakaye zaliwa hapa Kenya na awe ataishi hapa Kenya na asome hapa Kenya basi anahaki ya kua raia wa hapa Kenya pasipo na kizuizi aina yeyote. Hiyo ni njia moja ambayo tungependelea iwe bila kutatizana kuhusu vizazi, ingawaje serikali ina njia nyingi ya namna ya kupatia mtu citizenship ambayo kuna by birth, by registration and by naturalization. Lakini nimeongea tu kuhusu kwa kuzaliwa tu. Kijana yeyote atakaye zaliwa awe atakua ni Mkenya bila ya ubaguzi wa aina yeyote. Kama ambaye kuna sehemu za matatizo ambazo zinatokea hapa kwetu hizo ziondoshwe.

Kuhusu upande wa kupiga kura ni maoni ya kwamba kuanzia umri wa miaka kumi na sita mtu awe ataruhusiwa kuenda kupiga kura umbali wa miaka kumi na nane. Ikiwa tunaweza kuongezea itakua ni bora zaidi kuanzia umri wa miaka kumi na sita watu waruhusiwe kwenda kupiga kura.

Kuhusu ugombeaji wa Urais ubakie kwenye umri wa thelathini na tano lakini usizidi miaka sitini. Kuhusu malipo ya mishahara na marupu marupu ya wafanyi kazi wa serikali na wabunge wa sehemu za councils. Tungependelea wananchi wahusishwe

katika mipango juu ya maongezeko ya zile pesa zao na mishahara yao yawe yakijadiliwa na wananchi ili waweze na wao pia kushiriki kwa sehemu fulani iwe haki itaonenkana juu ya mishahara yao. Sio wawe watu wanajibadika mishahara kwa kupenda wao na kwa ajili ya manufaa yao wakiwaacha wenzao wengine kwa sehemu hizo hizo za serikali wakiwa wanapata taabu.

Nguvu za Rais ningependa zigawanywe ili asiwe na nguvu nyingi sana ili kama kila jambo ni lazima lipitie kwake. Ziwe zile nguvu zipunguzwe na kuwe kuna sehemu ambayo inahusika katika kumsaidia kwa kazi kama hizo. Kwani baadaye zinaleta matatizo na malalamiko yote yanateremka juu yake kama mtu mmoja.

Tukija kwenye mfumo wa kadhi, maoni yetu ni kwamba, idadi ya Makadhi walioko ni ndogo sana kulingana na Waislamu ambao wako hapa nchini. Kwa hivyo Makadhi wawe wawe wataongezwa kwa idadi kubwa zaidi. Tuko Waislamu karibu million nane, na tukiangalia Makadhi wanaowakilisha sehemu zao ni kidogo sana, ndio maana mara unaona Chief Kadhi, ukienda ofisini leo humpati yuko Nairobi, siku ingine Chief Kadhi yuko Kisumu, siku ingine Chief Kadhi yuko Nakuru na sababu ni kwamba shughuli zimemzidi, na kazi zimekua ni nyingi na yeye ni mtu mmoja anaye shughulika hivi. Kwa hivyo hao Makadhi wawe watakua na Makadhi wa provincial level ambao kutakua na Kadhi mmoja mkuu akiwahudumia na baada ya hiyo kutakua na Chief Kadhi ambaye yeye ndiye atakaye kua juu kabisa akishikirikiana na wale wa mikoa pamoja na wale wa vijiji. Hiyo itarahisisha kazi ya Kadhi na itakua ni ubora zaidi. Na sehemu ya Kadhi za Makadhi na Chief Kadhi ziongezwe wasiwe tu watabakishwa kwenye nyanja za talaka na ndoa, vitu ambavyo mpaka sasa ndio ambao Makadhi wanasimamia. Kunashuguli nyingi na ambapo tungependelea wawe Makadhi watapewa nyadhifa kubwa zaidi kuliko zile ambazo wamepewa hivi sasa. Koti ya Kadhi iongezwe ikiwezekana iwe hasa ni koti kuu ili kesi zote ziwe zitaanzia chini mpaka juu zimalizikie kwa Kadhi, sio ziwe zinaweza kurukishwa zitoke kwa Kadhi ziende kwa sehemu ya koti ingine ambayo hukumu ile itakua ni ya kinyume na ile hukumu ambayo imeanzilishwa huko nyuma kupitia kwa Kadhi. Makadhi wawe wanachaguliwa na vikao vya wana vyuoni halafu Kadhi mkuu awe anachaguliwa na taifa. Wananchi wote wawe wamemchagua. Pia Kadhi awe au Makadhi watakua na elimu ya hali ya juu kwa uchache, Kadhi awe ana degree ambao amesoma university na huku awe ana elimu upande huu wa Islamic Students asichanganye kwa pamoja ili aweze kwenda sambamba na ufumo wa kimaisha wa ki leo.

**Com. Ayonga**: Summarize please.

**Mustafa**: Kwa ufupi ni kwamba sehemu iliyobaki ni kuhusu vijana ambapo Katiba ipangwe sehemu ya kusimamia vijana katika Recreation Centers, na mipango mingine ya kuwahifadhi katika utamaduni wao ili wawache kuharibikiwa na kupotea. Na ipangwe sehemu katika Katiba ambayo itakua inamlida Muislam awe anaweza kufuata sheria ya haki ya dini yake inavyo paswa. Ili aweze kufuata dini yake, Muislam asiwe anaweza kukwepa maamrisho ambayo yamewekwa kidini. Kwa hivyo tunaiomba Katiba ipangwe sehemu ya kua Muislam atakua madhari yeye amekubali ni Muislam amejifunga katika kifungu, ambacho ni lazima ile dini itakua sheria yake inamfuatiliza bila ya kutoka kukimbilia sheria zingine. Kwa hayo machache ningetoa asante sana na washukuru nyote wasalam waleikum.

**Com. Ayonga**: Asante Bwana, unaweza kutoa maandishi yako. Next atakua Josphine Njeru, Muhamed Idrsspengine ametoka, Sakina Mosque.

**Imamu Muhamed**: Salaam aleikum. Kama mlivyo sikia, jina langu kidogo limekatwa, sababu kazi yangu ni Imamu Muhamed Idriss Msikiti Sakina Mombasa, Msikiti ambao nimaarufu sana East Africa au dunia mzima. Nam, lengo kubwa la kuja hapa, nafikiri kutoa mawazo yetu kama wananchi wa Kenya, kuhusu Katiba ya Kenya, inawahusu wa Kenya. Na lengo ni kutoa maoni, twataka nini katika Katiba hii ambayo kwamba itakayo kuja sasa si hile ambayo ilikuako haikupitia mikononi mwa wananchi. Na kabla sijaendelea Bwana mwenye kiti wa Tume lugha ambayo nitaizungumza lugha ya kiswahili sababu lugha yetu, na kama ilivyo ni Kiswahili. Kwanza naomba kujua dakika zangu ni ngapi nizungumze hadi nikijua dakika zangu fulani.

**Com. Ayonga**: Nikiangalia wingi wa watu waliomo sasa ningalipenda maana wewe ni mzee kiongozi wa Msikiti na kupa dakika tano. Hebu niongee, unajua kama tuna democracia hayo ni maoni yangu; na hebu nisikie aliyo nayo na kama anaweza kupeana within 5 minutes. Maanake ni hii, tumebaki na wakati kidogo na nikiangalia wakati ambao umebaki, mimi kama mwenyekiti nina haki ya kuweza kuona wakati nilionao na niwagawie watu wote hata kama wanapata kidogo kidogo, lakini sasa mkianza kusema la, la, hiyo haitatusaidia. Ikiwa mama ana chapati moja na ana watoto kumi hatampa mtoto mmoja ile chapati ataikata vipande vipande angalau kila moja apate, kwa hivyo wacha niongee, huyu ni mtu mzima, na nitajua yale aliyo nayo. Je unayo memorandum?

**Imamu Muhamed**: Ndio nata kuwajulisha wenzangu walioko hapa, hapa nafikiri ni mahali pa kuzungumza maneno mengi au marefu, muhimu ni kuandika memorandum tukapeleka. Natuliambiwa siku nyingi sana wapata mwezi wa pili huu tupeleke memorandum na ofisi ziko wazi. Hapa ni kutoa maoni kidogo tu kwa uchache kwa hivyo hata tukipewa dakika tano nafikiri tutosheke kua za tosha. Lakini muhimu tupeleke memorandum.

**Com. Ayonga**: Asante, lakini yale makubwa yote uliokua nayo, uyatoe.

**Imamu Muhamed**: Sisi kwanza Waislamu tukianza kufanya jambo lolote ua twasema bisimilahi rahmani rahimu maanake, kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi rehema Mwenye kurehemu. Sasa nami nasema, kabla sijaendelea na hayo ambayo nataka kuyasema, kwanza nasema hivi, kama watu Wapwani wa mkoa huu, jambo la kwanza muhimu twataka ni Majimbo. Pili nafikiri ndio kama bismilahi vile twasema kwanza Majimbo.

Halafu sasa naendelea, katika vitabu tulivyopawa kuiangalia Katiba yetu ya Kenya kuna kifungu inazungumzia haki za lazima kwa raia. Na raia ndio sisi. Na haki zote twajua haki ni kitu gani, na ikikosekana haki ndio matatizo utokea. Sasa mimi nazungumzia kidogo tu haki ya raia, uhuru wa kuwabudu, yaani ibada ni miogoni mwa haki za lazima kwa raia. Hili linaeleweka kwamba ibada ni kitu gani na watu wataka wafanye nini? Sisi kama ni Waislamu, nafikiri twaweza kusema hapa Kenya ni dini

mbili ambazo ndizo maarufu na ndizo zinatuongoza, Uislamu na Ukristo. Kama Waislamu twaweza kusema sisi tunayo Katiba yetu ambayo ni Koran. Lakini ni Waislamu lakini wa Kenya. Katiba ni ya Wakenya ijapokua ni Waislamu lakini tutoeni maoni yetu na tuzungumze yale ambayo yanayotuchoma sisi wa Kenya kama Waislamu.

Uhuru wa kuabudu ni jambo ambalo ni muhimu sana na nihaki ya raia ya lazima. Kuna haki nyingi, mfano haki ya elimu ya bure ni lazima kwa raia. Sasa mimi nikirudi upande wa kuabudu, kama sisi Waislamu ibada zetu tumepangiwa na Mungu, hakuna anayeweza kutupangia yeye mwenyewe. Mfano sisi tuna siku moja kubwa sana, inaitwa siku ya Ijumaa. Ijumaa ni siku yetu sisi moja ni kubwa sana, kama ilivyo wengine kuna siku ya Jumapili ni siku kubwa sana, na wengine pia siku ya jumamosi. Sasa sisi katika Katiba hii ambayo kwamba hivi sasa imekua vugu vugu la Kenya na Wakenya, kuunda Katiba ambayo itakwenda na mwelekeo wa Kenya vile ulivyo hivi sasa. Kwa hivyo ndani ya Katiba yetu itakayo kua kuwe na kifungu Waislamu ikifika saa tano unusu siku ya Ijumaa hata wakiwa ofisi gani waruhusiwe waende wakafanye ibada. Na jambo la pili, haya yote si kwamba twapanga sisi hayo tumepangiwa na Mungu, na ni haki yetu na ikiwa haki, ni lazima kila mmoja apewe haki yake. Hii ni haki yetu Waislamu lakini ni Wakenya, na vile vile sisi tuna Iddi ambazo tumepagiwa na Mungu. Idi moja tumepata kwa serikali ya Kenya ya Idi ya ramadhani kwamba inakua kwa wakenya wote, Waislamu na wasio kua Waislamu lakini bado mmoja, iwe ndani ya Katiba yetu Iddi mbili zote Waislamu wa Kenya zipatikane hiwe na pumziko kwa Waislamu wote na wasio kua Waislamu. Halafu tukirejea hii haki, sisi tukizungumzia kama Koran tumeikubali kwamba sisi ni Waislamu. Naikiwa tumeikubali ni haki yetu na zilivyo ndani ya Koran pia ni haki yetu.

Ndugu zangu wamezugumzia ofisi ya Kadhi hapa, ofisi ya Kadhi ndio inayotaka itumikie zaidi Koran. Kuna mambo mengi ndani ya Koran ambayo sisi ni lazima na zile kunakifungu kwamba ni lazima haki ya lazima, na sisi ile haki yetu tuipate. Iwe ni lazima tuipate ile haki yetu masalani ni mfano twasema, kama vile uwezo wa Kadhi uwe ni mkubwa, na Kadhi asiwe kuangalia ndoa na talaka na mirachi peke yake angalie na masilahi yote. Na kama ilipozungumzwa hapa sitaki kuzungumza, tumezungumza sana kwenye memorandum ambayo itapelekwa.

Halafu nikirudia pia, ndugu zangu bado walizungumza habari ya nguvu za Rais. Leo tumesoma katika Katiba, Rais aweza kumfuta mtu kua hampendi tu, asiwe na kosa, hasha, hampendi tu pengine ofisi ameingia ya DC, ya DO akaingia Rais akamuona mtu hakumpendeza pengine sura zake si nzuri au nini, basi aweza kumwambia DC mfute kazi, hana makosa. Hizi nguvu ziko kwa Rais, sasa zile nguvu zimezidi sana kwa Rais mpaka ikawa hali imekua hivi ilivyo hivi sasa. Kwa hivyo kwanza twasema nguvu za Rais lazima zipunguzwe. Na isitoshe, bunge ndio iwe chombo mategemeo ya raia wa Kenya. Mategemeo ya raia iwe ni Kenya hata Rais masalam aweza kuchagua Mwaziri, lakini wasipitishe Mawaziri wake kua Rais lazima wafike mbungeni kwanza. Mkuu wa sheria achaguliwe bungeni, mkuu wa jeshi achaguliwe ndani ya bunge, na wengine wote wachaguliwe ndani ya bunge, si Rais peke yake, haya yamekosekana ndio ile haki pia Kenya mpaka sasa ikawa hakuna; Yeyote utakaye mchagua kumfanya mkuu wa sheria au Judge na mwanaye wakaiba, yule Judge afanyia mtoto wa, nani, mtoto wa fulani ndio amenipa kiti hiki nikumhukumu sawa sawa mambo yatakua si mazuri, kwa hivyo hata kama kuna kesi itakua hakuna kesi. Na kama tunavyoona katika Katiba yetu ambao hii sasa twataka kuibadilisha hata ikiwa mtu amehukumiwa kufa

Rais ana haki ya kusema wewe huwezi kufa mwacheni awe huru. Hata Rais akifanya kosa ambalo kosa lenyewe pengine amedhulumu au ni haki ya raia, wale waliompatia kura Rais hawezi kupelekwa kotini. Nguvu hizi zimekwenda sana mpaka ikiwa nchi imefika hapa ilipofika leo. Lakini twasema nguvu kama hizi zipungue, natengemeo zaidi liwe ni bunge ndicho chombo ambacho chaweza kutoa mambo mengi au mamlaka mengi ikiwa mtu leo amechaguliwa mkuu wa sheria. mkuu jeshi alichaguliwa ndani ya bunge, nafikiri sauti ya kumfuta itakua ndani ya bunge. Hili twaomba liwe hivyo katika Katiba yetu ambayo kwamba tunayoitaka hivi sasa. Kwa hivyo nafikiri nachunga ile time dakika tano zangu zimekwisha.

**Com. Ayonga**: Nimekuongeza kidogo juu yake.

**Imamu Muhamed**: Umeniongeza ingine kidogo juu yake, kwa hivyo nafikiri haya ndio ilikua mambo muhimu. Sasa nitarudi kidogo basi, mzee mwenzangu ameniongeza wakati nitarudi upande wa afya. Afya twaweza kusema haki ya lazima kwa raia. Leo tuangalie hosipitali zetu ambazo twaweza kusema hospitali ya Mkoa. Bila ya shilingi mia huwezi kupata hapa panadol ya shilingi tano. Sasa hebu tumwangalie mwananchi wa kawaida, kuna mtu mwananchi wa kawaida anaweza kukaa wiki mzima hajui shilingi mia ni kitu gani, naye ni mgonjwa tutampeleka wapi. Kwa hivyo irudi iwe ni Katiba, kwamba Wakenya wote wanahaki ya lazima, afya yao iwe bure serikali iweke mfuko maalum kuangalia raia wa Kenya matibabu ya hosipitali za serikali zote iwe bure kwa sababu kuna watu hali zao mbaya hawajiwezi. Naikiwa hawajiwezi mtu aweza kukaa nyumbani afe na ile haki yake ataikosa, hii ni mwongoni mwa haki za lazima kwa raia wa Kenya.

Halafu turudi upande wa elimu, elimu pia vile vile huenda ikawa haya yamo ndani ya Katiba, lakini tatizo lenyewe ile Katiba yenyewe kupata, hata leo utaona na pia haya hayoko hapa watu wanasema ha, hata mkienda mkitoa nini ha hayo tu. Lakini sivyo, sisi kazi yetu ni kutoa na kupeleka yawe, yasiwe, yaweza kua wakati mmoja. Yawe hivi sasa au yasiwe lakini wakati fulani yaweza kua yale ambayo tuliotarajia. Najua nazungumza kiswahili cha hali ya juu kama cha fahamika au hakifahamiki, kwa sababu hiyo lugha yetu ni Kiswahili na sisi ni Waswahili. Ijapokua watu wasema hakuna watu wanaoitwa Waswahili lakini hakuna lugha isio na wenyewe.

Twashukuru pia serikali imeifanya kiswahili ni lugha ya taifa lakini kiswahili ni lugha ya wenyewe kutoka mwambao huu Wapwani wote wenyewe Waswahili na lugha yao ya kiswahili. Kwa hivyo lugha in aweneyewe, kwa hivyo nafikiri kwa uchache hayo yatosha na mengi ambayo kwamba tumeandika halafu twapeleka nashukuru mzee mwenzangu kwa nafasi hii ulionipatia.

**Com. Ayonga**: Asante sana, kwa maneno yako brief ambayo umetoa maneno ya maana sana na je utatupatia hiyo memoradum?

**Imamu Muhamed**: (Inaudible).

**Com. Ayonga**: Asante sasa next . Omari Muhamed, Evanson Kanyua.

**Interjection:** Amesema ya kwamba leo hakuja.

**Com. Ayonga**: Basi tumeelewa huyu ni ndugu wa ile lugha ngumu lakini tumeelewa, Omar Muhamed, Janet Miroki, Mama ambaye aitwa Janet Miroki. Lakini siuliongea jana mama?

**Janet:** Ndio.

**Com. Ayonga**: Na nikwanini leo tena? Ngoja kwanza wacha wale ambao hawajakunywa maji hata kutema mate wacha niwapatie nafasi. Sidio? Hiyo ni haki, John Magawi. Mwinyi kombo, akae karibu baada ya huyu mzee. Mzee kuna kiti hapa, endelea.

**John Magawina** : Asante sana mwenye kiti, kina mama na wazee.

**Com. Ayonga**: Sema majina yako yaingie katika kanda.

**John Magawi**: Jina langu ni John Magawi. Katika mambo ambayo ningependa kuyazungumzia hapa leo, ya kwanza kabisa ni katika sheria, in Law Courts. Katika hizi koti zetu utakuta kwamba haki hua haitimizwi sana kwa sababu mimi kama mwananchi wa kawaida, na kuna wananchi wa kawaida kama mimi ambao waniona hii. Mtu anapo pelekwa kotini akiwa na shida, hua tunasema kwamba, one is innocent until proven guilty. Sasa utakuta kwamba wakati unapelekwa kotini utakuta umekataa mashtaka, kwa kua haukutenda, baadaye utapelekwa rumande sasa ile kitu ningependa serikali iangalie ni kwamba hii duration ya kukaa rumande hua ni kama 14 days. Sasa wakati mtu yuko rumande yuko for 14 days na yeye is not guilty until he will be proved guilty, hua anaumia. Sasa ile kitu serikali iangalie ni kwamba haki ya mtu wa kawaida hata kama hajakua proved guilty hua twangalie hile muda wa kukaa pale rumande iwe kidogo kwa sababu hana hatia pengine. Kwa hivyo muda huo wangaliwe. Hiyo ni point no. one.

Point no. two, katika nchi tunaona aslimia zaidi ya hamsini vijana hatuna kazi, na serikali imejaribu sana ku-promote yaani kutengeneza hii sector ya Jua Kali, sasa katika sector ya Jua Kali unakuta kwamba serikali yenyewe haijatupa uhuru wa kufanya kazi katika Jua Kali. Ijapokua am very sorry to mention this kua just in recent time tumeona intimidation kwa watu wa Jua Kali kua umeambiwa ufanye kazi yako, ama umeanzisha kazi yako kufanya lakini serikali inajaribu kukata mikono yako. Ile kazi yako ambayo ungejipatia chakula, kulisha watoto na wasome, sasa inaharibiwa by the same same arm of the government. Sasa hiyo ndio sisi kitu naangalia kwamba serikali iangalie sana mtu wa kawaida huyu ambaye asilimia ni more than 50, they are jobless na wanatafuta njia ya kupata kazi. Hizo kazi zao zinaharibiwa na serikali. Serikali iangalie and this should respect the will of the public. Hiyo ni point no. two.

Point no. three, kuna sheria ambayo inasema kila mwanakenya ambaye ametimiza miaka kumi na nane awe amepata kitambulisho. Katika hali ya kitambulisho siku hizi naona ni nzuri watu wanaipata lakini police hawaielewei maana ya kitambulisho wakati na wapi kuibeba kitabulisho. Unakuta wewe mwananchi unatembea wakati wowote unashikwa na police unaulizwa wapi kitabulisho. Sasa kama hauna unaona kwamba unashikwa pengine unaenda kufanyiwa mambo ambayo pengine utatoa pesa ama utaumia. So the Constitution, I think inatakikana iseme, once any Kenyan is from 18 years and above they should own a National Identity card and not to carry a National Identity card, all the time so there should be a difference between kubeba kitambulisho wakati wowote na kua na kitabulisho. Kwa hivyo wananchi wanaumia sana hiyo ni point no. three.

Point no. four, katika institutions za serikali, the government institutions tunaona kwamba kuna public offices ambazo zinamilikiwa na watu, na hao watu pengine wamechaguliwa na wamekua appointed by the president, sasa kile kitu ningeomba kwanza, kwa sababu tumeona mara nyingi kwamba mtu, kwa mfano anakua retired general, akishatoka pale after retirement anapewa kazi ingine after all unaona kwamba kuna some other people ambao wangepata hizi kazi, kwa sababu hatusemi kwamba all retired people are experts, it we also have some experts who are not posted anywhere. So they should also have to be posted. Kwa hivyo hii mambo ya pengine President kua na ile nguvu ya kuchagua mtu yeyote kuweka katika post fulani ni vibaya kwa mfano unaweza kuona kitu kama vile nimesema retired general be the Minister for health. Sasa huyu unakuta hana idea ya udakitari ama hakusomea udakitari yeye alisomea kama mambo ya forces ama arms. Sasa anapelekwa katika health. Sasa mtu hapo unakuta kwamba kuna incompetence and inconvinience. Kwa hivyo hii pia serikali iangalie na hizo nguvu za President pia ziwe limited.

Point no. five, mtu yeyote ambaye atakua anagombea Urais, akigombea kwa mara ya kwanza hakufaulu, ya pili hajafaulu asigombee kwa mara ya tatu kwa sababu hiyo ni dhibitisho kwamba wananchi hawamtaki. Sasa hapa utakuta mtu ana vie for Presidency for more than two times, na bado anataka kuendelea for the third time knowing very kwamba yeye ashakataliwa na wananchi. Ni hayo tu ninayo kwa leo asanteni.

**Com. Ayonga**: Asante, kuna kitu ambacho utatuachia? Enda uweke kidole. Sasa ni mzee Kasim Mwinyi Kombo, sijui kama nimepata majina yake sawa sawa. Na je unamaandishi yeyote?

**Kassim Mwinyi**: Nitakupatia baadaye.

**Com. Ayonga**: Okay endelea.

**Kassim Mwinyi**: Salaam aleikum. Mimi nimekuja kwa niaba ya Najaha Muslim School.
**Interjection: Com. Ayonga**: Sema jina lako.

**Kassim Mwinyi**: Jina langu ni maarufu na julikana Maaalim Kassim Mwinyi Kombo, ambaye ni mdhiri wa Najaha Muslim school, majengo ya Roka. Nimesimama hapa au nimeketi kwa niaba ya wanafunzi na wazazi wa Najaha ili kutoa maoni, kwanza na muunga ndugu yangu aliyosema aliposema kua sisi twataka Majimbo. Majimbo ni muhimu sana kwa sababu wenzetu wa Bara wao wana Majimbo. Bara uweze Mdigo au Mjomvu kuweza kusimama kwa mfano kama Councillor, au Mayor, au Mbunge, kwa hivyo Bara yako Majimbo. Isipokua Pwani ndio hiki twaimba tu lakini hakijakua twataraji inshalla Tume itakubaliana na sisi nasi tuwe na uwezo kama wenzetu wa bara walivyo.

Sisi watu wa Pwani hakika hatuna haki jambo lolote, watoto wetu wanasoma wakimaliza hawapati kazi, waweza kuketi, mtu yuwaja, yuakuuliza Kilidini ni wapi? kumbe ameagiziwa, ashaadikwa kazi na hiyo Kilidilini haijui, watoto wazaliwa hapa na hakuna kazi. Sisi watu wa Pwani watoto wetu leo washikwa bure, mtoto akishikwa lazima atoe kitu, kama hatoi kitu atolea bangi kua ashikwa na bangi. Kwa hivyo ni unyonge, juu ya unyonge. Twaiomba Tume iambie serikali ya Kenya watu wa Pwani wamechoka kunyanyaswa na sisi Waislamu simagaidi wala si wakora sisi. Waislamu kwa sababu taabu wanazo pata ndio zimefika hadi sasa vipao vyao vimechafuka. Vipao vyao vimechafuka, kwa hivyo nyuma kulikua kuna amani sababu ilikua haki yatekelezwa. Sasa haki haitekelezwi mtaona watoto wanafujo na nini kwa sababu ya nini? Haki zao hawapati. Twaomba Tume ifikirie maswala haya kwa makini sana na iambie serikali yetu.

Jambo la pili Madrassa za Kislamu hizi mtoto wa Kislamu ukiwa katika Madrassa zetu asiye jua Koran mtoto yule atakua muovu, atakua mwizi, atakua jambazi pengine, pengine atakua rabu za kamwe, sababu ya nini? Hana mbele hana nyuma. Lakini ndini itamfudisha kujua Mungu wake, ajua serikali yake, hata wazazi wake, na hata haki za binadamu. Kwa hivyo wale wafanya vituko vituko wale, sio Uislamu ule, ule uko nje ya Uislamu. Kwa hivyo sasa twaomba Katiba iwe sisi walimu wa vyuo katika Kislamu ni Vyuo ambavyo vina faida kubwa kwa vijana wa Kislamu na umma wa Kenya pia.

Na jambo lingine kuhusu Chief Kadhi; sisi Waislamu Koran ndio Katiba yetu. Kwa upande wa dini sisi hatuna hiari lazima tufuate Koran. Sheria za nchi twaziandama lakini Koran ndio roho yetu sisi. Muislamu yoyote mfano lau ahukumiwe ni Chief Kadhi. Akakose lahaka aitakayo, akienda mahakama isiyokua ya Kiislamu moja kwa moja yule si Muislamu tena. Kwa hivyo sisi twasema huu uwezo walompa Chief Kadhi wetu usiwe ni ndoa na talaka na miradhi. Chief Kadhi atambuliwe kama Judge Mkuu wa Kiislamu. Akipitisha yeye hukumu yake hakuna nyingine, hivi maanake Muislam ndio. Hataka hajitaganze kua mimi si Muislam kwa hivyo nasonga mbele.

Na mwisho nikimaliza ni habari ya wakfu Commissioner. Sisi Waislamu tuna mali chungu nzima hapa yetu. Lakini mali hino ya simamiwa na wasio kua Waislamu. Wasio kua Waislamu waitumia kwa haja zao. Umefika wakati sasa wale watangulia wanasuni waisimamie hile Commissioner pamoja na Chief Kadhi, na Chama Kikuu cha Maimamu na Supreme Council na ikiwezekania chama cha Walimu pia nacho kisishirikishwe kiwe kitaangalia maswala haya ili Wakfu Commissioner Waislamu wawe wamefaidi. Maanake lau watapata haki zao Waislamu unyonge ukiondoka wataweza kujenga maskuli yao, watoto wao

wataweza kusoma wakapata tabia nzuri bila taabu yeyote.

Na mwisho ni kwa serikali isidhamini wanyama kuliko wanadamu. Maanake wanyama wanaua ndugu zetu kwale, kulipwa kwao ni shilingi thelathini alfu ndio malipo yao. Munyama leo Kenya ana dhamani kuliko mwanadamu. Kwa hivyo serikali ifikiri mwanadamu ni bora kuliko munyama kwa hivyo munyama akiua wale waliokufiwa na mtoto wao wapatiwe kitu kizuri cha kuwaliwaza katika maisha yao. Kwa hayo machache na shukuru Tume hii na Mwenyezi Mungu atajalia tulio yasema haya mtayapeleka na yatafikiriwa kwa makini asante shukurani na salaam aleikum.

**Com. Ayonga**: Asante na tafadhali ikiwa unaweza kujiandikisha kule. Mwakoma Mwadoe. Sema majina yako na uendelee.

**Mwakoma Mwadoe**: Namwamkua, Prof. Ghai na wananchi hamjambo? Jina langu ni Mwakoma Mwadoe kutoka nyumbani ni Taita, na kaa Majengo Liberty. Na shukuru kwa kunipatia nafasi kitu nitazungumzia ni kupitia mpango wa kazi; Mpango wa kazi mimi nimeketi tangu ukoloni nimeona serikali ya ukoloni, nikaona serikali ya Kenyatta, na hii ya Moi, hizo serikali zote tatu nimeziona, lakini shida ambayo tulikua tukipata wakati wa ukoloni ilikua ni kubwa lakini kwa wakati huu.

**Interjection:** Com. Ayonga: Hebu tunyamaze tumsike huyu mzee.

**Mwakoma:** Kupitia ilipochukuliwa nafasi ya Rais Moi tukafikiria sasa ndio hiyo mipango waliiweka wataitekeleza tupate manufaa, lakini mipango ikawa inazidi kudidimia. Kenyatta alitawala vizuri lakini kufika kwa Moi pia akatawala vizuri, kidogo sijui ilitokea aje ikawa sasa mambo inazidi kudidimia, hata wananchi wote wengi wakanza kushangaa. Tulisema tutapata matunda matunda ikawa imedidimia.

**Com. Ayonga**: Sasa toa maoni.

**Mwakoma:** Maoni ni hii, maoni kitu mzuri kupitia kwa upande wa Rais, ingekua Raias apunguzwe nguvu. Kupita kwa Rais kupunguzwa nguvu iwe ikiwa, Rais pale awe akiruhusu watu wakiwa wabunge tuliowachagua siku hizi waenda kinyume cha sheria. Tunapo wachagua waende bunge hua siku ingine unasikia wabunge wamekua ishirini au thelathini, na wabunge ni mia mbili na kitu, hiyo kitu iondolewe. Ikiwa ni siku zote tumewaandika wawe wakifika katika bunge tuone wakifika katika bunge. Ikiwa siku ambao watakua hawatafika hata hiyo siku mshahara wasipate. Itakuaje sisi tunachagua watuhudumie halafu wao ni kwenda na kuchezea kazi na sisi watu wengine tunatafuta kazi. Hiyo ni point ya kwanza.

Point ya pili mishahara walio jiongezea wamejiongezia kinyume, itakuaje watoto bado ujawafanyia chakula halafu unajiongezea, je watoto hao watakula nini. Hiyo point yangu. Mswada ya habari ya arusi au habari ya kuoa. Siku hizi wanawake wanalia ati wamenyimwa haki yao. Ni kweli hiyo haki wanaosema wamenyimwa haki yao ni kama haki gani? Ikiwa ni habari ya uridhi, mwanamke anaolewa labda kutoka Kikuyuni ameolewa Taita. Haki yake itakua kwao au itakua kwangu? Kwa hivyo ni vizuri

nimeona haki ya mwanamke mahali ambao ameolewa ndio haki yake iko sasa ikiwa atakua atapata sehemu mbili kule ambako ameolewa na kule kwao je ule mwanamme ataridhi sehemu mbili namna gani? Hao atapata haki gani? Kwa hivyo maoni yangu ni kua wanawake wakijua riziki yake ni kwa mume wake, na uridhi ni kwa mme wake na kichwani pa ndugu yake ataridhi si wataleta ugovi? Ni upande wa hiyo maneno wataiyangalia.

**Com. Ayonga**: Mzee neno la mwisho?

**Mwakoma**: Neno la mwisho ni hili, habari ya mshahara, mshahara Raia tumeteseka, mshahara tumeteseka ikiwa wewe ni tajiri umeajiri watu wako hivi leo kufanya kazi ni kufa na kupona; haki hawapati kulingana na ile kazi yao wanafanya, unawanyanyasa je wafikiria wale watu wataangalia nyumba zao namna gani ikiwa utawanyanyasa? Hiyo jambo iondolewe ikiwa ni kazi ya kampuni, ikiwa ni kazi ya mtu binafsi ameajiri watu wake, imekua kama kampuni kulingana na elimu yake na kulingana na kazi yake awe akilipa mshahara yake kulingana na yeye pia angalie maisha yake mwenyewe. Yangu hayo ni ya mwisho machache tu.

**Com. Ayonga**: Haya basi enda kule ujiandikishe. Next ni Nehema Khoka, mama yale utakayotoa ni mapya au ni yale yale tu.

**Nehema Khoka**: Mimi? Ni mapya.

**Com. Ayonga**: Ikiwa ni mapya, endelea.

**Nehema Khoka**: Salaam aleikum maBwana na mabibi. Mimi jina langu ni Nehema Khoka ni mzee wa mtaa wa hapa Majengo ya Musa. Mimi nina mambo matatu lakini katika haya matatu nitashika hilo la tatu ambalo ni muhimu kwetu sisi Waislamu. Hilo la tatu laanza hivi, huku kotini tunako kwenda sisi Waislamu huenda tukaapishwa kwa msahafu, hule msahafu mwenyewe unaambiwa au umesema usinishike kabla ujawa na udhu. Leo tunakuta kwamba mtu anapewa ule msahafu ambapo hayuko tohara ambapo hana udhu. Hilo ni ukumu la Chief Kadhi, lazima alitilie mkazo neno hili.

Jambo lingine ni kuhusu hawa chokora. Chokara Mombasa yetu mimi nilipokua leo sasa na miaka arubaini na nane, Mombasa ilikua haina chokora tumeshangaa hivi sasa ukitembea kuanzia majengo mpaka kokote chokora wako wengi, je Machokora hawa wametoka wapi? Hili ni jukumu la serikali yetu pamoja na police pia ni serikali, waanze kushika hao watoto na wawapeleke makwao, ni urongo kua hawana makwao, na hao waomba omba pia washikwe wanatutia aibu. Leo hii unakuta kila kabila inaomba, ikifikia hile alhamisi watu wameanza kuzunguka na kuomba, ni jukumu la serikali kushika chokora na hao omba omba waondoke kabisha. Na ikiwa chokora ameshikwa, ama omba omba atiwe ndani nafikiri watapungua.

Kazi twanyimwa, lakini omba omba ndio tumeletewa kwa wingi pamoja na chokora. Sasa ni jukumu la serikali watafute hao watu kwao si hapa kwetu. Chifu na wazee wa mitaa wanawajua watu wao walio wazuri na wabaya, sio mtu kutoka nje yuwaja

mtaani na jina ni chokora ama Omba Omba. Mfano mwingine ni hao traffic wetu. Wanawanyanyasa madereva wetu wa matatu bure, kudai hongo na hali mshahara wanapewa, nao wachukuliwe hatua wakichukua ile mia moja kila trip sisi wamama tutakula nini. Sisi ikiwa ndio uchumi wetu;

Mombasa ilikua haina wezi kama hao wakisasa. Swaleh ama Omar alikua hajui kuiba benki, leo hii amefundishwa na mabingwa wa mabingwa nao wakajiunga pamoja sasa utamkuta Swaleh ameekwa, wewe twende tukaibe mahali fulani, atakaye kufa wakwanza ni Swaleh, yule fulani na fulani wao utasikia hao wamekimbia. Kwa hiyo jamaa tuwe macho na yatizamwe hayo maneno. Badala ya polisi kuchunga usalama leo anachunga hongo, methali ya kiswahili yasema, paka akiwa judge panya hawezi kushinda kesi, hata wakili akiwa ni mama. Sina mengi hela ni hayo.

**Com. Ayonga**: Unaweza kutoa maandishi yako kule na ujiandikishe. Muhamed Sheiba. Wakati Muhamed anaendelea nataka Halima Muhamed pia awe tayari. Halima kama yuko.

**Muhamed Sheiba**: Kwa jina ni Muhamed Sheiba, natoka katika mtaa wa Minazini, na tunawalikisha baadhi ya walimu wa Madrasa, na pia Nyota Njema na vijana katika mtaa wetu. Mengi yamezungumzwa ambao ningependa kuzungumza na natilia mkazo na nafurahia kua wenzangu wametaja habari ya stakibadhi au uraia. Uraia katika nchi ya Kenya ni jambo ambalo ni muhimu sana na sina haja ya kufafanua zaidi, lakini ningependa tu kukueleza kua kila Raia inatakikana awe anapata birth certificate, Identity card na passport bila ya kusubuliwa.

Tukienda katika point ya ubunge na wabunge ningemuunga mkono mwenzangu aliyesema kua ikiwa mbunge hakuhudhuria kikao, basi zile siku ambazo hakuhudhulia akatiwe allowance yake. Na mbunge yeyote ambaye atatumia cheo chake vibaya basi achukuliwe hatua. Tukija katika sehemu ya utawala, sote twapendelea Majimbo, na kila mtawala kuanzia ngazi ya chini mpaka ngazi ya juu awe ni mzaliwa wa sehemu ile ambayo anayoitawala, ili aweze kuwaelewa watu wake na aweze kuwatumikia vilivyo. Kwa mfano baraza la mji wa Mombasa wakati wa nyuma, kulikuako asilimia kubwa si ya watu wa hapa, ndio unakuta barabara nyingine zimetiwa majina ambayo hayaeleweki, barabara yaitwa Nyoka, barabara sijui yaitwa mambo ambayo hayaeleweki, lakini kama ilikuako wenyeji wale wanaongoza baraza ni watu wa hapa, basi majina labda ya kihistoria ambao wenyeji wa hapa wanastahili kupata majina kama yale wangepewa lakini kwa vile ni kinyume basi nenda kinyume. Majina ambayo hayaeleweki.

Na nikija upande wa polisi, tungependa wasishike watu bila hatia, na ikiwa watashika watu basi wasiwapige wala kuwasumbua. Wawachukue tu mpaka kituo cha polisi wawandikie zile hatua ambazo nizakisawa lakini wasiwapige. Kwa hivyo twapendekeza kua polisi wasiadhibu wananchi bila ya sababu. Na katika msako raia akitoa kitambulisho au barua ya kazi ama kadi basi iwe inatosha kua inamtabulisha kua yeye ni nani. Lakini asisumbuliwe, na ikiwa atapelekwa cell basi mshukiwa aruhusiwe kuasiliana na watu wake wa nyumbani ili apeleke mawasiliana maanake wale wasije wakamtafuata haijulikani yuku wapi kumbe polisi wamemzuia. Na katika vile vituo vya polisi tunaomba wenyeji wa Pwani au watakao simamia wasimamizi

wa kituo wawe ni wenyeji wa area ile maana kutakuwako heshima fulani ambao itapewana. Lakini ikiwa mtu ni mgeni basi mambo kama hayo yataharibika.

Katika mambo ya rasmali yamesemwa mengi, lakini tungependa kwa mfano KPA iko hapa tungependa courses ya KPA iwe Mombasa isiwe Nairobi kwa nini KPA iwe hapa na kazi zote hapa halafu tunapelekwa Nairobi. Mambo ya utalii pia ofisi iko Nairobi, mambo kama hayo si sawa.

Ardhi, masquater utakuta watu wengine wamekaa katika ardhi wao, babu zao, nyanya zao wao wamezaa hapo, wanavitukuu wajukuu, vitukuu, na bado ni masquater, mambo kama haya hayaridhishi. Na viongozi wakichukua ardhi za umma basi wachukuliwe hatua iwezekanavyo, maanake ardhi za umma zizuchukuliwe na zikapewa watu binafsi, isipokua zipawe wale wanaohusika katika miradi ya maendeleo lakini wasipewe watu ovyo ovyo.

Katika huru wa kuabudu Muislamu anaongozwa na Koran tukufu na hadithi yaani mafunzo ya mtume. Hivyo basi kwenda kinyume na mafunzo ya Allah ni kwenda kinyume na imani yake, mfano ni kua wakati mtoto wa kike anapobalehe yeye tayari huwa na sheria ya Kiislamu inambana katika sheria, inambana maanake katika mambo fulani. Inamaanisha kua, kwa mfano mavazi yake, yanatakikana ya msitiri mwili mzima, kwa hivyo kuna baadhi ya shule hairuhusu watoto wa Kiislamu wa kike kujistiri na hii inakiuka mipaka ambao sheria za Mwenyeji Mungu zinaweka. Kwa hivyo twaomba ule uhuru wa kuabudu usiwe ni kwenda Msikitini peke yake, ni kila pahali. Muislam sheria inamfuata kwanzia na kwamka mpaka anapo kwenda lala na ni kila siku, kwa hivyo twaomba zile shule wawaruhusu watoto wa Kiislam ku-practice their religion wherever there are, kama wakati wa kufunga waruhusiwe kufunga, kuna shule zingine hawaruhusu watoto wa Kiislam kufunga, kwa vile wasema ni boarding school, au mambo kama hayo, hakuna, kwa hivyo ningeomba sheria za Kiislam zitumika mpaka katika shule.

Na kuna hivi karibuni viongozi walisema kua msichana asiolewa akiwa na miaka kumi na tatu, sasa watoto wetu hawa tunavyowajua jamani ikiwa mtu atakuja atamsiri atamuoa mtoto kama yule itakua ni bora kuolewa ama aachwe warange range azae ovyo nje. Sheria ya Kiislamu inasema mtoto wa kike akisha vunja ungo akiwa amekuja mto amemposa aolewe. Kwa hivyo sisi tutakataa kusema tutamzuia kumwoza mtoto kama yule itakua ni hasara kwetu, maanake mambo ya friendship haya tunayaona tumeona the Bold and the Beautiful na mengineyo, mambo kama haya yanawatatiza watoto wetu na nijukumu la serikali kuona vipindi ambavyo wanavileta katika runinga zetu wanazi censor, wasilete vitu vyote maanake mambo kama haya yanachangia katika watoto wetu kuharibika.

**Com. Ayonga**: Hebu malizia malizia.

**Mohamed Sheiba**: Kuhusu mambo ya Ukimwi, hivi karibu tulikuwako na workshop, tukasema kua kwa nini hao watalii wakija hawafanyiwi blood test kabla hawajaruhusiwa kuingia hapa. Wao wanakuja hapa wanaeneza ukimwi, halafu wanarudi makwao salama salamini halafu huku serikali inapoteza mamilion ya pesa tukisema sisi tunachunga mambo ya ukimwi usienee.

Vipi usienee na wao ikiwa tutaruhusu ma-bar, turuhusu watoto wa kike wanafaa mavazi na mambo ya kisherati yanaendelea bila ya kuchukua hatua na serikali ndio inatoa leseni, kwa hivyo wazuie leseni katika mambo kama haya ya madisco na mambo kama haya hili watoto wetu wasalimikie, lau kama sivyo mambo yataendelea. Point yangu ya mwisho Bwana mwenye kiti kusema la kweli, mwanamke katika sheria za Kiislamu analindwa sana, mwanamke katika sheria ya Kiislam hapiki hapakui, hafui wala hana ruhusa ya kupigwa, kwa hivyo tunapendekeza sisi wanawake wetu wa Kiislam na hasa wengine pia tunaweza kuwatia hapo not to be ruled na sheria nyingine waruhusiwe katika mada ile ya Kiislam. Na mwisho kabisa kabla sijaondoka tungepende kua mambo kama haya yanatekelezwa vilivyo. Hii memoramdum nitaitoa kule. Ningependa kusema mambo mengi lakini wakati ndio hakuna.

**Com. Ayonga**. Tafhadali enda kule ujiandikishe.

**Salim Abdirishak Badamana**: Mimi kwa jina naitwa Salim Abdirishak Badamana, mimi nimekuja kutoa maoni wala sikuja kubadilisha sheria, katika maoni yangu mimi naona Katiba yetu ya Kenya iliotuongoza kwa miaka thelathini na nane au miaka thelathini na saba ni Katiba ambayo ni nzuri sana. Na tena, katika Afrika hakuna Katiba ambayo ilitungwa sawa sawa na viongozi wetu na wale ambao wakoloni wetu ambao wametupangia na nawanasiasa wetu isipokua kwa bahati mbaya tuliingiliwa na pepo mbaya.

Pepo mbaya hao ni mahasidi ambao walifuja mali ya umma, wakajitungia masheria ya juu juu kulingana na matakwa yao, kulingana na haja zao, hadi leo Kenya tumefungiwa milango ya kigeni, hatupati misaada, mahosipitali yetu yamefungwa mtu amefika katika university amesomeshwa na pesa za umma ushakua na degree, umesomeshwa ni account ya serikali, umeshidwa kuendesha huduma za wananchi. Lawama inakuja baadaye tunasema serikali, serikali, kwa hivyo Bwana mwenyekiti, kile ambacho mimi nataka kutao maoni hapa, ni kua mwananchi apewe uwezo, ambao akiona dalili yoyote ambayo inazorotesha ama inadhoofisha uwezo wa yule mtu ambaye ameapishwa kuhudumia; kiapo ambacho amekula katika utumishi ambao amepewa madaraka katika serikali iwe ataweza kuhukumiwa, na kama hakuna hukumu ya kumhukumu yule mtu, Tume yetu na wala si sheria yetu itungwe sheria ambayo anaweza kufungwa commissioner wa polisi ikiwa barabara ya Makadara watu wanakojoa, na sheria ya kukojoa naambiwa si sheria, na polisi wakipiga patrol, na mtu ana pita pale anakutwa mikojo na mavi tele, yule Commissioner ambae anahusika pale iwe anaweza kuhukumiwa kwa nini uchafu huu umetokea. Nimetaja kitu kama mkojo kwa sababu ndio kitu ambao ni kidogo, lakini natoa mfano kwa wale ambao wameapishwa kuchukua daraka la serikali kuhudumia wananchi. Vile wanaifanya kashfa Katiba yetu na haki mwisho wamekua ni mahasidi wataka kuangamiza Katiba ambayo inatuongoza kwa miaka yote.

Pili sisi tumebahatika kuona Katiba kwa sababu Katiba yetu peke yake imetuongoza sisi tuonaongozwa na Mungu. Hata bendera yetu inasema “eh Mungu nguvu yetu, ilete baraka kwetu”. Sasa ikiwa sisi wenyewe kwa wenyewe ni mahasidi, wa Kenya ni mahasidi Mkikuyu akimwo Mkamba kesho atapigwa na panga kwa sababu ya ardhi, umoja uko wapi? Mungu yuko wapi Muislamu, Mkristo kesho imekua fujo, kwa sababu ya urasmi, siyo taifa hiyo nataka tuongoze tuwe na umoja

tutaipata wapi? Kwa hivyo naomba Kamisheni hii mchunguze haya mambo mashehe, na pastor, na padri waitwa ili watoe sauti yao yao kwa nini kue na mgawanyiko badala tuwe na taifa moja tumekua mahasidi wenyewe kwa wenyewe. Hiyo ndio ituongoza tuwe na taifa la kudumu, taifa ambao Muislamu ataabudu ijapokua taifa letu umetupa uhuru wa kuabudu.

Leo Muislamu anashindwa kujua uhuru wake wa kuabudu, hakuna mtu alienyimwa asifanye maendeleo, hakuna mtu asiyejua bustani yake asiogelea na nguo tupu, kaogelea na nguo refu, na mwingine akawa ameogelea akavua saa ni bahati yake. Kwa hivyo tushikane, na Bwana Kamishena nakuomba Katiba yetu ni nzuri, isipokua zile sehemu ambazo zimekua stilted muende mkaziambue, kwa sababu vifungu vingi ambao vinatupa haki sisi wananchi, na wale ambao wameapishwa kulingana na degree zao na diploma zao na wamepewa ofisi kwa manufaa yao, na ikiwa wao na uhasidi wao na mapepo yao ya kutaka anasa, walienda wakazibadika cellotape kua hii sasa imepitishwa na bunge kwa hivyo si sheria. Kwa mfano wewe mtu kiongozi una mali yako unachukua msichana wa mtu unakwenda kumtia mimba huko, kisha ule mtu unamwambia mtoto si wangu mimi, kwa sababu, na sisi tunasema mtoto yeyote mzaliwa Kenya ni wa Kenya, kisha tunasema huyu mtoto hana baba, hakuna aliyezaliwa ambaye hana baba duniani. Kwa hivyo utaona mtu kama yule ni mheshimiwa vile anaweza kupitisha bunge sheria ile kua mtu ambaye amezaliwa ikiwa hajaolewa ni out of wedlock kwa hivyo hana haki kwangu mimi ni Waziri niko na mashamba yangu mtu amepita njiani amchukue mara moja lakini hajui madhara ambayo ameletea taifa.

**Com. Ayonga**: Kwa hayo machache naomba mturekebishie Katiba ambayo tutakaa kwa upendo na amani na ustawi. Asante.

**Com. Ayonga**, (inaudible) uende kule ujiandikishe.

**Com. Ayonga**: Kuja hapa mzee.

**Salim**: Ndugu Makamishena na waliohudhuria hapa nyote, asalamu aleikum, nimepata dakika mbili peke yake, kwa heshima ya Kameshina, kwa hivyo sitaweza kuzunguza yote ambayo ningependa kuyazungmza leo ambayo nilikua nimebakisha lakini nitajaribu mawili au matatu tu, na yale mengine nitafanya bidii nitafute angaa shilingi mia tano nipate typist atengeze niwa-postie kule Nairobi.

Sasa naomba Kamisheni hii ikubali kuweka page moja, pande mbele kabla ya Katiba yao, waeleze kwa nini tumepata hii Constitution Review Commission, tulikua na bunge letu term saba kwa miaka mitano, wabunge hawakutuletea kitu kama hiki tunacho kipata leo Kenya. Kuna sababu iliyo sababisha tukapata hii Constitution Review Commission, sijui ni Saba Saba, ni nani, wengine walikua Matyrs walikufa wakapigania mpaka ikatoka hii. Naomba historically itolewe hata kama ni page moja kuonyesha kitu gani kimesababisha mpaka ikapatikana hii. Iwe kama kumbu kumbu ya wale walitoa roho zao ili hii tuweze kupata fursa hii Kenya leo.

La pili, napenda kuzungumzia habari yenu Commission nyinyi kwa heshima, kumetokea maneno mengi kua mnapata pesa nyingi sana labda wanasema 4 billion na kumekua na complain hapa na pale. Lakini kwa hesabu ninaona kwamba mbunge anapata, na naweza kua nimekosea, laki nne, wengine wanasema laki sita kwa mwezi, kwa bunge mmjoja anapata million saba laki mbili kwa mwaka, wabunge mia mbili wanapata karibu billion moja na million mia nne kwa mwaka.  Kwa miaka mitano wanapata billion saba point mbili, vipindi vitano wamepata pesa kama hizo ingawaje kule nyuma zilikua ndogo, lakini kwa ile exchange factor wamepata billion nyingi sana.  Kwa hivyo wale wameshindwa kutuletea kitu Kenya kama hiki leo, ambacho tunakipata Review Commission kutengeza Kenya mpya, katiba mpya, ni na hisi kwamba billioni nne mlizopewa, ingawaje zaonekana nyingi, ni ndogo kulingana na yale mabillion mengi yanayotumiwa na bunge ambao hawakutufanyia kazi yoyote Kenya isipokua kutuharibia uchumi na kuharibu jamii yetu.  Ningeomba kama wananchi wenzangu wataishidikiza bunge iwapatie angaa, billion moja ama mbili zaidi ili Civc Education ifanyike hata kama si nyinyi watakao kuja baada yenu, waweze kuendelea na continous Civic Education mpaka kila mwananchi wa Kenya aelewe haki zake kikamilifu.

Jambo la mwisho, napenda kusema, mwisho wa hii Katiba ni nini, utakua vipi?  Je leo tunaweza kuangalia mwisho wake, tunaweza kua na vision tukaangalia mwisho itakua vipi?  Katiba tunayo Kenya, kwingine kunaupungufu lakini ina sehemu nyingi zilikua nzuri, shida ilikua utekelezaji wa ile Katiba, tuna guarantee gani, kwamba yale mamba ambao wananchi ya Kenya leo wanayaoyasema kweli yatafanyika.  Enforcement ya ile Constitution Mpya kama itapatikana, kutoka leo haijajulikana kama itakua, tunaweza kusikia kesho radio KBC imevunja wote rudini nyumbani.  Inaweza kufanyika. Lakini ikiwa itafanyika, enforcement methodology, ili mwananchi wa kawaida aweze kupata haki yake kulingana na hiyo Katiba itakayo kuja; On the spot asiwekwe miaka kumi, anangonja kotini kutafuta haki yake ya Katiba, iwe explicit, watu waifahamu, iwe rahisi, iwe cheap sina haja kutafua wakili elfu hamsini kwenda kutafuta constitutional court iwe constituted.  Tena naomba Katiba hii iweke, hatuna haja ya kwenda kwa Chief Justice atuletee constitution of the constitutional  court; kuwe na full time constitutional court in every province and every district nikiwa na shida ya constitution saa hiyo hiyo napata haki yangu.  Kwa hayo machache kwa sababu nauona pale muda wangu ni mchache, asanteni.

**Com. Ayonga**:  Twashukuru, tafadhali hayo maadishi yatoe kule na uende uweke sahihi yako.   Sasa wa mwisho na nitamwomba atuwie radhi kwa sababu wakati ni mchache, ni Mzee Mwinyi Kombo Salim.

**Mwinyi Kombo Salim**:  Salaam aleikum, nitaanza kwa jina la Mwenyezi Mungu kwa sababu sisi Waislamu lazima tufikishe kwanza Mwenyezi Mungu mbele.  Nataka kuunga mkono kidogo sheria ya Kadhi.  Kwa upande wa Kadhi, Makadhi ni wachache, vile vile kuna Kadhi na Chief Kadhi na huyu Chief Kadhi anachukuliwa kihivi hivi, lakini kunatakiwa yule Chief Kadhi awe ndio Kadhi mkuu yaani ni kama Chief Justice, kwa sababu hiyo ikiwa mtu anaona anaonewa kwa mfano katika rufaa, hii koti ya kanuni kuingilia mambo ya Kislamu si haki kwa sababu haiwezi kabisa kusubutisha mambo ya noradhi ya Kislamu.

Yengine, ni upande wa sheria. Sheria Bwana mwenyekiti ilioko kwa sasa haitufai: Sheria ilioko kwa sababu sasa hivi hata mbunge pia wametutupa, mimi ninavyo kubuka bunge ikiwa kunataka kupitishwa msaada wowote, yeye anarudi kwa raia kuja kuwazungumzia yale mambo ambayo yatakiwa yapitishwe kule bunge. Lakini mbunge utamwona kwa jambo kama hilo zile siku anazozitaka kura, basi tu, utamwona tena mpaka siku nyingine ambao tena anataka kura. Kwa hivyo wabunge wanatukosea, mimi mwenyewe nilikua nikifanya kazi Port nika-retire, kwa sababu ya kusema sheria haziridhishi, kuna wakati tulikuja tukaunganisha baina ya cargo na KPA, wakati huo sisi hatukushauriwa, order ilitoka tu moja kwa moja kwamba atakaye kua mwandishi hapa bandarini ni fulani. Hili jambo tuliendelea nalo lakini kwa shingo upande, mambo kama hayo Bwana mwenyekiti yanavunja watu moyo sana, kwa sababu lazima raia wa nchi hii apewe haki yake yakuchagua yule anayemtaka.

Na watu wengi wa Pwani tukija hapa sisi twalalamika kwa sababu ya Majimbo, watu wengi wafahamu swala la Majimbo kimakosa wanaona labda ni kufukuza watu wa Bara, au pengine Majimbo yatakua ni ya watu wa Pwani peke yake, la si hivyo, Jimbo tunalolitaka ni lile lilokubaliwa kutoka Lancaster house kwa sababu vyama vilivyo kuja na uhuru hapa Kenya ni vyama ilikua nafikiri ni viwili, baina ya Kanu na Kadu, na wakati huo Kadu ilikua nikama iliruka sakafu kwa maelewano baina ya Chama cha Kanu na Kadu. Maeleano yao kwamba hawa waingereza au tuseme wakoloni walikuja wakatutenganisha kwa hivyo sasa afadhali sisi tuwe na chama kimoja na tukakubaliana tukawa na chama kimoja, lakini ukiangalia chama kimoja hiki kinamanufaa kwa upande mmoja. Chama kimoja kinamanufaa kwa upande moja, na manufaa ya upande mmoja ninayosema, tukija upande wamashirika utaona watu wakibara watupu, hii si ukabila, maanake ndivyo ilivyo. Hatuwezi kusema kua ni ukabila watu wa Kibara watupu wameanza kutoka juu mpaka chini kwa sasa, mimi nikitoka Port, ilikua tuko karibu sawa sawa hamsini, kwa hamsini lakini hivi sasa hivi nafikiri watu wa Pwani waweza kuwapata labda ni kama watu watano tu kwa mia. Hii ndio sababu sisi tunapigania Majimbo, na Jimbo lenyewe liwe na uwezo wa kujitegemea, iwe kuwe tutakua tuna asilimia kama thamanini kwa mia, tuwe tukimiliki sisi wenyewe ardhi.

Na tatizo lingine ambalo linasumbua watu wa Pwani, ni la Uraia, huu Uraia, mimi sioni kama unasumbua sana isipokua watu wa Pwani wanatabia za kuficha ficha zile asili zao, huu ndio ukweli. Mtu hataki kujitaja yeye kua mimi, Mwinyi Kombo Salim jina langu aona shame. Na ikiwa utajitaja tu Ali Athumani Omar, lazima uonekane na una asili ya kiarabu, sasa ukioneka una asili ya kiarabu ukiulizwa ulizwa, mwarabu lazima asili yake atoka nje, namna itakavyo kua, ni watu ambao tumeoana nao, ndugu sisi sote kwa sababu tuliowana nao, lakini lazima mtu ajitakase katika kujieleza ile asili yake, sijue kwa nini watu wanaongopa na huu utumwa ulishaondoka kitambo Bwana. Sijui kwa nini wata wana haya na jambo kama hilo. Kwa hayo machache Bwana Mwenye kiti naona nikomee hapo.

**Com. Ayonga**: Nashukuru kwa maoni ulio toa tafadhali uende kule ujiandikishe. Ndugu na dada ambao tumekua nao hapa leo, na jana, tumekua na siku ambazo ni mzuri sana za kuchukua maoni ambayo mmetupa. Ni maoni ambayo ni ya watu wazima. Maoni yanayotaka kurekebisha na kutengenezwa Kenya yetu hii, iwe Kenya iliobora, si Kenya ya ukabila, si Kenya ya kuweka watu wengine kando na kufanya mambo mengine kando ambayo wote hawahusiki. Tunataka Kenya ambayo kila

mmoja anajisikia yuko kwao Kenya, na pahali popote ambapo mtu yuko, yuko katika ya ndugu na dada na yuko katika Kenya. Na katika uchumi, uchumi wote ulioko, mali ya asili iliomo ni yenu tusiwe na maskini, tusiwe na tajiri ambao hawezi kugawa mali yote; tuwe tukitumia sote ambavyo Mungu ametubariki nayo. Na kwa hayo nataka kuwashukuru tena. Bado tungali hapa Pwani, na tutaendelea kuona watu ambao wako, (inaudible) na kuja kwenu kumekua vizuri sana kwa maana hii nyumba inaenda inakajaa kama mawingu, unaona hayo, hayo, nyumba imejaa. Halafu tukienda kumaliza wengine wakaenda na wengine tena wakarudi na tunaona tuko hapo baada ya saa kumi ni moja hii inaonyesha moyo tulio nayo na jukumu ambalo tutataka kuona kwamba Katiba yetu imerekebishwa. Asubuhi tulipoaanza mkutano tulianza kwa kuomba baraka ya Mwenywezi Mungu, nilisikia vizuri sana mzee moja alipo sema kwamba nchi yetu hii tunasema kwanza "eh Mungu nguvu yetu." na kama mungu ndio alitupatia nguvu zetu asubuhi na akatuleta salama salamini Mungu huyo huyo tutafunga naye mkutano, tumshukuru kwa wema wake na pia nguvu hizo ziende pamoja nasi na atulinde. Unajua badiliko la mtu linatoka moyoni, si badiliko la nje; kwamba kitu ambacho tuliombea. Je Katiba hii kweli itakwisha hau itaenda itafikia hapo na tukaanza kusika kwa radio kwamba Katiba ilisimamishwa? Yote hayo tumweleze Mwenyezi Mungu yeye anajua yaliyo mbele, na anajua yalimo ambao sisi hatujui. Mambo yalio mbele ya watu sisi hatuwezi kujua, lakini nia zetu na nyoyo zetu ni kurudia yule ambaye ni Mwenyezi, ili mapenzi yake yatendeke na jina lake litukuzwe kwa kila kitu. Kwa hivyo nawaomba zote tusimame kwa maombi ya kumaliza huu mkutano hebu na tuombe.

**Prayer: Com. Ayonga**: Mungu Baba wetu ulie juu mbinguni, Mungu Mwenyezi, ulituumba, na ulitupa nchi hii nzuri, twaomba fahari na vyote vilivyoko, tuko hapa katika mwambao wa Kenya hapa katika Coast Province, tumekua na wana na binti zako ambao wamekuja kutoa maoni yao, Mungu tumeona tuna shida, lakini shida zingine nizile ambazo binadamu tumezijenga sisi wenyewe, tumejenga shida zingine kupitia choyo tulio nayo, choyo ambayo hatufikiri zetu, choyo ambayo hatufikiri masilahi ya wengine, tunaomba kwamba utupe moyo ule wa utu ili tuweze kuhurumiana, tuweze kutendeana vizuri kwa maana tukipenda mwenzetu na pia kutaka mwenzetu atendewe tunavyo taka sisi tutendewe. Tunaomba tukiamini kwamba yote haya yatafanyika. Hebu tuombeni na wale wanao tuongoza wabariki na pia uwape hekima ya kuweza kutatua yale ambayo ni magumu, na uwape macho ya kuona yale ambao hawayaoni, ili tunapofanya kazi ya kutengeneza Katiba na kuirekebisha Mungu tunaomba kwamba jina lako lionekane katika hii Katiba. Kwa maana jina lako likionekana, Katiba itakayotengenezwa na kurekebishwa itakua ile ambayo italeta utukufu na wote mtapata nehema na rehema zako kupitia kwa hii Katiba; kwani tunaomba tukikuamini. Amen.

Meeting ended at 5.30 p.m.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&